SUPA JACKPOT
TZS. 1,058,211,696
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



UKURASA 3

**BALOZI** wa Tanzania Austria alivyoteketea kwa moto ajali ya gari




UKURASA 13


# Nipashe

Ijumaa Desemba 16, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581161

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US


# Siri ya walimu mikopo umiza




UKURASA 2




Abiria wakipanda kwenye mabehewa mapya ya treni katika stesheni ya Dar es Salaam jana kwenda mkoani Kigoma. **Habari ukurasa wa 4. PICHA: JAMES KANDOYA.**

## Majaliwa awaanika vigogo, awakabidhi TAKUKURU

UKURASA 16

## Bil. 697/- WB kuongeza maji, nishati vijijini

UKURASA 2

**MICHEZO** **YANGA YAKIRI IPO KUNDI GUMU CAF** UK. 32

**KATUNI** UK. 6

# Bil. 697/- mkopo wa WB kuwanufaisha wananchi maji, vyoo

**Na Maulid Mmbaga**

BENKI ya Dunia (WB) imeidhinisha ufadhili wa ziada ambao unatarajiwa kuwanufaisha Watanzania milioni 10 kwa kupatiwa huduma bora ya maji na wengine milioni tisa watakaopata miundombinu bora ya vyoo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Mkurugenzi wa Benki hiyo Tanzania, Malawi, Zambia na Zimbabwe, Nathan Belete, ufadhili huo uliidhinishwa juzi.

Sambamba na hilo, taarifa hiyo inabainisha kuwa mkopo mpya wa dola milioni 300 (Sh. bilioni 697) wa Shirika la Maendeleo la Kimataifa (IDA) na ruzuku ya dola milioni 4.9 ya Mpango wa Usaidizi wa Sekta ya Nishati (ESMAP) kwa ajili ya Programu Endelevu ya Ugavi wa Maji Vijijini na Usafi wa Mazingira (SRWSSP), itasaidia upanuzi wa programu hiyo kutoka wilaya 86 katika mikoa 17 hadi wilaya 137 kwenye mikoa 25 nchini.

Mkurugenzi huyo alisema ufadhili huo utawezesha shule za msingi za umma 1,850 na vituo 2,600 vya huduma za afya kufikiwa kwa kuboreshewa huduma za usafi wa mazingira na utasaidia pia majaribio ya skimu 206 za maji ambazo zitajengwa chini ya mipango ya umma na ya kibinafsi.

"Tunatiwa moyo sana na matokeo ya ufadhili wa awali wa programu ambayo zaidi ya watu milioni 3.3 walipatiwa huduma ya maji bora na maendeleo makubwa katika upatikanaji wa vyoo kwa kaya, shule na vituo vya afya.

"Huduma hizi zinakuza mtaji wa wananchi na ushirikishwaji wa kijamii, kwani zinasaidia kukomboa wakati wa wanawake kwa ubia wenye tija na pia kuboresha utendaji wa wanafunzi," alisema Belete.

Aliongeza kuwa mkopo wa awali wa dola milioni 350 kwa ajili ya SRWSSP, uliidhinishwa Juni 2018, lengo likiwa ni kuongeza upatikanaji wa huduma ya maji na usafi wa mazingira vijijini kwenye wilaya zinazoshiriki na kuimarisha uwezo wa taasisi za sekta teule ili kuendeleza utoaji wa huduma.

Mtaalamu Mwandamizi wa Ugavi wa Maji na Usafi wa Mazingira wa WB, Ruth Kennedy, alisema kasi na ukubwa wa matokeo ambayo yamefikiwa na programu ya wazazi inaweza kuhusishwa na sababu kadhaa na kwamba muhimu zaidi ni kuanzishwa kwa RUWASA.

Pia alisema ufadhili huo wa ziada unasaidia mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Maji wa Serikali (WSDP) awamu ya tatu ambao ulizinduliwa mwaka huu na utaendelea hadi mwaka 2025.


DRC DANISH REFUGEE COUNCIL

17197502

TANGAZO LA ZABUNI

SHIRIKA LA KUHUDUMIA WAKIMBIZI LA DANISHI LINATARAJIA KUINGIA MKATABA WA KAZI ZIFUATAZO

1. RFP-PA-004-DRC-2023-2024 FLIGHT TICKETING
2. ITB-PA-005-DRC-TZA-2023-2024 VEHICLE SERVICING
3. ITB-PA-002-DRC-TZA-2023-2024 ASSET AND EQUIPMENT
4. ITB-PA-001-DRC-TZA-2023-2024 CORE RELIEF ITEMS

HIVYO SHIRIKA LA DANISHI LINATANGAZA ZABUNI TAJWA HAPO JUU NA WAZABUNI WAFUATE MAELEKEZO YAFUATAYO.

- USIFUTE KWENYE BEI
- USITUMIE WINO WA MAJI KUSAHIHISHA UNAPOFANYA KOSA.TUMIA KARATASI MPYA
- USIBADILISHE KARATASI ZA ZABUNI KWENDA KWENYE MFUMO WORD/EXCEL,
- ZINGATIA SEHEMU ZA KUSAINI NA KUGONGA MUHURI AMBAZO NI LAZIMA
- USISAHAU KUAMBATANISHA NYARAKA ZINAZOHITAJIKA KAMA VILE KIAMBATISHO A.1, KIAMBATISHO A.2, CHETI CHA KUKUBALI TUZO YA ZABUNI NA KANDARASI, WASIFU WA MUUZAJI NA FOMU YA USAJILI, HALI YA MKATABA WA JUMLA WA DRC, MAELEZO YA KAMPUNI, KANUNI YA MWENENDO WA WASAMBAZAJI WA DRC BAADA YA KUMALIZA SEHEMU ZOTE KAMILI, SAINI, GONGA MUHURI, WEKA TAREHE.

KWAHIYO SHIRIKA LA DANISHI LILILOPO KIBONDO LINAWAARIKA WAZABUNI KULETA BEI ZAO.

NYARAKA ZA KUJAZIA BEI ZINAPATIKANA KATIKA OFISI ZA DANISHI KIBONDO KUANZIA TAREHE 16.12.2022 HADI TAREHE 29.12.2022 SIKU ZA KAZI SAA 2:00 ASUBUHI MPAKA SAA 10:30 JIONI. TUNAPATIKANA BARABARA YA IRC KIBONDO.

KWA MAWASILIANO ZAIDI PIGA 0625482649 au BARUA PEPE sadock.kabuko@drc.ngo

ZABUNI ZITAFUNGULIWA HADHARANI TAREHE 30.12.2022 SAA 4:00 ASUBUHI OFISI ZA DANISHI KIBONDO NA KAMATI YA KUFUNGUA ZABUNI.

UNAWEZA KURUDISHA ZABUNI KUPITIA RFQ.TZA@DRC.NGO AU KULETA MOJAKWA MOJA OFISINI VINGINEVYO NI BATILI.




Balozi wa Tanzania nchini Zimbabwe, Simon Sirro (kulia), akisalimiana na Rais Emmerson Mnangagwa, alipofika nchini Zimbabwe kuwasilisha hati za utambulisho jana. **PICHA: WIZARA YA MAMBO YA NJE**

# Siri walimu mikopo umiza

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

CHAMA cha Walimu Tanzania (CWT) kimesema ili walimu waondokane na mikopo umiza na inayowafedhehesha, ni vyema serikali ikaomba benki zishushe riba ili kuwapa unafuu.

Akiwasilisha risala ya chama hicho jana kwenye Mkutano Mkuu wa CWT, Kaimu Katibu Mkuu, Japhet Maganga alisema: "Serikali iombe benki mbalimbali kushusha kiwango cha riba kinachotozwa na benki katika mikopo ili kuwapa unafuu walimu na watumishi wengine kutojiingiza katika mikopo inayofedhehesha."

Mbali na riba za benki, walimu wamekuwa wakikimbilia kwenye mikopo umiza ili kuukwepa utaratibu wa kisheria unaozuia makato kwenye mshahara wa mtumishi kutozidi theluthi mbili ya mshahara.

Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa Mwaka 2019/20, mbali na mambo mengine, imebainisha ukiukwaji wa kanuni katika ulipaji wa mishahara ya watumishi kutokana na mikopo waliyonayo.

CAG anafafanua kuwa Kifungu cha 3 cha Sheria ya Maofisa Waliobainishwa (Urejeshwaji wa Madeni) Sheria Na. 7 ya Mwaka 1970 kama ilivyosisitizwa na Mwongozo wenye Kumb. Na. 26/46/01/1/66 wa tarehe 28 Novemba 2012, watumishi wanatakiwa kulipwa si chini ya theluthi moja ya mishahara yao ya kila mwezi.

"Kama ilivyooneshwa katika ripoti zangu za miaka iliyopita, bado kuna watumishi wa umma ambao mishahara yao ya kila mwezi inapunguzwa zaidi ya 2/3.

"Uchambuzi uliofanywa katika Mamlaka 35 za Serikali za Mitaa ulibaini watumishi 3,038 waliokuwa wakipokea chini ya 1/3 ya mishahara yao," anasema.

Katika hilo, CAG ana angalizo kwamba utaratibu huu wa kukopa usiodhibitiwa unaweza kuathiri utendaji wa watumishi na kuathiri utendaji wa jumla wa Mamlaka za Serikali za Mitaa.

"Nilibaini kuwa hali hii ilichangiwa na ulipaji wa deni la Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ambalo hutoza asilimia 15 ya mshahara wa mtumishi ambaye ni mnufaika wa mkopo.

"Katika hali isiyo ya kawaida, pia nilibaini watumishi wanane (8) katika Mamlaka sita za Serikali za Mitaa ambao kila mwisho wa mwezi hawapati kiasi chochote cha mshahara.

"Mamlaka hizo na idadi ya watumishi ni Halmashauri ya Jiji la Arusha (1), Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto (1), Halmashauri ya Wilaya ya Njombe (1), Halmashauri ya Manispaa ya Temeke (1), Halmashauri ya Wilaya ya Rombo (3) na Halmashauri ya Wilaya ya Same (1).

"Ninapata wasiwasi na ustawi wa watumishi hawa katika kupata mahitaji yao muhimu kama vile chakula, mavazi na malazi," CAG Kichere anatahadharisha.

Katika risala ya CWT jana, Maganga pia aliiomba serikali kuona uwezekano katika bajeti ijayo kutoa nyongeza ya mshahara itakayoendana na gharama halisi ya maisha.

Pia aliishauri serikali kuongeza kasi ya ujenzi wa nyumba za walimu ili kuendana na kasi ya ujenzi wa vyumba vya madarasa.

"Kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2022 kutoka Ofisi ya Rais TAMISEMI, Taifa lina jumla ya walimu 274,901 wa shule za msingi na sekondari na nyumba za walimu zilizoko ni 59,417 tu sawa na asilimia 21.6 ya mahitaji," alibainisha.

Alifafanua kuwa walimu 215,484 sawa na asilimia 78.4 hawana nyumba.

Aliiomba serikali kuongeza kasi ya kulipa madeni ya mishahara yaliyolimbikizwa kipindi cha nyuma ili kuendana na mfumo mpya wa sasa (HCMIS) kwa kuwa athari za kutofanya hivyo ni kubwa hasa kwa walimu ambao wamefikia umri wa kustaafu na wengine tayari wamestaafu kabla ya kulipwa madeni.

**ONYO MAKUNDI**

Katika hatua nyingine, serikali imeonya makundi yanayoendelea ndani ya CWT na kuagiza kama kuna hoja ziwasilishwe ngazi husika ili kushughulikiwa.

Inadaiwa kuwa ndani ya chama hicho kwa muda mrefu kumekuwa na mvutano wa makundi yanayounga mkono uongozi ulipo sasa na ule ambao viongozi wake walisimamishwa kwa sababu mbalimbali ikiwamo matumizi mabaya ya madaraka.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako, akifungua mkutano huo kwa niaba ya Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, alisema:

"Nimepewa taarifa kuwa ndani ya chama hiki kuna tatizo kubwa la makundi kwenye hili niseme bila kupepesa macho serikali haitavumilia hili liendelee, kwa kuwa walimu ni kioo cha jamii, hatutegemei kufanya mambo kinyume cha maslahi yenu."

Kuhusu kuvuja kwa mitihani, aliagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) na Jeshi la Polisi kuchunguza matukio yote ya aina hii na kuhakikisha wanafikisha wahusika wote kwenye mikono ya sheria.

Kuhusu madeni ya walimu, aliwaomba wawe wavumilivu wakati serikali inaendelea kuwalipa huku akibainisha hadi sasa walimu 88,297 wamelipwa Sh. bilioni 117.6.

Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Willy Komba, alisema licha ya mpango mzuri wa kuhakikisha watoto wote wanapata elimu iliyo bora, kumekuwa na tatizo la ongezeko la idadi ya wafunzi shuleni kulinganishwa na idadi ya walimu, hali inayosababisha walimu kuwa na mzigo mkubwa wakati wa ufundishaji.

## HABARI KITAIFA

# Serikali yatoa tamko mwekezaji kuchoma vifaranga

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

SAKATA la mwekezaji wa shamba la kuku wa nyama na mayai mkoani Kilimanjaro, kuteketeza kwa moto vifaranga 50,000 vya kuku kwa madai ya kukosa soko, limechukua sura mpya, baada ya serikali kusema inakusudia kuchukua hatua dhidi ya kampuni hiyo.

Juzi, Mkurugenzi wa Idara ya Huduma za Mifugo, Prof. Hezron Nonga, alinukuliwa na kituo kimoja cha televisheni nchini, akisema kilichofanywa na mwekezaji huyo ni kinyume cha Sheria ya Ustawi wa Wanyama ya Mwaka 2010.

"Vifaranga wanawekwa kwenye matanuru ya moto, vifaranga vinalia machozi lakini vinachomwa moto ili viungue.

Hiyo ni kinyume cha Sheria ya Ustawi wa Wanyama ya Mwaka 2010. Serikali tunakusudia kuchukua hatua dhidi ya kampuni ile kwa kitendo ilichofanya," alisema.

Desemba 13, mwaka huu, Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, anayesimamia sekta ya mifugo, Tixon nzunda, wakati anafungua kikao cha wadau wa tasnia ya kuku, kilichofanyika jijini Dodoma, alinukuliwa akiwataka wazalishaji wa vifaranga vya kuku nchini kuzalisha vifaranga kwa kuzingatia ubora wa kitaifa na kimataifa na mahitaji yaliyopo.

Kikao hicho kilikuwa kikijadili hali ya upatikanaji na bei ya vifaranga na vyakula vya kuku pamoja na kushuka kwa soko na bei ya kuku wa nyama nchini.

Kwa mujibu wa wavuti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, pia kikao hicho kilijadili namna ya kupunguza gharama za uzalishaji wa kuku, hasa wa nyama ikiwa msingi mmojawapo wa kuwawezesha wafugaji wadogo na walaji kumudu gharama.

Pia wadau hao walijadili kuhusu gharama kubwa za utengenezaji wa chakula cha kuku, ili kuona namna gani wanaweza kuzipunguza, na hivyo kumsaidia mfugaji kupunguza gharama za ufugaji.

Mkurugenzi huyo alipoulizwa kuhusu malalamiko ya utoaji wa vibali vya uingizaji wa vifaranga unaolalamikiwa na wengi, alisema: "Tumekuwa tukiwaeleza kwamba vifaranga hawa wanaoendelea kuruhusiwa, walikuwa wameshalipiwa kabla ya katazo.

"Kwa hiyo sasa, serikali haikuwa na sababu yeyote ya kuwakatalia hawa wakati walishalipia vifaranga, na ndio ambao tumeendelea kuwaruhusu kuingiza vifaranga, lakini ukomo wa kuingia kwa vifaranga hivi itakuwa ni Desemba 31, mwaka huu," mwaka huu.

Kuhusu wafanyabiashara wachache ambao wamesalia kuingiza vifaranga, alisema wafugaji wengi hasa wa kuku na nyama wameacha kufuga.

"Aidha wamefunga kabisa mabanda au wamepunguza idadi ya kuku waliokuwa wanafuga. Kama mtu alikuwa anafuga kuku 2,000 kwa wakati mmoja utakuta anafuga kuku 200 kwa wakati mmoja.

"Kwa nini hao watu wameacha kufuga, moja, chakula cha kuku kimepanda bei sana. Kilikuwa kinauzwa 65,000 mpaka 70,000 kwa mfuko wa kilogramu 50, sasa hivi chakula cha kuku kinauzwa kwa shilingi 90 mpaka 95 kwa mfuko wa kilogramu 50," alisema.

"Kuku 500 wanakula mfuko mmoja kwa siku, sasa huyu mfugaji akipiga hesabu pale hakuna atakachokipata. Ukiweka gharama za chakula, mambo ya maji, chanjo, madawa na huduma zingine, huyu mfugaji hakuna anachokipata sana sana anapata hasara.

"Pamoja na hao kuku anaowafuga kwa hasara, bado bei ya kuku imepungua sana. Zamani bei ya kuku Dar es Salaam, kuku mmoja wa nyama alikuwa anauzwa kwa Sh. 7,000 mpaka 8,000. Sasa hivi anauzwa Sh. 4,000 hadi 5,000," aliongeza.

Alipoulizwa serikali inawasaidiaje wafugaji hao wa kuku, Prof. Nonga alisisitiza ni lazima wafugaji wajue kwamba kuna msimu wa mavuno sana na kuna msimu wa hasara.

"Walivuna sana kipindi mahitaji ya vifaranga ni makubwa, walikuwa wanauza mpaka 2,500 na bado mtu analipia leo vifaranga 5,000 anasubiri mpaka miezi mitatu.

Hiki ni kipindi cha mpito, hali itatengemaa tu.

Kufikia mwishoni mwa mwezi huu, vifaranga watapanda tu bei." alisema.

Zaidi ya vifaranga 50,000 vya kuku wa nyama na mayai vimeteketezwa kwa moto mkoani Kilimanjaro kwa madai ya kukosa soko kutokana na kuwapo kuku wanaoingizwa kutoka nje ya nchi kuathiri soko la ndani.

Mwekezaji huyo wa shamba la kuku (jina limehifadhiwa), akizungumzia uamuzi wake wa kuvichoma moto vifaranga hivyo, alisema ameamua kufanya hivyo kwa sababu hali ya soko la kuku nchini kwa sasa si la kuridhisha kutokana na wafugaji kupata hasara baada ya wafugaji kutumia gharama kubwa za uzalishaji.

"Sasa tuna mayai 8,000 kwenye mashine, tunatotoa kila wiki 2,000 lakini hakuna biashara. Siku nne zilizopita tuliuza vifaranga kwa Sh. 1,000 mpaka 900 watu hawataki. Umeona mwenyewe vifaranga 34,000 vimerudi havina biashara," alisema mwekezaji huyo.

Hivi karibuni, wafugaji waliiomba serikali kuangalia uwezekano wa kudhibiti vifaranga kutoka nje,ambavyo vimejaa sokoni huku bei ya chakula ikizidi kupaa na kuwalazimu kuuza kwa bei ya hasara Sh. 4,000 kutoka 6,500.

Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Wafugaji wa Kuku wa Nyama Tanzania (TABROFA), Aloyce Makoye, alisema hali sio ya kuridhisha na watu wanalazimika kuachana na biashara hiyo, lakini serikali imeendelea kuruhusu vifaranga kutoka nchi mbalimbali.

# Balozi wa Tanzania Austria alivyoteketea ajali ya gari

**Na Elizabeth Zaya**

BALOZI wa Tanzania nchini Austria na Mwakilishi wa Kudumu wa Mashirika ya Kimataifa Vienna, Celestine Mushy, amefariki dunia katika ajali ya gari huku mwili wake ukiteketea kwa moto katika eneo la Mkata, mkoani Tanga.

Kutokana na kifo hicho, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ametuma salamu za rambirambi huku akieleza kuwa nchi imepata pigo kubwa.

Kwa mujibu wa ujumbe wa pole ulioandikwa kwenye akaunti ya Twitter, Rais Samia alisema taifa limeondokewa na mwanadiplomasia mahiri.

"Tumeondokewa na mwanadiplomaia mahiri na mtumishi makini wa umma. Mungu amweke mahali pema. Amina," ilisema taarifa hiyo ya Rais.

Mkuu wa Wilaya ya Handeni, Siriel Mchembe, aliiambia Nipashe kuwa Balozi Mushy alifariki dunia juzi kwa ajali ya gari eneo la Mkata akiwa njiani kwenda Moshi mkoani Kilimanjaro.

Alisema Balozi Mushy alikuwa anaendesha gari mwenyewe na alipata ajali baada ya kugongana na lori kisha likawaka moto. "Hilo tukio lilitokea Jumanne usiku wakati akisafiri kuelekea Moshi. Aligongana na lori na magari yote yaliteketea kwa moto. Mwili wake umehifadhiwa katika Hospitali ya Wilaya ya Handeni. "Mwili wa balozi ulikutwa umeungua na tuliuchukua eneo la ajali usiku na tukaupeleka Hospitali ya Handeni. Ndugu zake wako njiani kutokea Dar es Salaam kwa ajili ya kuutambua na kuuchukua," aliongeza. Akizungumza na Nipashe, mdogo wa Balozi Mushy, Ernest Mushi, ambaye alikuwa amefika katika hospitali ya Handeni kwa ajili ya utambuzi wa mwili alisema: "Sisi ndio tumefika hapa hospitalini. Bado tuko nje tunasubiri kuutambua mwili na baada ya hapo ndipo taratibu nyingine tutajua tunafanyaje," alisema.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Henry Mwaibambe, alisema ajali hiyo ilihusisha magari mawili, moja dogo aina ya Toyota Crown lenye namba ya usajili T 175 DMF mali ya Balozi Mushy ambalo lilikuwa linaendeshwa na mtu mmoja na liliungua hadi majivu.

"Ilikuwa ajali iliyohusisha magari mawili kugongana. Gari dogo aina ya Toyota Crown lilikuwa linaendeshwa na mtu mmoja na liliungua hadi majivu. Kwa hiyo tulikuwa kwenye utaratibu wa kupima mabaki ya mwili ili kujua kama kweli ni ya Balozi Mushy kutokana na kuungua sana kiasi cha kutokutambulika kwa macho," alisema Kamanda Mwaibambe. "Baadhi ya ndugu wa Balozi walikuja. Kwenye usajili wa gari, jina lake linaonyesha ni lake hiyo ndiyo maana wanahisi ni yeye. Tunasubiri uchunguzi wa wataalam ufanyike kwa haraka tutajua tu," alisisitiza Kamanda Mwaibambe.

Balozi Mushy aliteuliwa na Rais Samia kushika nafasi hiyo Januari, mwaka huu, na Mei aliwasilisha Hati ya Utambulisho kwa Rais wa Jamhuri ya Austria, Alexander Van Der Bellen.


SPY TECH

**SPYTECH AND SECURITY SUPPLIES LTD**

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA.**

Kwa idhini tuliyopewa na **MUCOBA BANK PLC** tutauza dhamana za wadaiwa ili kufidia madeni yao wanayodaiwa kwa njia ya mnada wa hadhara kuanzia tarehe 21/12/2022 na kuendelea.

Mnada utafanyika mahali dhamana za wadaiwa zilipo kama inavyoonekana hapo chini.

| NA. | JINA LA MDAIWA | DHAMANA | MAHALA ILIPO DHAMANA | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | THOMAS Y. KIDENYA | NYUMBA | KINYANAMBO "C" | KUANZIA TAREHE 21/12/2022 NA KUENDELEA |
| 2 | KIHANGA WOMAN SACCOS | NYUMBA | KINYANAMBO "A" | |
| 3 | STEPHEN AIDAN MOSHA | NYUMBA | MALINGUMU-MAFINGA MJINI | |
| 4 | ABDALLAH MSAFIRI ZINGO | NYUMBA | CHANGARAWE BLOCK "J" | |
| 5 | GODFREY MASAWE | NYUMBA | IGOWOLE-MUFINDI | |
| 6 | GETRUDE MBOGO | NYUMBA/ | MGODI-MAFINGA | |
| 7 | NASSIR LUFYAGILE | KIWANJA | BALALI-MAFINGA | |
| 8 | WITNESS CHUMI | NYUMBA | GANGILONGA-MAFINGA | |
| 9 | JAPHET MLEMBE | NYUMBA | IGOWOLE – MUFINDI | |
| 10 | LUTA TURUKA | KIWANJA | IHONGOLE-MAFINGA | |
| 11 | SOSTEN ISACK MWIKE | PAGALE | LUMWAGO-MAFINGA | |
| 12 | ASHARO STEPHAN NGIMBA | NYUMBA | IKANGAMWANI-MUFINDI | |
| 13 | EMMANUEL NGAILO | NYUMBA | MBAGALA-MAFINGA | |
| 14 | STANFORD ADELTUS KISINGA | NYUMBA | MADIBIRA/MBARALI-MBEYA | |
| 15 | DICKSON J. KITAMKNGA | NYUMBA | MADIBIRA/MBARALI-MBEYA | |
| 16 | OMARY THOMAS LUMATO | NYUMBA | MADIBIRA/MBARALI-MBEYA | |
| 17 | ERICK H. SENYAGWA | NYUMBA | MADIBIRA/MBARALI-MBEYA | |
| 18 | MOSES MAIKO MANGA | NYUMBA | MADIBIRA/MBARALI-MBEYA | |
| 19 | MADIBIRA SACCOS | NYUMBA | MADIBIRA/MBARALI-MBEYA | |
| 20 | ROBERT A KILOVELE | NYUMBA | ILULA/KILOLO-IRINGA | |
| 21 | BENNY C. MBUNDAMILA | NYUMBA | ILULA/KILOLO-IRINGA | |
| 22 | AMOSI L. SANGA | NYUMBA | RUAHA/MBUYUNI/KILOLO-IRINGA | |
| 23 | ESTER NGANDANGO | NYUMBA | IMAGE-KILOLO- IRINGA | |
| 24 | MANENO MWOFUGA | NYUMBA | CHANGARAWE-BLOCK J | |
| 25 | RUTH MATTOWO | NYUMBA | CHANGARAWE-BLOCK J | |

**MASHARTI YA MNADA.**

1. Dhamana itauzwa "kama ilivyo"
2. Ukaguzi wa dhamana utafanyika kuanzia siku ya tangazo hili kutoka kuanzia saa 4:00 asubuhi hadi saa 10:00 jioni
3. Mnunuzi atatakiwa kulipia asilimia 25% siku ya mnada na asilimia 75% iliyobaki amalizie ndani ya siku 14.
4. Endapo mteja atashindwa kumalizia asilimia 75% ya Kiasi kilichosalia ndani ya siku 14, hatarudishiwa kiasi alicholipa awali na mnada utarudiwa tena.
5. Gharama za kubadilisha hati miliki (transfer of ownership) na gharama nyingine zikiwemo usafiri ni za mnunuzi.

**Kwa Maelezo zaidi wasiliana nasi:**
**MKURUGENZI MTENDAJI,**
**SPYTECH AND SECURITY SUPPLIE LTD,**
**P O. BOX 480**
**MAFINGA-IRINGA,**
**SIMU: 0755 815 974 / 0623 815 974 AU Email: spytechz@gmail.com**

17196802

# TRC yaongeza mabehewa kukabili adha usafiri

**Na Romana Mallya**

KATIKA kukabili shida ya usafiri kwa abiria wanaokwenda mikoa ya Kaskazini, Shirika la Reli Tanzania (TRC), limeongeza mabehewa 16 ya treni ya Deluxe.

Aidha, mabehewa mapya 21 kati ya 22 yaliyonunuliwa na serikali yameanza kazi rasmi jana kwa kubeba abiria 1,500 kuelekea Kigoma.

Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano TRC, Jamila Mbarouk, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumzia safari ya Kigoma ambayo abiria waliondoka jana saa mbili asubuhi na kutarajia kufika leo jioni.

Alisema safari ya kuelekea Kigoma imefanyika baada ya majaribio ya awali ya umbali wa kilometa 400 kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro na Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini (LATRA), imeridhia mabehewa hayo kuanza kazi.

"Kati ya mapya 21, mabehewa 20 ni kwa ajili ya kubeba abiria na moja litatumika kwa huduma ya mgahawa, yameondoka leo (jana) yakiwa na abiria 1,500," alisema.Pia alisema kutokana na ununuzi huo wa mabehewa, TRC limeongeza idadi ya mabehewa ya treni ya Deluxe kuelekea mikoa ya Kaskazini kutoka mabehewa sita hadi 16 na njia ya reli ya kati kutoka mabehewa 14 hadi 20. "Treni ya Deluxe mwanzoni ilikuwa na mabehewa 22 ambapo tuliivunja, ili iweze kusaidia kubeba abiria wanaokwenda Kigoma na wa Kaskazini. Katika kuigawa tulikuwa tunapata changamoto ya watu kuwa wengi na behewa kutotosha.

"Mfano, njia ya Kaskazini kwa mwaka jana kipindi kama hiki cha sikukuu tulikuwa tunakwenda mara sita kwa wiki na siku nyingine ilitulazimu kupeleka treni ya ziada ambayo haipo kwenye ratiba ya kawaida. Jana waliondoka abiria 700."

Alisema katika kukabiliana na wingi wa abiria kuanzia Jumatatu ya wiki hii wamekuwa wakipeleka mabehewa 16 na yote hujaa.



Meza za wamachinga zikiwa juu ya mtaro eneo la Mbezi Luis Dar es Salaam jana licha ya serikali kutoa maelekezo ya kuacha mitaro hiyo iwe wazi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Mkurugenzi matatani kutotekeleza hukumu

**Na Grace Gurisha**

WAKILI Joseph Rutabingwa wa Kampuni ya Coast Textiles Ltd amedai Mahakama Kuu kuwa Mkurugenzi wa Bodi ya Bima ya Amana (DIB), Isack Kihwili, anapaswa kuonyesha sababu kwa nini asipelekwe gerezani kwa kushindwa kulipa Sh. bilioni 145.9 katika kutekeleza hukumu iliyotolewa miaka saba iliyopita.

Vilevile, kampuni hiyo imeiomba mahakama hiyo itupilie mbali ombi la Wakili Mkuu wa Serikali, Jacline Kinyasi la kutaka kupinga mwenendo wa utekelezaji wa hukumu iliyotolewa dhidi ya mkurugenzi huyo kuhusu malipo ya fedha hizo katika kesi inayohusu Benki ya FBME.

Wakili Rutabingwa alidai hayo jana mbele ya Jaji Amir Mruma kuwa mkurugenzi huyo anapaswa kuonyesha sababu kwanini asipelekwe gerezani kwa kushindwa kulipa kiasi hicho cha fedha katika kutekeleza hukumu ya Mahakama Kuu iliyotolewa miaka saba iliyopita.

Rutabingwa alidai kampuni hiyo ilipaswa kufuata utaratibu uliowekwa chini ya sheria ya mashauri ya serikali ili kutekeleza mchakato wa kukaza hukumu.

Wakili Kinyasi alidai kampuni hiyo ilitakiwa kuwasilisha cheti Wizara ya Fedha kupitia kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kutekeleza malipo hayo kwa kuwa Mkurugenzi Kihwili ni mtumishi wa umma.

Pia aliiomba mahakama kusitisha utekelezaji wa hukumu hiyo kwa sababu wamewasilisha taarifa ya kukata rufani dhidi ya amri iliyotolewa na Jaji Mruma Mei 20, mwaka huu ya kumtaka Mkurugenzi wa DIB kulipa kiasi hicho cha fedha.

"Endapo kutakuwa na haja ya Mkurugenzi wa DIB kujitokeza kama ilivyoagizwa wapewe muda wa kuwasilisha hati ya kiapo, ili aweze kujieleza kwa nini hajalipa fedha hizo katika utekelezaji wa hukumu iliyotolewa mwaka 2015 na Jaji Aloysius Mujulizi," alidai Kinyasi.

Baada ya Kinyasi kudai hayo, Rutabingwa alidai kuwa uamuzi uliotolewa na Jaji Mruma Mei 21, mwaka huu, ulikuwa wa mwisho na hadi wakati huo Kihwili alikuwa tayari amewasilisha hati ya kiapo kueleza kwanini hakutekeleza hukumu ya mahakama.

Alidai kuwa kwa mazingira hayo, Kahwili hawezi kupewa nafasi nyingine ya kueleza jambo lilelile, kilichokuwapo mbele ya mahakama kwa sasa ni kueleza kwanini asifungwe gerezani kwa kushindwa kutekeleza hukumu ya mahakama.

Wakili Rutabingwa alidai kuwa hakuna rufani yoyote ambayo iliwasilishwa dhidi ya hukumu iliyotolewa na Mahakama Kuu kuhusu suala hilo, hivyo utekelezaji wake unapaswa kuendelea. Alidai kuwa fedha zinazotakiwa kulipwa siyo za serikali.

Rutabingwa aliendelea kudai kuwa kinachofanywa na Ofisi ya Wakili Mkuu ni kuchelewesha utekelezaji wa hukumu hiyo na kwamba kitendo hicho kinadharau hukumu halali ya mahakama, kwa kuwa suala hilo tayari limeamuliwa na mahakama kwenye ngazi mbalimbali.

Mei 21, mwaka huu, Jaji Mruma alitoa amri hiyo dhidi ya Mkurugenzi wa DIB, mlalamikiwa, ambaye aliteuliwa na Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kuwa Mfilisi wa Benki ya FBME baada ya kuridhia maombi ya utekelezaji wa hukumu yaliyowasilishwa na Costal Textiles Limited, mwombaji.

Jaji huyo alibainisha zaidi kuwa hakuna sababu zilizotolewa na mfilisi kuonyesha kwanini benki husika ilifungwa na baada ya hapo kunyang'anywa leseni yake ya uendeshaji.

Jaji Mruma alisema amri ya mahakama ni ya mwisho, hivyo haiwezi kuchunguzwa au kuorodheshwa na mfilisi, hivyo alikataa kutoa uamuzi kwamba mwasilishaji maombi hawezi kutekeleza hukumu ya mahakama.

Kampuni hiyo ya kitanzania iliwasilisha maombi ya utekelezaji hukumu ikidai kuwa kiasi cha Sh. 145,946,500,641 kilipwe na DIB, taasisi ambayo ilichukua ufilisi wa FBME na kama itashindwa, Mkurugenzi wa DIB awajibishwe kwa kulipa fedha hizo.

## Watanzania watakiwa kuchanja kabla kusafiri

**Na Elizabeth Zaya**

MGANGA Mkuu Mkoa wa Dar es Salaam, Dk. Rashid Mfaume, amewataka Watanzania kuchanja chanjo ya UVIKO-19 kabla ya kusafiri nje ya nchi, ili kutoa nafasi kwa kinga hiyo kufanya kazi vizuri.

Akizungumza na Nipashe katika mahojiano ofisini kwake kuhusu umuhimu wa chanjo kitaalamu, alisema baadhi ya watu hukimbilia kuchanja wanapoona wanatakiwa kusafiri jambo ambalo sio sahihi.

Alisema ni vizuri watu waendelee kuchanja kwa lengo la kujikinga, badala ya kusubiri mpaka wapate safari za nje.

"Kuna mtu akipata safari nje ya Tanzania eti ndio anakimbizana kwenda kuchanja, tulipata kesi za namna hiyo mwanzoni na tukawashauri kwamba hiyo haiwezi kuwa sababu pekee ya kufanya hivyo kwa sababu lengo kuu ni kumkinga mtu, ili ikusaidie ni lazima uwe umechanja angalau wiki mbili kabla ya kusafiri, siyo unachanja leo halafu kesho unasafiri hapana," alibainisha Dk. Mfaume.

"Tunataka ukichanja ikusaidie kukukinga wewe na wengine, hakuna sababu ya kuwa na dharura, kwa nini usichanje mapema, ni vyema watu wakajijengea utaratibu wa kuona umuhimu wa chanjo."

Kuhusu watu wanaotakiwa kurudi kwa ajili ya chanjo ya mara ya pili, Dk. Mfaume alisema ni muhimu kila mtu kufanya hivyo ili kukamilisha chanjo na kinga.

"Ni lazima ukamilishe chanjo ya pili, huwezi kukamilisha dozi endapo hujachanja kwa mara ya pili endapo chanjo yako ya awali inahitaji uchanje mara mbili, sio kwamba ukipata moja utakuwa umekingwa kwa asilimia 100 unakuwa unajidanganya, ili upate kinga kamili lazima ukamilishe chanjo."

"Na bahati nzuri katika mfumo wetu wa kielektroniki unaotoa vyeti unaeleza kabisa kwamba unatakiwa urejee lini kwa ajili ya kupata chanjo ya pili kwa zile chanjo za mara mbili, kwa hiyo tusidharau hakikisha unakamilisha chanjo.

"Kama hujarudi unakuwa hujakingwa, unakuwa na kinga ambayo haikusaidiii sana kisayansi, sio tu unaambiwa ukamilishe dozi mbili, bali ni tafiti za kisayansi ambazo zinaonyesha ukikamilisha hizo mbili ndio unakuwa umekingwa kikamilifu."

Mpaka sasa chanjo zilizoletwa Tanzania ni aina tano ikiwamo Janssen and Jassen, Pfizer, Moderna, Sinopharm, na Sinovac.

Hadi Desemba 2, mwaka huu jumla ya Watanzania milioni 29,123, 387 walichanjwa kati yake wa Dar es Salaam ni milioni 3.2.

Ugonjwa wa UVIKO-19 ulianzia nchini China na ulisambaa duniani na kusababisha vifo na madhara mengine kiuchumi.

TANGAZO

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

# TAARIFA KWA UMMA
## MATUMIZI YA NAMBA YA UTAMBULISHO (TIN) SAHIHI KWA WAAJIRIWA NA AINA YA AJIRA

Mamlaka ya Mapato Tanzania ("TRA" au "Mamlaka") inapenda kuwakumbusha waajiri wote kuhusu uzingatiaji wa matumizi ya TIN sahihi kwa waajiriwa wote katika uwasilishaji wa ritani za Pay as You Earn (PAYE). Mamlaka imefanya maboresho katika mfumo wa uwasilishaji ritani ambapo kushindwa kutumia TIN sahihi kutakwamisha uwasilishaji wa ritani sahihi kwa waajiri katika mfumo huo na hivyo kupelekea usumbufu usio wa lazima ikiwemo riba na adhabu.

Ikumbukwe kuwa, Mamlaka imekuwa ikuwakumbusha waajiri wote kuhakikisha kuwa waajiriwa wao wana TIN na zinatumika kikamilifu sawa na matakwa ya **kifungu cha 22 cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura 438.** Pamoja na ukweli kwamba waajiri wengi wameonesha mwitikio chanya bado kuna baadhi ya waajiri ambao wameshindwa kusimamia matakwa hayo ya kisheria kwa kuendelea kuwasilisha ritani za PAYE bila kutumia TIN sahihi za waajiriwa au kutumia **TIN 999 999 999**.

Kufuatia hilo, Mamlaka inapenda kuwakumbusha waajiri na waajiriwa wote kuhakikisha kuwa wanazingatia takwa hili la kisheria la kuhakikisha matumizi sahihi ya TIN katika uwasilishaji wa ritani ya **PAYE** kuanzia mwezi **Disemba, 2022**. Mfumo wa uwasilishaji ulioboreshwa ***(Upgraded e-filing)*** utashindwa kupokea majina ya waajiriwa wasio na TIN sahihi na hivyo kuathiri usahihi wa ritani husika. Sambamba na matumizi ya TIN sahihi, waajiriwa wanakumbushwa kuhakikisha wanaweka rekodi sahihi za ajira za waajiriwa wao kati ya ***ajira ya msingi (Primary Employment) au ajira ya ziada (Secondary Employment).***

Ikumbukwe kuwa TIN hutolewa bure na upatikanaji wake ni rahisi ambapo kwa waajiriwa wenye namba za usajili inayotolewa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), wanaweza kuomba TIN kwa njia ya mtandao kupitia mfumo wa **Online TIN Registration** kupitia tovuti ya TRA (www.tra.go.tz). Waajiriwa wasio na namba ya NIDA wanakumbushwa kutembelea Ofisi za TRA ili kupatiwa TIN.
Kwa taarifa zaidi, tembelea Ofisi za TRA zilizo karibu nawe au wasiliana nasi kupitia:

| | |
|---|---|
| **Tovuti** | : **www.tra.go.tz** |
| **Namba za Simu bila malipo** | : **0800 750 075 au 0800 780 078** |
| **WhatsApp** | : **0744 23 33 33** |
| **Barua pepe** | : **huduma@tra.go.tz au services@tra.go.tz** |

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***

Imetolewa na;

**IDARA YA HUDUMA NA ELIMU KWA MLIPAKODI**

17195002

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kilio cha mabweni kwa wanafunzi kimesikika

**SERIKALI** imetangaza wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwakani na kutoa kipaumbele kwa wanaokwenda vijijini shule za kitaifa za bweni.

Hatua hiyo inatokana na kilio cha muda mrefu cha wanafunzi kupangiwa shule za mbali na kusababisha watembee umbali mrefu kufuata masomo.

Kutokana na shule kuwa mbali, baadhi yao hukatisha masomo kwasababu ya utoro au wanafunzi wasichana kupata mimba za utotoni kwa vishawishi wanavyopata wakiwa njiani kuelekea shuleni.

Hivi karibuni tu wanafunzi wa kidato cha tano na sita wa Shule ya Sekondari Hai, walitoa kilio chao cha upungufu wa mabweni na kulazimika kutumia vyumba vya madarasa kulala.

Kilio hicho walikifikisha kwa Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, huku Mwenyekiti wa wilaya hiyo, Edmund Rutaraka, akiwasilisha ombi maalum la kuomba mkoa huo uongeze nguvu ya fedha kwa ajili ya ujenzi wa mabweni mawili ya kidato cha tano na cha sita.

Akizungumzia kilio hicho, Mkuu wa Mkoa alisema ameliona tatizo kwa macho yake na atalifanyia kazi haraka iwezekanavyo kwa kuhakikisha fedha zinapatikana za ujenzi huo wa mabweni pamoja uzio.

Akitangaza wanafunzi wanaojiunga na kidato cha kwanza, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Angella Kairuki, aliagiza wanafunzi wote waliochaguliwa kujiunga na shule za bweni, kuripoti shuleni Januari 7, mwakani na waliochaguliwa kujiunga shule za kutwa kuripoti Januari 9.

Kwa mujibu wa Waziri Kairuki, wanafunzi 3,224 sawa na asilimia 0.39 wamechaguliwa kujiunga na shule za bweni za kitaifa, kati yao 932 wakiwamo wavulana 512 na wasichana 420, wamechaguliwa kujiunga na shule za sekondari za wanafunzi wenye ufaulu mzuri zaidi.

Juhudi za serikali kujenga mabweni kwenye shule ni hatua itakayosaidia wanafunzi wengi zaidi kutimiza ndoto zao zilizokuwa zikikatishwa kwa sababu mbalimbali zikiwamo za umbali wa shule.

Hii ni fursa nzuri kwa wanafunzi kuwa karibu na shule na kupata muda mwingi wa kujisomea na kufanya vizuri kwenye masomo yao.

Umuhimu wa shule za bweni ni kutoa nafasi kubwa kwa wanafunzi kupata muda mwingi kujisomea tofauti na wanaporudi nyumbani, wengine hutumikishwa kazi mbalimbali na kukosa muda huo.

Wanafunzi wanapokuwa pamoja pia hutoa fursa ya wao wenyewe kusaidiana iwapo baadhi yao uelewa unapokuwa mdogo.

Pia husaidia kwa sababu wanafunzi wengine wanapofundishwa darasani hawaelewi mara moja mpaka watakapopata ufafanuzi kutoka kwa wenzao.

Wanafunzi wanapoishi pamoja na kusaidiana, huwajengea umoja, upendo na kuishi kama ndugu. Ndiyo maana kuna baadhi yao wanaona ni bora kuishi shule kuliko nyumbani kutokana na wengine kukosa mapenzi kutoka kwa wazazi au walezi wao na muda wa kuweka mkazo kwenye masomo hukosekana kwa sababu ya mawazo.

Wanafunzi wengi waliosoma katika shule za bweni, hujikuta wakifanya vizuri zaidi kuliko wa kutwa kwa kuwa wanapata muda mwingi wa kujisomea.

Tunasema hatua hii ya serikali ya kutoa kipaumbele kwa shule za bweni itasaidia sana kuleta matokeo mazuri kwenye elimu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

Na Mwandishi Wetu

# Mwaka umefika ukingoni, umejifunza kupanga bajeti, kuwekeza mitaji yako?

**WOTE** tuna matumizi yanayohusisha fedha, kila siku hili ni hitaji lisiloepukika, ama iwe ni moja kwa moja au kwa njia nyingine.

Ingawa wengi hawana bajeti ya siku, mwezi au mwaka, matumizi yanapishana kutokana na kutokuwapo mpangilo maalumu wa matumizi hayo ikiwamo manunuzi ya chakula, nishati, nauli na mengineyo.

Wengi wakiulizwa mwaka jana tulitumia shilingi ngapi hakuna majibu, pengine hawajui hata matumizi yao, kwa kutojua matumizi ni ngumu kubaini nini kifanyike na kipi kisifanyike na pengine kipi kisubiri.

Ni vyema kupanga matumizi kwa ajili ya chakula, usafiri, na mambo yote muhimu na pengine yasiyo muhimu au ziada. Tumia kidogo na weka zaidi kwa ajili ya furaha ya baadae. Yaani jifunze kuweka.

Uwekezaji hauna kuchelewa kwenye faida jumuishi ambazo hupatikana kwenye mifuko yetu nyumbani UTT AMIS. Mfano wa faida jumuishi ni kama ukiwekeza Sh. 50,000 ndiyo kiwango cha awali, halafu kila mwezi ukawekeza shilingi 200,000 utakuwa umeweka shilingi milioni 29 kwa miaka 10.

Kama hela hizo zitakuwa kwa riba ya asilimia 1.2 kwa mwezi, utakuwa na jumla ya zaidi ya shilingi milioni 74 miaka 10. Yaani wewe umewekeza shilingi milioni 29, lakini umepata zaidi ya shilingi milioni 74. Haya ndiyo maajabu ya uwekezaji kupitia mifuko ya uwekezaji wa pamoja.

Pia, kumbuka Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) inasisitiza kwamba thamani ya kipande inaweza kupanda au kushuka. Tabia ya uwekezaji wowote, hata kwenye duka au hoteli kuna siku utapata zaidi na kuna siku kidogo kwa uwekezaji huo huo, au hata pale unapokuwa umeongeza mtaji.

Wakati wa kustaafu si wakati wa kujenga nyumba, ila kama hukuwahi kujenga au kununua nyumba kabla ya kustaafu na ukashawishika kufanya hivyo baada ya ukomo wa ajira, basi nunua nyumba ndogo. Hii ina maana muhimu kuwa makini kwenye matumizi na kununua, ni vizuri mambo hayo yazingatiwe wakati wa kwenye ajira na ajira binafsi, kwa kufanya tathmini ya kina, ni kiasi gani uwe unatenga kwa ajili ya kustaafu.

Madeni nayo ni shughuli nyingine, madeni yakiwa mengi na makubwa yanatoa tafsiri ya uchache wa akiba au uwekezaji. Usipoangalia utaingia kwenye kustaafu na madeni mengi, huu ni mzigo tena mkubwa ambao utaubeba huku nguvu zikiwa zinafifia.

Hisabati inatajwa ni mtu anatawanya uwekezaji wake na anachagua kwenye nafuu ya kodi, mfano kwenye mifuko tajwa ukiwekeza kwenye mfuko mmoja unakuwa kama vile umewekeza sehemu nyingi. Mfano mfuko wa Umoja unawekeza kwenye hisa za kampuni mbalimbali, na pia kwenye hati fungani za serikali na kwenye benki.

Nafasi inakuja pia kwa mwenza katika familia, anaweza akatangualia mbele ya haki mapema. Pengine yeye ndiye alikuwa kichwa cha familia, ili kukwepa mshituko wa kiuchumi, ulitambue hili na uwe umejiandaa mapema kwa sababu mmoja wetu akitangulia, mambo mengi yanabadilika, kipato, kodi, maisha yenyewe vinachukua mwelekeo mwingine.

Usisahau bima. Hili halikwepeki, kwani ni vigumu kulipa gharama za matibabu kutoka mfukoni na magonjwa kama saratani, kisukari, na shinikizo la damu, ni magonjwa yenye gharama kubwa sana ambazo ukisema ulipe kutoka mfukoni ni ngumu.

Najua zamani watu walikuwa wana koma kufanya kazi na miaka 50 na ikifika miaka 60 wengi wao washapoteza maisha, lakini maendeleo ya huduma za afya, uelewa wa ulaji mzuri na mazoezi unawezesha watu kuishi mpaka miaka 90 hadi 100.

Mwaka ujao kama mwaka huu hayakutimia, tafuta marafiki ambao wana maarifa mapya, epuka upweke, shiriki kwenye kazi au huduma zinazogusa jamii na utakuwa mwenye furaha milele. Endelea kujifunza elimu ya fedha na uwekezaji. Ishi kama hautakufa, kazi ni nyingi unaweza kuwa yaya, kiongozi wa kundi la kusoma vitabu, mtengeneza matangazo kwa kompyuta, unaweza kusaidia katika kuremba nyumba za watu na mazingira yake, unaweza anzisha biashara ya mbwa, samaki wa mapambo, kushona na kubuni mavazi.

Kumbuka hakuna tafsiri kamili kuhusu uzee, kwani wengine kuanzia miaka 40 tu wanaitwa wazee, na saa nyingine wa miaka 70 anaonekana mdogo zaidi ya wa miaka 50. Hivyo, kusema uzee ni umri usio na mpaka hivyo basi pale tutakapoanza kusema 'sasa basi tumezeeka ' ndipo hapo hapo yaweza kuwa chanzo cha matatizo kama vile ufukara, na ukosefu wa furaha.

# ‘Tumieni msimu sikukuu mwisho wa mwaka kwa kuhuisha namba za simu’

**Na Frank Monyo**

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) imewasihi watumiaji wa huduma za mawasiliano, kutumia msimu wa sikukuu za mwisho wa mwaka kuhakiki laini zao za simu ili kujilinda na uhalifu mtandaoni.

Akizungumza jana kwenye kipindi cha televisheni cha Morning Trumpet kinachorushwa na kituo cha Azam, Meneja wa Usimamizi wa Huduma za Mawasiliano ya Simu na Intaneti wa TCRA, Mhandisi Sadath Kalolo, alisema uhakiki wa laini za simu unalenga kuwasaidia wananchi hasa watumiaji wa huduma za mawasiliano ya simu na intaneti kuwa salama wakati wote wanapotumia huduma za mawasiliano.

“Unapohakiki laini zako za simu unajiweka salama wewe na watumiaji wengine wa mawasiliano kwa kuwa wale wasiosajili laini wanazotumia kwa utambulisho wao watakosa huduma kwa kuwa ukizifuta namba hizo zinafungwa,” alisema.

Alielekeza jinsi ya kufanya uhakiki ambapo mtumiaji anapaswa kubofya *106 kisha kufuata maelekezo yanayotolewa kwa menyu yenye maelekezo ya aina tano. Mosi, kuangalia usajili, pili, kujua namba zilizosajiliwa katika mtandao mmoja, tatu; namba zilizosajiliwa mitandao yote, nne, kufuta usajili na tano; kuhakiki au kuongeza namba.

Kwa mujibu wa ofisa huyo, uhakiki huo ni kuangalia iwapo usajili wa laini umefanyika kwa usahihi, kuhakiki iwapo unatambua laini zote zilizosajiliwa kwa kutumia namba ya kitambulisho cha taifa na kurasimishaji namba ambazo mtu anamiliki kwa kuitambulisha namba kuu na namba za ziada.

Aliongeza kuwa mtumiaji wa huduma za mawasiliano ya simu anapobaini uwapo wa namba ngeni kwenye orodha ya menyu ya uhakiki, anapaswa kuzifuta mara moja kwa kuwasiliana na mtoa huduma wa mtandao anaotumia kupitia namba 100 au kufika kwenye duka la mtoa huduma au wakala wa mtoa huduma wa mtandao wake.

Kalolo alisisitiza kuwa kazi ya kuhakiki na kuhamasisha uhakiki ilianza Desemba Mosi, mwaka huu, na itaendelea hadi Januari 30, mwakani huku akisisitiza kuwa baada ya kampeni ya uhamasishaji kukamilika, watumiaji ambao namba zao za simu hazitakuwa zimehakikiwa kwa utambulisho wa kitambulisho cha uraia, zitafungwa kwa kuzingatia kuwa sheria inaelekeza kila mtumiaji wa huduma za mawasiliano ya simu anapaswa kusajili laini yake kwa njia ya bayometria.

Kuhusu watumiaji ambao walisajiliwa laini za simu na watu wengine kwa sababu mbalimbali zikiwamo kutokidhi vigezo vya umri au kukosa namba ya kitambulisho cha uraia, TCRA ilielekeza wahakikishe wanapata namba ya kitambulisho cha uraia kutoka Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) na kusajili kwa utambulisho wao kwa kuwa kumsajilia mtu mwingine ni kosa isipokuwa mtumiaji mwenye umri chini ya miaka 18.

Mamlaka hiyo ilisisitiza kuwa vijana ambao tayari wametimiza umri wa miaka 18 na walisajiliwa laini zao na wazazi au walezi, wanapaswa kupata namba ya kitambulisho cha uraia, kisha kuhuisha usajili kwa kutumia namba zao za uraia.




Mkuu wa Idara ya Mauzo na Usambazaji wa Vodacom Tanzania, George Lugata, akielezea namna ambavyo wateja wa kampuni hiyo wataweza kununua bidhaa mbalimbali za kampuni kupitia mtandao (Online Shopping) na kupelekewa eneo aliko, katika uzinduzi wa huduma hiyo mpya jana jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# PM aitaka TAKUKURU kuongeza kasi uchunguzi wa fedha za miradi

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa ameiagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Rukwa kuongeza kasi katika uchunguzi wa miradi yenye changamoto ili serikali ichukue hatua kwa wakati.

Agizo hilo alilitoa jana wakati akikagua maendeleo ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Sumbawanga na kukuta zaidi ya Sh. bilioni 1.8 zilizotolewa Aprili, 2020 kwa ajili ya kujenga majengo saba, zimetumika kwa kujenga matano tu na fedha zote zimekwisha. Majaliwa alisema TAKUKURU inapaswa kufanya haraka katika uchunguzi unaoendelea nao katika mradi huo ili serikali ichukue hatua kwa wale wote watakaobainika kuwa sababu ya matumizi mabaya ya fedha hizo.

“Nawaagiza TAKUKURU fanyeni haraka katika uchunguzi mnaoendelea nao. Mmeuanza tangu mwezi Oktoba, malizeni haraka ili serikali ichukue hatua. Haiwezekani watu wakacheza na fedha za serikali halafu wakaachwa hivi hivi. Ni lazima tuchukue hatua na wananchi waone kuwa hatua zinachukuliwa,” alisema.

Waziri Mkuu alisema licha ya halmashauri hiyo kupokea Sh. bilioni 1.8 pia zimeongezwa Sh. milioni 700 lakini bado hospitali hiyo haijakamilika wakati wananchi wanataka huduma, jambo ambalo ni kuwachelewesha kupata huduma.

Akiwa katika Kituo cha afya Matanga kilichoko Manispaa ya Sumbawanga, Waziri Mkuu alionyesha kutoridhika na maendeleo ya ujenzi kwa kuwa tayari zimeshatumika Sh. milioni 500 lakini bado hakijakamilika.

Alisema amelazimika kutembelea miradi ya ujenzi wa hospitali ya wilaya pamoja na kituo cha afya Matanga ambavyo havikuwa katika ratiba aliyoandaliwa baada ya kupata taarifa kuwa miradi hiyo imetumia fedha nyingi na imejengwa kwa muda mrefu tena chini ya kiwango na bado haijakamilika mpaka sasa.

Wakati akiweka jiwe la msingi katika ujenzi wa jengo la ofisi ya mkuu wa wilaya ya Kalambo aliwataka watumishi wa umma kote nchini kutumia siku tatu ofisini na siku zilizobaki katika wiki watoke ofisini na kwenda kuwahudumia wananchi vijijini.

Awali, Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, Queen Sendiga, aliwaambia wananchi wa mkoa huo kuwa Waziri Mkuu amefika mkoani humo kwenye ziara ya kawaida ya kiutendaji kukagua maendeleo ya miradi ambayo serikali ilitoa fedha na kuangalia thamani ya fedha. Mbunge wa Sumbawanga Mjini, Aeshi Hilal, aliishukuru serikali kwa kutekeleza miradi ya maendeleo katika Manispaa ya Sumbawanga kwa kuwa itawaletea maendeleo wananchi na kutatua changamoto walizo nazo.

**KABWELA** Na Fadhili Mohammed



MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

# TAARIFA KWA UMMA

## UHUISHAJI WA LESENI ZA UZALISHAJI BIDHAA ZINAZOTOZWA USHURU WA BIDHAA / SPIRITI ZENYE VIONJO

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inapenda kuwakumbusha wazalishaji na wanaotarajia kuanza uzalishaji wa bidhaa zinazotozwa ushuru wa bidhaa au spiriti yenye vionjo (denatured spirits) kuwa, leseni za mwaka 2022 zilizotolewa chini ya kifungu Na. 8 na/au Na.16 cha Sheria ya Usimamizi wa Ushuru wa Bidhaa (Excise (Management & Tariff) Act) Sura ya 147, zinatarajiwa kufikia ukomo wa matumizi mnamo tarehe 31 Desemba 2022. Hivyo basi, wazalishaji wanakumbushwa kuleta maombi kwa Kamishna Mkuu ili kuhuisha leseni zao kwa ajili ya mwaka 2023 na kuepuka usumbufu unaoweza kujitokeza mara baada ya leseni zao za sasa kufikia ukomo.

**Masharti ya Leseni;**

i). Maombi yafanywe kwa Kamishna Mkuu kwa kutumia Fomu Na. ITX258.01. E inayopatikana kwenye tovuti ya TRA (www.tra.go.tz) na kwenye ofisi za TRA nchi nzima. Fomu za maombi ziwasilishwe kwenye ofisi ya TRA ya mwombaji.

ii). Maombi tofauti yatafanywa kwa kila kiwanda kinachojihusisha na uzalishaji wa bidhaa zinazotozwa ushuru wa bidhaa pamoja na kila kundi la bidhaa zinazotozwa ushuru wa bidhaa.

iii). Leseni itatolewa kwa mwombaji husika, na itatumika katika kiwanda husika na itatumika kuzalisha bidhaa iliyopewa leseni pekee.

iv). Sigara na tumbaku iliyoboreshwa vitahesabika kama kundi moja la bidhaa zinazotozwa ushuru wa bidhaa.

v). Mzalishaji mwenye leseni hatoruhusiwa kuihamisha leseni husika, kiwanda au kutengeneza bidhaa iliyo kwenye kundi jingine (different class of excisable goods) bila kuomba na kuruhusiwa na Kamishna Mkuu.

vi). Leseni itatolewa baada ya kuwasilishwa kwa ushahidi wa malipo ya ada ya maombi ya leseni ya shilingi Laki Tatu (300,000/=) kama ilivyotajwa katika Kanuni ya 4 ya Kanuni za Leseni na Usimamizi wa Wazalishaji wa Bidhaa Zinazotozwa Ushuru wa Bidhaa na/au Spiriti zenye vionjo (Denatured Spirits) za mwaka 2020

Ifahamike kuwa, kwa mujibu wa Kifungu Na. 8 na 16 cha Sheria ya Usimamizi wa Ushuru wa Bidhaa (Excise (Management & Tariff) Act) Sura ya 147, ni makosa kuzalisha bidhaa zinazotozwa ushuru wa bidhaa au spiriti yenye vionjo bila ya kuwa na leseni halali inayotolewa na Kamishna Mkuu. Kosa hilo linaweza kupelekea adhabu ya faini au kifungo au vyote kwa pamoja. TRA itaendesha ukaguzi wa kina kubaini wazalishaji wa bidhaa husika wanaoendesha shughuli zao bila ya kuwa na leseni halali na kuwachukulia hatua stahiki.

**"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"**

**Imetolewa Na;**
**MKURUGENZI WA HUDUMA NA ELIMU KWA MLIPAKODI**
**12 Desemba 2022**

17197602

# Polisi yatia mbaroni wahamiaji haramu 36

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

JESHI la Polisi Mkoa wa Singida limekamata wahamiaji haramu 36 kutoka nchi tofauti tano ambao walikuwa wakisafirishwa kupelekwa Afrika Kusini kutafuta kazi.

Aidha, jeshi hilo limemkamata mtuhumiwa kinara wa kusafirisha wahamiaji haramu, Hamad Abdallah, mkazi wa Mbeya ambaye alikamatiwa wilayani Moshi mkoani Kilimanjaro.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Singida, Kamishna Msaidizi (ACP), Stella Mutabihirwa, alisema hayo jana wakati akitoa taarifa kwa vyombo vya habari kuhusu hali ya usalama ya mkoa katika kipindi cha miezi 11 kuanzi Januari hadi Novemba, mwaka huu.

Alisema wahamiaji hao waliokamatwa kwa nyakati tofauti katika operesheni zinazofanywa na jeshi hilo, ni kutoka Kenya (watatu) Ethiopia (tisa), Somalia (13), Eritrea (watatu) na Burundi wanane.

Aliongeza kuwa katika operesheni hiyo, pia yalikamatwa magari mawili yenye namba za usajili T 845 APV aina ya Mitsubishi Pajero na T 133 DKR aina ya Toyota Chaser ambayo yalikuwa yakitumika kusafirisha wahamiaji haramu na kinara wa kusafirisha wahamiaji haramu, Abdallah, pia amekamatwa.

Kamanda Mutahibirwa alisema katika kipindi hicho, Jeshi la Polisi limefanya misako mbalimbali na kukamata bangi kilo mbili na gramu 540, mafuta ya diesel lita 180, pombe ya moshi lita 375, mirungi kilo 19 na gramu 513, kreti tupu 9 za bia, silaha aina ya gobore 15, kitanda na godoro, redio mbili za sabufa, baiskeli nne na pikipiki 13.

Alisema katika misako hiyo watuhumiwa kadhaa walikamatwa na kufikishwa mahakamani na kuhukumiwa vifungo gerezani.

Aliwataja waliohukumiwa kuwa ni Idd Masinga (32) ambaye alihukumiwa miaka 30 kwa kumbaka mwanamke mwenye umri wa miaka 54, Silvanus Vedastus (24) alihukumiwa jela miaka 30; kwa kosa la kumlawiti mtoto wa miaka 10 na Deshi Kahanza (32) alihukumiwa jela miaka 20 kwa kupatikana na meno mawili ya tembo.

Aidha, alitangaza kupiga marufuku disko toto katika kipindi cha sikukuu ya Krismasi na mwaka mpya kwa kuwa maeneo hayo yamekuwa chanzo kikubwa cha watoto wengi kubakwa.

Kamanda Mutabihirwa amewaomba viongozi wa serikali za mitaa kutoa ushirikiano kwa askari wa doria na askari kata katika suala la kuimarisha ulinzi katika maeneo yao kwa kutoa taarifa za uhalifu na viashiria vya uvunjifu wa amani.



Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu (katikati), akikata utepe kuzindua ukamilishaji wa ukarabati wa kiwanda cha kusindika tangawizi kilichoko Mamba Miamba wilayani Same jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ndejembi aonya watumishi udokozi

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deogratius Ndejembi, amekemea tabia ya baadhi ya watumishi wa umma katika idara na taasisi za serikali kujihusisha na vitendo vya wizi.

Amesema vitendo hivyo vinakwenda kinyume na dhamira ya serikali ya kuujenga utumishi wa umma wenye uadilifu na unaowajibika kwa wananchi kwa kutoa huduma bora. Akizungumza na watumishi wa umma wa Wilaya ya Ilala jana, Ndejembi alisema Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ana maono makubwa ya kujenga utumishi wa umma wenye uadilifu, hivyo akawataka watumishi wa umma nchini kutokumwangusha badala yake wafanye kazi kwa bidii na uadilifu.

"Rais Dk. Samia amejipambanua wazi kututhamini watumishi wa umma kwa kuboresha maslahi na stahili zetu, hivyo hatuna budi kufanya kazi kwa bidii na uadilifu ili kuunga mkono kwa vitendo dhamira yake ya kuujenga utumishi wa umma wenye uadilifu na unaowajibika kwa wananchi," alisema Ndejembi.

Pia aliwataka watumishi wa umma kutafakari madhara ya wizi na kutathmini mienendo yao ili kutokuwa sehemu ya kukwamisha dhamira ya Rais Samia ya kuboresha huduma kwa wananchi na kuliletea taifa maendeleo katika sekta zote muhimu kama vile afya, kilimo, uvuvi, biashara, uwekezaji na miundombinu.

Sambamba na hilo, Ndejembi aliwataka waajiri na maofisa utumishi serikalini kuwasimamia vyema watumishi wanaowaongoza badala ya kusubiri mpaka viongozi wa juu wa kitaifa kufika katika maeneo yao ya kazi kukemea uovu na kutatua changamoto zinazowakabili watumishi wa umma.

Kuhusu matumizi ya fedha za umma, Ndejembi alisema zinapaswa kutumika kwa malengo yaliyokusudiwa na serikali kwa kuwa kinyume na hilo ni ukosefu wa maadili katika utumishi wa umma.

Aliweka bayana kuwa serikali haitomvumilia mtumishi yeyote atakayekwenda kinyume cha maadili ya utumishi wa umma kwa kujihusisha na vitendo vya wizi katika eneo lake la kazi.

Naibu Waziri Ndejembi ameendelea na ziara ya kikazi mkoani Dar es Salaam yenye lengo la kuhimiza uwajibikaji kwa watumishi wa umma na kukagua utekelezaji wa Mpango wa Kuzinusuru Kaya Maskini nchini unaoratibiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).

# RC awatoa hofu wananchi kuhusu mbolea

**Na Gideon Mwakanosya,**
MBINGA

MKUU wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Laban Thomas, amewatoa hofu wananchi kuwa mbolea ipo ya kutosha na kwamba mbolea ndiyo uhai wa mkoa.

Akizungumza na wananchi wilayani Mbinga, Kanali Thomas amesema changamoto ni mfumo wa kielektroniki ambao unashughulikiwa na wananchi watapata mbolea ya ruzuku ambayo imetolewa na serikali ili kuwapunguzia gharama kubwa ya mbolea iliyokuwapo kabla ya mfumo huu.

Kanali Laban alisema amekutana na kamati iliyoundwa kutoka Wizara ya Kilimo ambayo iko mkoani Ruvuma kwa lengo la kufanya tathmini ya ufuatiliaji wa mbolea ya ruzuku.

"Nawaagiza wakuu wa wilaya fuatilieni usambazaji wa mbolea na kuhakikisha zinawafikia wananchi. Kama kuna mtu yeyote anaficha mbolea achukuliwe hatua," alisisitiza.

Awali, akitoa taarifa ya upatikanaji wa mbolea katika Wilaya ya Mbinga, Mkuu wa Wilaya hiyo, Aziza Mangosongo, alisema Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga pekee hadi sasa kuna mbolea zaidi ya tani 2,600 na kwamba juzi ilipokea tani 1,200 za mbolea ya ruzuku.

Mkuu huyo wa Wilaya alisema wanatarajia kutumia Vyama vya Ushirika vya Msingi (AMCOS) kupeleka mbolea kwa wananchi ili kupunguza kero ya umbali.

Mkoa wa Ruvuma kwa miaka minne mfululizo umekuwa kapu la chakula la taifa kwa kuongoza katika uzalishaji wa mazao ya chakula nchini.

# Afungwa kifungo cha nje mauaji ya shemeji yake bila kukusudia

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, imemhukumu Silas Tugala, kifungo cha nje cha miaka miwili, baada ya kupatikana na hatia ya kumuua bila kukusudia shemeji yake, Peter Elias, aliyekwenda nyumbani kwao kwa ajili ya kusuluhisha ugomvi wa wanandoa hao.

Hukumu hiyo ilitolewa juzi na Hakimu Mkazi Mkuu, Susan Kihawa, baada ya kuzingatia kuwa ni kweli mshtakiwa alimchoma kisu Elias kutokana na ugomvi ambao ulikuwa umetokea.

Alisema ugomvi huo ulikuwa kati ya mke na mume lakini mke alitoka ndani ya nyumba na kukimbilia nje, kwa hiyo kama ndugu zake yaani Elias na Moses Elias, wangemchukua dada yao, Florence, wakaondoka naye basi mauaji hayo yasingetokea.

"Ndugu hawa walitakiwa watumie busara kuwa dada yao amegombana na shemeji yao na shemeji yao yuko ndani kafunga mlango na kuna giza. Wao walitakiwa kuondoka na kurudi siku nyingine lakini waliingia kama vibaka katika nyumba ya mshtakiwa," alisema.

Kutokana na hali hiyo, hakimu alibadilisha kesi hiyo kutoka mauaji hadi kuua bila kukusudia kwa sababu Elias na kaka yake Moses waliingia ndani na kuanza kugombana na shemeji yao.

"Mahakama inakuhukumu kifungo cha nje cha miezi 24 kwa kuzingatia muda uliokaa mahabusu wa miaka sita, umri wa mshtakiwa, una wategemezi wengi wanaokutegemea na pia hakuua kwa kukusudia.

"Kwa sababu hata mshtakiwa na marehemu walikuwa marafiki, hawakuwa na ugomvi wowote, kwa hiyo mshtakiwa anajutia kosa lake," alisema Kihawa.

Kabla ya hukumu hiyo kutolewa, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Grace Mwanga, aliomba mahakama itoe adhabu kali kwa mshtakiwa huku upande wa utetezi ukiomba mahakama izingatie muda wa miaka sita aliokaa gerezani, umri wa mshtakiwa miaka 62 na pia ana wategemezi wengi wanaomtegemea na pia ni kosa lake la mara ya kwanza.

Katika kesi hiyo, mke wa Silas (Florence) na mtoto wake, Rebeca walitoa ushahidi dhidi yake wakidai kuwa mshtakiwa ni mgomvi hata siku ya ugomvi majirani hawakuthubutu kufika katika nyumba ya mshtakiwa kwa kumhofia.

Florence alidai wakati wa kurupushani zinatokea nyumbani kwake na wadogo zake wawili kuchomwa visu na shemeji yao, alipiga kelele kuomba msaada kwa majirani lakini hakuna aliyethubutu kwenda kwa madai kuwa mume wake ni mkorofi sana.

Katika ushahidi wa Rebeca, aliomba mahakama kuchukua maelezo alioyatoa mahakamani hapo kwani maelezo hayo ndio anauhakika nayo na sio maelezo aliyoyatoa kituo cha polisi wakati tukio limetokea.

Tugala alishtakiwa kumuua kwa kukusudia Peter Elias Januari 19, 2017 eneo la Mbezi Juu, Dar es Salaam.




Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani wa Benki ya Absa Tanzania, George Binde (kushoto), akikabidhi madawati 37 yenye thamani ya Sh. milioni 10 yaliyopatikana kwa michango ya wafanyakazi wa benki hiyo, kwa Mkuu wa Shule ya Msingi Uhuru Mchanganyiko, Sezaria Kiwango, katika hafla iliyofanyika shuleni hapo, Kariakoo, Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Dalili uwapo mafuta Kilosa zaonekana

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

SHIRIKA la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) kwa kushirikiana na Kampuni ya Swala, linaendelea na utafiti katika kitalu cha Kilosa - Kilombero kilichoko mkoani Morogoro baada ya kuonyesha miamba yake kuwa na dalili za kuwepo kwa mafuta.

Ofisa kutoka Idara ya Mkondo wa Juu wa TPDC, Gastony Canuty, alisema hayo juzi kwenye mafunzo ya waandishi wa habari wa mkoa wa Morogoro yaliyolenga kuwajengea uwezo wa kuandika na kutoa taarifa sahihi zinazohusu mafuta na gesi asilia yaliyofanyika kwa siku moja mjini hapo.

Canuty alisema utafiti uliofanyika unaonyesha kitalu hicho ambacho kinaunganisha wilaya za Kilosa na Kilombero huenda kikawa na mafuta na kwa sasa kazi inayofanyika ni kuanza kuchimba kisima kuona kwamba hayo mafuta yapo na kwa kiasi gani.

"Kazi inayoendelea hivi sasa ni maandalizi ya uchimbaji kisima ili kujua hayo mafuta kama yapo na kwa kiasi gani na kazi hiyo inafanywa na kampuni ya Swala ambayo ina wazalendo wa hapa nchini," alisema.

Canuty alisema TPDC inaendelea na utafutaji, uzalishaji, uchakataji, usambazaji wa gesi asilia, uhifadhi na biashara ya mafuta ili kuhakikisha uwapo wa nishati ya kutosha nchini.

Alisema mpaka sasa kiasi cha gesi asilia kilichogundulika ni futi za ujazo trilioni 57.54 ambazo zimejumuishwa za nchi kavu trilioni 10.41 na baharini trilioni 47.13.

Kwa mujibu wa Canuty, sehemu ya kiasi hicho kinatumika katika miradi mbalimbali ikiwamo kuzalisha umeme na kwamba zaidi ya asilimia 70 ya umeme unaozalishwa katika gridi ya taifa unatokana na gesi asilia na kuendeshea mitambo viwandani.

"TPDC mpaka sasa kwa nchi kavu tumegundua eneo la Songo Songo, Mnazi Bay, Mkuranga, Ruvuma eneo la Ntorya pamoja na Ruvu na gesi asilia inayotumia ni ile ya Songo Songo na Mnazi Bay," alisema Canuty.

Ofisa huyo alisema kwa sasa mikataba ya uzalishaji na ugawanaji inayofanya kazi iko 11, ikiwamo mitano ya utafutaji nchi kavu, mitatu utafutaji katika kina kirefu cha bahari na mitatu ni ya uendelezaji.

Avitaja vitalu vitano vyenye leseni za utafutaji maeneo ya nchi kavu na kampuni zake kwenye mabano ni Ruvu (DODSAL ), Ruvuma (ARA), Kilosa - Kilombero (Swala), Tanga (AFREN) na Nyuni (Ndovu Resources).

Pia alisema vitalu vingine vina leseni ya utafutaji kina kirefu baharini na kampuni zake katika mabano ni kitalu namna 1 & 4 (Shell, Ophir na Pavillion Energy), kitalu namba 2 ( Equinor Exxonmobil).

Vingine vitatu, alisema vina mikataba yenye leseni ya uendelezaji nchi kavu na kampuni zake kwenye mabano ni Songo Songo (PAET), Kiliwani North ( Ndovu Resources) na Mnazi Bay ( Maurel & Prom).

Alisema kazi inayoendelea katika kitalu cha Ruvu ni uchakataji na utafsiri wa data za mitetemo za 3D kilometa za mraba 481 umekamilika na maandalizi ya uchorongaji wa visima viwili kwa sasa unaendelea.

Katika kitalu cha Ruvuma eneo la Ntorya alisema, kazi inayoendelea ni ukusanyaji wa data za mitetemo za 3D ambayo imekamilika.

## NBC yafunga mauzo hati fungani ya Twiga

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC) imetangaza kufunga mauzo ya hati fungani yake iliyofahamika kama NBC Twiga Bond kwa mafanikio makubwa.

Mauzo hayo yamekuwa na mafanikio baada ya kukusanya Sh. bilioni 38.9 ikilinganishwa na zilizotarajiwa kukusanywa awali.

Akizungumza kwenye hafla fupi ya utangazaji wa matokeo ya mauzo ya hati fungani hiyo iliyofanyika Dar es Salaam juzi, iliyohudhuriwa na wadau mbalimbali wakiwamo Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) na Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Mkurugenzi wa Biashara wa NBC, Elvis Ndunguru, alisema dhamana hiyo ya mwezi mmoja ilifungwa rasmi Desemba 7, mwaka huu.

"Awali lengo letu lilikuwa kukusanya takribani Sh. bilioni 30 na tumefunga hati fungani hii tukiwa tumekusanya Sh. bilioni 38.9 ambazo ni sawa na asilimia 130 ya malengo yetu ya awali. Kiasi kilichopatikana kimetoka kwa wawekezaji takribani 661 kutoka sekta mbalimba wakiwamo wawekezaji binafsi wakubwa kwa watoto chini ya usimamizi wa wazazi, taasisi na mashirika mbalimbali kutoka kila kona ya nchi," alisema Ndunguru.

Kwa mujibu wa Ndunguru, hiyo ni mara ya kwanza kwa benki kutoa hati fungani kwa ajili ya umma na ikiwalenga wajasiriamali, wakulima na wafanyabiashara wadogo ambao ndio sehemu kubwa ya ajira za vijana nchini Tanzania.

"Wawekezaji katika hati fungani ya NBC Twiga Bond watapata riba kubwa ya asilimia 10 kwa mwaka, inayolipwa nusu mwaka katika kipindi chote cha miaka mitano hadi Novemba 2027. Kiwango cha riba kinacholipwa hakina punguzo la kodi," alisema.

Hati fungani ya Twiga ni ya kwanza kutolewa na NBC na inatarajiwa kushughulikia sekta zingine muhimu za uwezeshaji kiuchumi, changamoto ya ufadhili wa mikopo midogo na ya kati nchini.

Kwa mujibu wa Ndunguru, benki hiyo itaendelea kutangaza hati fungani zaidi kwa kuwa lengo ni kukusanya Sh. bilioni 300 ambazo zitatumika katika kufadhili sekta ndogo na za kati, kilimo na sekta zinginezo muhimu kiuchumi nchini.

Akizungumzia zaidi mafanikio hayo, Mkurugenzi wa Hazina na Masoko NBC, Peter Nalitolela, alisema hati fungani hiyo imekuwa sehemu ya fursa kwa Watanzania kuwa sehemu ya ukuaji wa benki hiyo.

"Mafanikio haya yanaonyesha imani kubwa waliyo nayo Watanzania kwa Benki ya NBC na zaidi wanavutiwa na huduma za benki hii kongwe katika huduma za kifedha," alisema.



# Wanawake waanzisha kiwanda kuchakata muhogo

**Na Oscar Assenga,** MKINGA

WANAWAKE 40 ambao ni wajasiriamali wameungana na kuanzisha kiwanda cha kuchakata muhogo ili kuliongezea thamani.

Hali hiyo imetokana na kilio cha muda mrefu cha wakulima wa mihogo kukosa soko la uhakika.

Kiwanda hicho cha Mkinga Food Processing Factory, kilichojengwa kwa ufadhili wa Shirika la Misaada la Japan (JIKA), kwa kushirikiana na Shirika la World Vision Tanzania, kwa gharama ya zaidi ya Sh. milioni 150.172, kiko eneo la Kasera, Wilaya ya Mkinga, mkoani Tanga.

Jana, Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la World Vision Tanzania, Makarios Charles, alisema lengo la mradi huo ni kufungua milango na fursa za kiuchumi kwa wanawake kuwekeza katika sekta ya viwanda badala ya kudhani jukumu hilo linawahusu wanaume wafanyabiashara pekee.

"Pamoja na mambo mengine, tunataka kuweka ulinzi kwa watoto kupitia wanawake, ambao watakapozalisha kwa wingi kwa kulima muhogo na viazi lishe na kisha kusindikwa, watakuwa wameleta suluhisho la tatizo hilo."

Alisema shirika hilo ambalo kwa Tanzania lipo katika mikoa 18, kwa Mkoa wa Tanga wako katika Wilaya za Mkinga, Korogwe, Kilindi na Handeni, wakiwa wamejikita kwenye miradi ya kilimo, kuzikwamua kaya maskini kiuchumi na ulinzi wa watoto.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga, Elizabeth Malali, akizungumzia uwekezaji huo, alisema kupitia kiwanda hicho, serikali inatarajia wanawake wataweza kujikwamua kiuchumi na kuzalisha kwa tija.

Alisema kwa mwaka 2021, Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga, ilitoa Sh. milioni 247 kupitia mapato yake ya ndani kwa ajili ya kutoa mkopo usio na riba kwa wanawake, vijana na jamii ya watu wenye ulemavu.

Hata hivyo, mwenyekiti wa kikundi hicho kinachomiliki na kiwanda hicho, Mwanakombo Hussein, alisema kwa kuwa kina uwezo mkubwa wa kusindika muhogo na viazi lishe tatizo litakuwa ni upatikanaji wa malighafi ya kutosheleza kiwanda hicho na soko la bidhaa zitakazosindikwa.

Mbunge wa Mkinga, Danstan Kitandula, alisema kiwanda hicho ni ufumbuzi wa soko la muhogo lililokuwa likiwakabili wakulima wa Wilaya ya Mkinga na Mkoa wa Tanga.

Alisema wakulima waliokuwa wakilalamika mihogo yao kukosa wanunuzi, sasa wamepata kimbilio na kwamba Ofisi ya Mbunge, Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) na Halmashauri ya Wilaya hiyo, kazi yao itakuwa ni kuwatafutia masoko ya uhakika na ya kudumu ya bidhaa zitakazosindikwa kupitia kiwanda hicho.



Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Omary Mgumba (katikati), akikata utepe kuzindua kivuko cha Mv Tanga kilichokarabatiwa na Wakala wa Ufundi na Umeme Nchini (TEMESA) kwa zaidi ya Sh. bilioni 1, juzi wilayani Pangani. (Wa tatu kulia) ni Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Ludovick Nduhiye na (wa tatu kushoto) Mbunge wa Pangani, Juma Aweso. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA**

# DC aagiza madarasa yanayotishia usalama wa wanafunzi yakarabatiwe

**Na Mwandishi Wetu,** HAI

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, ameagiza Halmashauri ya Wilaya ya Hai kutoa sehemu ya mapato yake ya ndani na kuelekeza katika ukarabati wa madarasa chakavu yanayotishia usalama wa wanafunzi na walimu. Miongoni mwa shule chakavu zinazotishia usalama hivi sasa ni Shule ya Msingi Narumu, Usari na Roo, ambazo licha ya uchakavu wa vyumba vya madarasa, havina vyoo vya walimu.

Babu alitoa agizo hilo juzi alipokuwa katika Shule ya Sekondari ya Hai, wakati wa ukaguzi na makabidhiano ya vyumba 10 vya madarasa yaliyojengwa na serikali.

Babu aliagiza halmashauri hiyo pamoja na halmashauri nyingine za Mkoa wa Kilimanjaro, kutumia fedha za ndani kukarabati madarasa chakavu.

"Hai na halmashauri nyingine, nataka suala la ukarabati wa madarasa chakavu liwe ajenda muhimu kuanzia sasa. Nitapita kuangalia agizo langu kama linatekelezwa kwa kiwango gani na watakaopuuza sitawachekea, nitawawajibisha," alisema.

Mbali na vyumba vya madarasa, Novemba mwaka huu, Mkuu wa Wilaya ya Hai, Juma Irando, akizungumza na madiwani wa wilaya hiyo, alieleza masikitiko yake kuhusu shule za sekondari za Tumo na Roo, wanafunzi kupishana kwenye mlango wa choo na walimu wao, kutokana na shule hizo kukosa vyoo.

Diwani wa Kata ya Machame Narumu, John Lengai, alinukuliwa akisema katika kata yake pekee kuna shule mbili za msingi na moja ya sekondari, ambazo hazina vyoo na walimu wake wanasubiriana mlangoni na wanafunzi wakati wa kujisaidia.

Alisema kuwa walimu wa kike wa Shule ya Msingi Usari, wao hawana vyoo na wanalazimika kuomba huduma hiyo katika vyoo vya watawa wa Kanisa Katoliki, Parokia ya Narumu.

Mbunge wa Hai (CCM), Saashisha Mafuwe akizungumzia miundombinu ya shule na hali ya vyoo katika jimbo hilo, alisema shule nyingi za msingi na sekondari wilayani humo zilijengwa kuanzia mwaka 1920 hadi 1950, hivyo nyingi ni chakavu sana.

# Maofisa elimu watakiwa kuwabaini watoto wenye mahitaji

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Angellah Kairuki, amewaagiza maofisa elimu maalum nchini, kuhakikisha wanasimamia uchunguzi wa awali wa watoto, ili kubaini watoto wenye mahitaji maalum katika jamii.

Kairuki alitoa agizo hilo jana alipokuwa katika Chuo cha Ualimu Patandi kilichoko wilayani Arumeru, mkoani Arusha wakati wa ufunguzi wa mafunzo kwa maofisa elimu watu wazima na maofisa elimu maalum.

Aliwataka kuhakikisha wanatumia vituo vya uchunguzi na kuwaelekeza watoto wenye mahitaji maalum katika shule stahiki ambazo wanapaswa kupelekwa ili wapate afua stahiki. "Nafahamu mkiwabaini watoto hawa wenye mahitaji maalum watapata stahiki zao zinazotakiwa bila shida, hivyo lazima msimame katika kuwafanyia watoto uchunguzi wa kina ili kuwabaini," alisema. Pia alielekeza shughuli za usimamizi na uendeshaji wa elimu zihusishe kikamilifu masuala ya elimu maalumu na elimu ya watu wazima, kwa kuhakikisha wanashirikiana na viongozi katika jamii kuratibu shughuli za elimu ya watu wazima na elimu maalum katika shule za msingi na sekondari. "Lakini nyie maofisa wekeni utaratibu wa kupokea wanafunzi wenye mahitaji maalumu wa kidato cha kwanza, darasa la kwanza na awali kwa mwaka 2023, kwa kushirikiana na viongozi katika maeneo yao, ili kuweka mazingira bora kwa wanafunzi hao," alisema.

Kairuki aliagiza viongozi wa elimu katika ngazi ya shule, kata, halmashauri na mikoa kufuatilia ufundishaji na ujifunzaji shuleni na kushirikiana na walimu katika kuhakikisha wanafunzi wanapata umahiri uliokusudiwa badala ya kukaa ofisini.

Alisema kila mwalimu anapaswa kujiwekea malengo binafsi katika masomo anayofundisha na kuhakikisha hakuna mwanafunzi anayeshindwa kupata umahiri uliokusudiwa katika somo lake ifikapo mwishoni mwa kila mwaka.





## TCDC yaingilia sakata wadaiwa sugu mikopo ushirika

**Na Mary Mosha,** MOSHI

HATIMAYE Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), imeingilia kati sakata la wadaiwa sugu wa mikopo ya Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo (SACCOS) na Vyama vya Ushirika wa Mazao (AMCOS), ambao wanatajwa kukwamisha uwekezaji wa shughuli mbalimbali za kiuchumi.

Imesema uamuzi huo unalenga kuvilinda vyama hivyo visitetereke zaidi kutokana na taswira inayoanza kujijenga ya wadaiwa hao kutaka kuvififisha kiuchumi.

Hatua hiyo ilitangazwa juzi na Mrajisi Msaidizi wa Vyama vya Ushirika, Mkoa wa Kilimanjaro, Jackline Senzige, alipokuwa akizungumza na wanachama wa Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo cha ELCT ND Saccos, wakati wa siku ya familia.

Chama hicho kinachomilikiwa na Dayosisi ya Kaskazini ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), kina mtaji wa wanahisa 12,879.

"Tume ya Maendeleo ya Ushirika, kupitia kitengo chake cha tafiti na mafunzo kimehakiki madeni chechefu, hasa kwa wadaiwa ambao mikopo imepita muda wake katika vyama vya akiba na mikopo na tayari kimewaandikia notisi (ilani) ikiwataka wadaiwa sugu kulipa madeni hayo mara moja.

"Wapo baadhi ya wanachama wasio waaminifu, huchelewesha mikopo na hivyo kurejesha jitihada za maendeleo nyuma. Lengo la uanzishwaji wa vyama hivi ni kuhakikisha vinawakopesha wananchi kwa gharama nafuu ili kuwainua kiuchumi, lakini kwa yoyote anayechelewesha rungu hili lazima limpate, kwa kuwa anachelewesha jitihada za maendeleo." alisema.

Kabla ya kauli hiyo ya Mrajisi Msaidizi, Mhasibu Mkuu wa chama hicho, Elifuraha Mduma, alisema kwa mwaka 2023, wanatarajia kutoa mikopo ya zaidi ya Sh. bilioni 19, kusajili wanachama wapya zaidi ya 2,000.

# Siha waanza kampeni kutokomeza magonjwa tishio

**Na Anjela Mhando,SIHA**

KAMPENI ya nyumba kwa nyumba inayolenga udhibiti wa magonjwa saba tishio kwa uhai wa watoto wenye umri chini ya miaka mitano, imeanza kutekelezwa kwa kutumia huduma mkoba inayovihusisha vijiji 60 vya Wilaya ya Siha, mkoani Kilimanjaro.

Udhibiti wa magonjwa hayo kupitia chanjo, unayahusisha maradhi ya rubella, surua, kifua kikuu, polio, rota, nimonia na kuzuia ulemavu wa ghafla inatekelezwa kwa siku 10.

Akizungumzia jana kampeni hiyo ya huduma mkoba kwa chanjo jumuishi, Mratibu wa Huduma za Chanjo wa Wilaya hiyo, Paul Issack, alisema chanjo hiyo ilianza kutolewa jana na itaendelea kutolewa kwa watoto wote hadi ifikapo Desemba 24 mwaka huu.

"Tunapita nyumba kwa nyumba vijiji vyote 60 kutoa chanjo kwa watoto ambao aidha hawajapata chanjo kabisa kwa kipindi cha umri wao kutoka kuzaliwa mpaka miaka mitano au katika ratiba ya kawaida ya chanjo, hawajafanikiwa kukamilisha ratiba yao ya chanjo.

"Chanjo ambazo zinaenda kutolewa ni chanjo zote, ambazo ziko kwenye utaratibu wa kawaida wa kliniki. Ninawaomba wazazi na walezi wenye watoto ambao hawajapata chanjo na wamefikisha umri wa kupata chanjo au hawajakamilisha ratiba ya chanjo kutokana na sababu mbalimbali.

"Wawaandae watoto wao kwa ajili ya kupatiwa huduma hii muhimu ya chanjo ili kuzuia magonjwa yote yanayozuilika,"alisema Issack

Mkuu wa Wilaya ya Siha, Thomas Apson, akizungumza katika kikao kazi cha utoaji wa chanjo jumuishi kwa shule za msingi, alisisitiza kuwa jamii inapaswa kutilia maanani umuhimu wa chanjo hizo, hasa chanjo ya rota ambayo kirusi chake huongoza kusababisha ugonjwa wa kuharisha kwa watoto wadogo.

Tafiti zinaonyesha kuwa kila mtoto duniani kabla ya kufikisha umri wa miaka mitano, atakuwa ameambukizwa angalau mara moja na kirusi huyo.



Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Charles Makongoro Nyerere (katikati), akipokea zawadi ya picha kwa Teddy Bayo aliyopiga na Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Manyara, Peter Toima, baada ya kutembelea vijana wajasiriamali wa Dream Studio wilayani Hanang' juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# CCM yatoa msaada matofali 200 ujenzi zahanati

**Na Anjela Mhando,** SIHA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro kimetoa msaada wa tofali 200 kwa wananchi wa Kijiji cha Mowonjamu kilichoko Kata ya Livishi ambao wako katika ujenzi wa Zahanati ya Mowonjamu.

Ujenzi wa zahanati hiyo utasogeza karibu huduma za tiba na uchunguzi wa kitabibu, baada ya kuzifuata umbali wa zaidi ya kilometa 20 katika kata jirani.

Hatua ya CCM kutoa msaada huo ni baada ya wakazi hao kuanza ujenzi wa zahanati hiyo kwa nguvu zao kwa kutoa mchango wa saruji, tofali, mawe na fedha.

Akizungumza jana wakati wa hafla ya kukabidhi tofali hizo, Katibu wa Siasa na Uenezi wa CCM, Wilaya ya Siha, Emanuel Mushali, alisema chama hicho kimeguswa na mchakato huo hivyo kulazimika kuwaunga mkono, baada ya kuona kuna wazee wenye umri wa miaka 90 wameweza kuchangia mradi huo wa ujenzi.

"Kujitolea kwetu ni jadi na desturi yetu au utamaduni wetu. Wananchi pale wanapokuwa na jambo lao, hatutasita kuwaunga mkono, ndiyo maana tumewaletea tofali 200 kwa ajili ya kuwasapoti kuendelea na ujenzi wa jengo hili la zahanati,"alisema

Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Mowonjamu, Julius Masawe, alisema wamekubaliana kuchangia kila familia ili kuchangia ujenzi huo ukamilike na kumaliza adha hiyo ya kufuata huduma za afya katika Hospitali ya Wilaya ya Siha iliyoko Sanya Juu pamoja na Hospitali ya Rufani ya Taifa ya Magonjwa Ambukizi ya Kibong'oto.

Alisema mradi huo unatarajia kugharimu kati ya Sh. milioni 120 hadi Sh. milioni 150 kutokana na michoro ya Wizara ya Afya.

Diwani wa Livishi, Lukasi Nkini, alisema wananchi wa kijiji hicho wameamua kuanza ujenzi wa zahanati hiyo na wanategemea itakapokamilika itawahudumia na kuondokana na adha waliyokuwa wakiipata ya kutumia gharama kubwa za usafiri.

"Nimatarajio yangu serikali itatuunga mkono kwasababu kwenye fedha za mfuko wa jimbo nimeshaomba halmashauri mahali hapa ili kuisapoti jamii kwenye hizi nguvu ambazo wamekwisha kuzianza," alisisitiza Nkini.



Ukurasa 17

Chifu Hangaya endelea kutenda wema wende zako salama


# BUFE

IJUMAA DESEMBA 16, 2022

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

Nipashe




**Naibu Waziri Mary Masanja: Soko la asali kubwa sana, linatusubiri**

Ukurasa 15

# Watafiti washtukia athari tabianchi, zinamletea hatari kichanga tumboni

**Na Mwandishi Wetu**

VIWANGO vya joto vinaweza kuathiri afya ya kijusi tumboni. Kulingana na utafiti wa hivi karibuni, mjamzito anayefanya kazi katika eneo lenye joto kali, anaweza kumdhuru mtoto anayembeba tumboni.

Miongoni mwa athari zinazotajwa kuweza kujitokeza ni pamoja na ongezeko la mapigo ya moyo ya kijusi na kupungua kasi ya damu kusambaa katika kiunga mwana (umbilical cord).

Watafiti wanasema mikakati yenye ufanisi inahitajika kuwalinda wajawazito wanaokabiliwa na athari za mabadiliko ya tabianchi yanayosababisha kupanda kwa viwango vya joto. Ni hali inayokumba maeneo mbalimbali ya dunia.

Utafiti uliochapishwa katika jarida la kiafya liitwalo Lancet Planetary Health, anafichua kila ongezeko la nyuzi joto la joto la kupindukia, husababisha ongezeko la asilimia 17 ya shinikizo kwa kijusi tumboni.

Licha ya utafiti umefanyika kuhusu athari za joto kwa wajawazito wanaoishi katika nchi zinazoendelea, inaaminiwa inagusa kote na ni utafiti wa kwanza kuchunguza athari za joto la juu kwa wanawake wajawazito wanaoishi katika nchi zenye pato la chini.

Kuna mfano, wanaofanya kazi katika mashamba ya mpunga katika eneo la West Kiang, Gambia hushinda kwenye jua na joto kali kwa saa nane, nyuzi joto takriban 45, wakati wa msimu wa mvua, kiwango cha juu cha unyevunyevu husababisha joto ambalo ni gumu kuhimili.



Dk. Ana Bonell, akifanya uchunguzi wa uhusiano baina ya tabianchi na ulezi wa ujauzito. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

Wataalamu, kwa usaidizi wa vifaa vya kupima afya ya mtoto tumboni (ultrasound), walirekodi kiwango cha joto cha vijusi na vipimo vilifanywa baada ya wanawake kuanza kazi na baada ya kumaliza siku ya kazi.

Wataalamu pia walichunguza athari za joto kwa kinamama, mfano hali ya maumivu ya kichwa, uchovu na kichefuchefu. Hapo, mchunguzi Dk. Ana Bonell, anasema kuwa kuhangaika kwa kijusi kulishuhudiwa katika nyuzijoto 33.

Pia, Daktari Bonell, anasema: "Tulishituka sana kubaini kuwa vijusi viliathiriwa na joto la juu. Kwa upande wa kijusi, tuliona mapigo ya moyo yakiongezeka kwa viwango vya juu kupita kiasi. Hali mbaya sana!"

Anasema jamii imeshuhudia athari katika mzunguko wa damu, kwa sababu mfuko wa uzazi pia uliathiriwa na joto hilo, huku majibu yakiwa mabadiliko ya tabianchi ndio sababu kubwa.

"Ni muhimu kuhakikisha kwamba wanawake wote kote duniani wana mimba salama. Inapaswa kutambuliwa kuwa tukiwa na mabadiliko ya tabia nchi, tunakuwa na viwango vya juu vya joto, hususan mawimbi ya joto.

"Kama hakuna kitakachofanyika, wanawake wanaoshinda katika viwango vya juu vya joto wanakabiliwa na hatari watoto wanaugua wakati wa kuzaliwa. Pia, tunaweza kutarajia uzazi wa mapema au kuzaliwa kwa watoto njiti.

"Tuna matumaini kuwa utafiti huu utawanusuru wanawake wengi na watoto wao. Lakini pia, mapambano dhidi ya mabadiliko ya tabia."

Daktari Bonell anasema kuwa, utafiti zaidi unahitajika kuchunguza athari za kusambaa damu katika kijusi na ni muhimu kutambua athari za sumu zinazotengenezwa na mama wakati wa joto kali katika ukuaji wa kijusi.

Hali hiyo inatawala, huku wanaume wengi wanasimulia kawaida ya kuahirisha mpango wa kuwa baba, mpaka wanapotimu miaka 35, kwa sababu ya elimu ndogo waliyo nayo, pia malengo ya kitaaluma kwa maana ya masomo zaidi, kikazi na kimaisha.

- ***Kwa mujibu wa BBC***



Ulivyo ujauzito.

BIASHARA

# Buyuni Festival; kinamama 13 wanaotoa jibu jinsia yao inauweza uchumi wa bluu

**Na Jenifer Gilla**

SAA tatu kamili asubuhi, Shangwe na vigelegele vinatawala katika mwalo wa samaki wa Buyuni, Kigamboni Dar es Salaam, jumla ya kinamama 13 wa kikundi cha Buyuni Yetu wanaingia uwanjani kwa furaha wakisindikizwa na nyimbo zenye kuashiria ushujaa, huku umati uliowazunguka hauamini kinachoendelea.

Furaha iliyopitiliza kutoka kwa wanawake hao, inatokana na kuzishinda changamoto mbalimbali wanazopitia wenzao wengi nchini wanaojaribu kuzifuatilia fursa zilizopo katika uchumi wa buluu, ambao haujulikani sana kwa wengi hasa Tanzania Bara.

Ugumu wa kijinsia, unaanzia penye imani iliyojengeka miongoni mwa jamii, kuwa wanawake hawawezi kupenya katika sekta hiyo.

Mwenyekiti wa kikundi cha wanawake cha Buyuni Yetu, Fatuma Mwalimu, anaiambia Nipashe kuwa sherehe hiyo ni matokeo ya kudumu kwa mwaka mmoja katika shughuli za kujitafutia kipato baharini, pamoja na changamoto kubwa wanazokutana nazo.

Anasema, tangu waingie kwenye uchumi wa bahari kwa kutengeneza urembo unaotokana na mabaki ya samaki, maisha yao yamebadilika na kufikia hatua ya kuwasaidia waume zao majukumu ya nyumbani, ikiwamo kununua chakula na vifaa vya shule vya watoto.

"Tuliamua kuanzisha kikundi hiki kwa ajili ya kusaidiana na kupeana moyo katika shughuli za bahari kwa sababu kazi ni ngumu, lakini tulichoka kukaa nyumbani wakati fursa tunaiona Mungu ametuletea karibu kabisa na makazi yetu.Tukaamua kuingia mzigoni, sasa kikundi kina Sh.700,000 benki baada ya kutoa hela za sherehe, hatukutegemea kufika hapa tulipo" anasema Fatuma.

Mwanakikundi cha Buyuni Yetu, Mwajabu Mohamed (54), anasema shughuli ya kutengeneza urembo unaotokana na mabaki ya samaki, umerudisha heshima yake katika familia, baada ya kukaa muda mrefu bila ya shughuli, akibaki nyumbani.

"Aisee, nilikuwa na maisha magumu baada ya kuachana na shughuli za uvuvi, nikawa namtegemea mwanaume ahudumie familia kwa shughuli za uvuvi ambazo hazilipi, alikuwa anazidiwa na mimi roho ilikuwa inaniuma, angalau sasa na mimi naleta chochote nyumbani tunagawana majukumu, sasa namuona mume wangu akijivunia kuwa na mke" anasema.



Mkurugenzi wa Shirika la Aqua Farm (AFO), Jerry Mang'ena (wa kwanza kushoto waliokaa) na Ofisa Mifugo na Uvuvi wa Manispaa ya Kigamboni, Ernest Kamata , wakiwa na wana kikundi cha Buyuni, kusherehekea mafanikio ya kikundi hicho, Kigamboni, Dar es Salaam.

Anasimulia kwamba, kupitia biashara hiyo pamoja na kutengeneza viatu, mikeka na kofia ana uhakika wa kupata Sh. 10,000 kwa siku ambayo inamsaidia kuhudumia familia, ikiwamo kuwapa watoto nauli na pesa ya kutumia shuleni wakati mume wake akihudumia mahitaji mengine.

### MZIZI WA MAFUNZO

Mweyekiti, Fatuma, anasema kuwa miezi sita iliyopita walipata, mafunzo ya namna ya kutengeneza urembo kupitia mabaki ya samaki kwa wataalamu waliofadhiliwa na shirika la Aqua Farms (AFO), iliyowaongezea ujuzi wa kutengeneza aina mbalimbali za urembo.

"Mwanzo tulikuwa tunaenda kuokota na kusafisha kisha kuziuza kama zilivyo, lakini kupitia shirika la AFO sasa hivi tuna uwezo wa kutengeneza aina mbalimbali za urembo ambazo tunaweza kuziuza hata katika masoko ya kimataifa " anasema Fatuma.

Mkurugenzi wa AFO, Jerry Mang'ena, anasema kuwa waliguswa kuwashika mkono kinamama hao baada ya kuona juhudi zao za kujikwamua kiuchumi zikirudishwa nyuma na changamoto mbalimbali ikiwamo ukosefu wa elimu na vifaa.

"Tulikuja hapa kufanya utafiti juu ya viumbe bahari, na moja ya watu tuliokutana na kufanya nao kazi ni hawa wakina mama, tukavutiwa na juhudi zao, tunaona tuwape elimu juu ya teknolojia na vifaa ya kutengeneza vifaa urembo na tunafurahi tukiona kuwa kile tulichowapatia kinangia kuboresha maisha yao," anatamka Jerry.

Aidha, Jerry anasema kuwa mchango wao hautoishia hapo, bado wataendelea kuwashika mkono wanawake hao na vikundi vingine vya kinamama vinavyotafuta riziki kupitia uchumi wa buluu ambapo sasa wataelekea mkoani Kilwa, katika kijiji cha Songosongo kusaidia kikundi kama hicho.

### OFISA UVUVI

Ofisa Uvuvi wa Manispaa ya Kigamboni, Ernest Kamata ,anasema ni jambo la kufurahisha kuona wanawake hao wameziba masikio dhidi ya maneno yanayokatisha tamaa kuhusu dai hawawezi kushiriki katika uchumi wa buluu na hatimaye kuushangaza umati uliohudhuria sherehe hiyo.

Anasema Halmashauri ya Wilaya ya Kigamboni, ipo pamoja nao na imeshaaza kutoa mikopo ya kuwawezesha kinamama wanaotafuta fursa kupitia uchumi wa buluu, ikiwamo kuwakopesha fedha na mitumbwi ya kisasa kwa ajili ya shughuli za uvuvi.

"Tunatoa wito kwa wanawake wote mnaojihusisha na bahari, undeni vikundi kama hichi cha Buyuni Yetu, mvisajili kisha mje halmashauri, mna fungu lenu maalum la mikopo ya maendeleo, tumieni fursa hii kujikomboa kiuchumi na kujiletea maendeleo," anasema.

### CHANGAMOTO ZAO

Amles Mkole, anasema kuwa amekuwa aking'atwa na samaki wenye sumu, akiwamo aina za manyangale, chofu na nyenga wanapokuwa katika shughuli hizo, hali iliyompa ulemavu wa mguu mpaka sasa.

"Samaki hao wanatung'ata mikononi tunavyowashika na miguuni kwa sababu hatuna vifaa vya kujikinga. Alining'ata samaki anaitwa nyenga, nilikaa nyumbani wiki mbili nauguza mguu kwa sababu ulivimba na kuweka usaha, mpaka sasa huu mguu ikifika kipindi cha baridi unauma hivyo nasimamisha shughuli za uvuvi hadi utakapoacha," anasema .

Pia, anataja ugumu mwingine ni kukosa vitendea kazi vya kisasa vya urembo huo, hali inayosababisha watengeneze vifaa hivyo kwa teknolojia ya kawaida ambayo havikidhi kusafirishwa kwa masoko ya nje ya nchi.

Kwa mujibu wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Biashara na Maendeleo, (UNCTAD), wanawake ndio wanaofanya kazi nyingi za utalii wa pwani na baharini na bado wanalipwa mshahara wa chini, wakiwa katika hadhi ya chini na kazi yenye usalama mdogo.

Aidha shirika hilo linasema kama wanawake watawezeshwa kufikia fursa za kiuchumi, ikiwamo uchumi wa buluu na kupunguza pengo la kijinsia, wanaweza kuongeza pato la taifa kwa wastani wa dola trilioni 13 mpaka kufikia mwaka 2030.

Aidha, Uchunguzi uliofanywa na mwansayansi bahari, Frocklin na wenzake, mwaka 2013, wanaonyesha tofauti na wanaume, wanawake hawapo katika kamati za usimamizi wa uvuvi wa kijiji au vikundi vya wafanyabiashara rasmi wa samaki hali inayochangia sauti zao kutosikika.



Wakazi wa Buyuni, Manispaa ya Kigamboni, wakiangalia filamu inayohusu jongoo bahari iliyofanywa katika ukanda wa bahari ya pwani, katika hafla hiyo. **PICHA ZOTE: JENIFER GILLA.**

### NINI KIFANYIKE?

Mtafiti wa viumbe bahari kutoka Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam, Prof Philip Bwathoni, anashauri elimu itolewe kwa jamii, kubadili mtazamo hasi walionao kuwa wanawake hawawezi kushiriki katika shughuli za bahari.

"Zaidi tunapaswa kuwaelimisha wanaume wanaoishi katika jamii inayojihusisha na uchumi wa bahari kwa sababu hawa ndio wanawazuia wake zao kuingia baharini, tukianza na hawa basi tutakuwa tumeokoa wanawake katika jamii hizo," anasema.

Anasema pia kazi kubwa ifanyike kuwashawishi wanawake kujihusisha na shughuli za uvuvi kwa sababu wanadhani hawaruhusiwi kujishughulisha baharini, lakini kuwashika mkono kwa kuwapatia elimu na vifaa kutawarahisishia kubadili hali hiyo.

BIASHARA

# Naibu Waziri Mary Masanja: Soko la asali kubwa sana, linatusubiri

**Na Christina Haule, Morogoro**



Mizinga ya nyuki iliyoandaliwa kisasa. **PICHA ZOTE: MAKTABA.**

KUFANYA shughuli za usimamizi endelevu wa misitu wenye kuleta tija kwa kuwekeza kwenye ufugaji nyuki na kufanya biashara yenye faida mara 10 zaidi, kunatajwa kusaidia uhifadhi misitu kuliko kukata, kuchoma na kuuza mkaa kiholela ambayo ina faida ndogo.

Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja, anasema biashara na masoko ya asali ni kubwa, ndani na nje ya nchi na asali inayohitajika haijakidhi mahitaji sokoni.

Anarejea gunia la mkaa huuzwa shilingi 10,000 kijijini na likifika mjini huongezeka bei hadi shilingi kati ya 20,000 hadi 25,000, huku mti mmoja unaokatwa unachomwa mkaa hupatikana gunia mbili pekee.

Anafafanua mti huo, usingekatwa ungebeba mzinga mmoja wa nyuki na kila baada ya miezi sita, mkulima anavuna asali si chini ya lita 10 hadi 20, wakati lita ya asali kijijini bei yake ni shilingi 10,000 na ikifika mjini inauzwa si chini ya shilingi 15,000.

Naibu Waziri anasema, serikali ipo tayari kutoa mizinga ya nyuki kwa kijiji chochote kitakachohitaji ili kuendeleza utunzaji misitu na kuacha kukata miti kiholela, kwa lengo la kujipatia kipato.

Aidha anawataka wanawake kufanya kampeni ya kulinda misitu, akiendelea: "Mama ukimuona baba amebeba shoka anatoka nje kwenda kukata mti, ongea nae tu taratibu, mwambie aende akavune asali.

"Muandae mizinga kwa kushirikiana, mkishirikiana licha ya kuhifadhi misitu mna nafasi ya kuongeza kipato kwa manufaa ya familia zenu."

Naibu Waziri Masanja anataja faida ya nyuki kibiashara ni nta, maziwa, asali ambazo zina masoko makubwa nje ya nchi. Anasema misitu inayoruhusu uvunaji, uwekwe utaratibu wa kuruhusu wanawake kuvuna uyoga, jambo litakalosaidia kufanya biashara huku wakihifadhi misitu.

Mary anasema juhudi za pamoja za kinamama, zinawahitaj vijana kutunza na kusimamia misitu, kwa sababu ndio watumiaji wakubwa wa misitu kuendeleza shughuli zao kuanzia mkaa, hadi mbao.

**WAHIFADHI MISITU**

Ofisa wa Kujenga Uwezo kutoka Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG), Simon Lugazo, anasema wanatekeleza miradi ya ufugaji nyuki kwenye milima ya TAO la Mashariki, Usambara Magharibi - Korogwe na Lushoto, Chome.

Pia, anataja ujenzi wa kiwanda cha kuchakata asali chini ya wanajamii husika kilichopo milima ya Bungu wilayani Korogwe, mkoani Tanga, wana zaidi ya watu 300 wanaoelimishwa ufugaji nyuki na baadhi yao wamenufaika kifedha, ikiwemo kupeleka watoto shule hadi vyuo vikuu, ujenzi wa nyumba na kuondokana na umaskini.

Lugazo anafafanua kuwa, kiwanda hicho kilifika mbali hatua ya kufungasha asali, kuweka nembo na kuuza kwa soko la ndani, akisema TFCG kwa kushirikiana na Mtandao wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu ya Jamii Tanzania (MJUMITA), Shirika la Kuendeleza Nishati Tanzania (TaTEDO) la Uswisi (SDC), uzalishaji waliofanya walishindwa kutimiza masoko ya nje, kwa sababu ya uzalishaji mdogo.

Anaeleza kwamba walitakiwa kupeleka tani mbili ambazo ni kilo 2000, lakini walishindwa hata wakaishia kumudu kilo 200 pekee kwa wiki, akifafanua: "Ikumbukwe kuwa wanakozalisha asali ni maeneo ya milimani ambako huzalisha asali mara mbili kwa mwaka, tofauti na wanaozalisha kwenye maeneo ya misitu ya miombo ambao huzalisha mara nyingi."

**WANUFAIKA**

Mnufaika wa ufugaji nyuki, Halima Juma (45), mkazi wa kijiji cha Maramba wilayani Mkinga, mkoani Tanga anasema ufugaji nyuki umemsaidia katika kufanikiwa kimaisha akaondokana na umaskini, akijenga nyumba, yenye umeme na anasomesha watoto wake, kutokana na kipato cha mazao ya nyuki.

Halima anasema, Umoja wa Hifadhi ya Misitu ya Usambara, Kaya ya Mhinduli wilayani Mkinga (UMAKAMO), alipata elimu ya ufugaji nyuki akiwa na wenzake jumla yao 10, mwaka 2011 kutoka shirika la TFCG na akapatiwa mizinga mitano. Kwa sasa, kikundi chao wamebaki watano.

Anasema alihamasika baada ya kuona mafanikio ya kikundi cha wavuna asali, wakachongesha mizinga 10 akiwa na mumewe mwaka 2013 na akaendeleza ufugaji nyuki wadogo anaosema hawana hasara, wala hawampi mfugaji majeraha na asali yake ina bei kubwa.

Anafafanua kuwa, lita ya asali ya nyuki wadogo huuzwa shilingi 25,000, wakati nyuki wakubwa ni shilingi 10,000. Kwa sasa anasema wana mizinga 180 ya nyuki wadogo waliyoitundika pembezoni mwa nyumba.



Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja.

Anaeleza huwa anaitumia kupanda maua kama vile maboga na kunde, inayowahamasisha nyuki kutengeneza asali ya kutosha.

Pia anasema, mwaka 2019 akiwa na mumewe waliuza asali ya nyuki wakubwa lita 20 na ikawapatia shilingi 200,000 na wadogo walipata lita 10 na kupata jumla shilingi 250,000.

Vilevile anarejea mwaka 2020 walipata lita saba za asali ya nyuki wakubwa na ikawapatia shilingi 70,000 huku kwa nyuki wadogo walipata lita tano, zikiwapa shilingi 125,000.

Aidha, mwaka jana anasema walipata lita tatu kwa nyuki wakubwa na kupata shilingi laki tatu na kwa nyuki wadogo walipata shilingi 75,000 na uzalishaji huo umeonekana kupungua, kutokana na ukame uliosababishwa na mabadiliko ya tabianchi.

Hivyo, anasema akiwa mama wa watoto watatu awali aliishi kwenye nyumba ya makuti, hakuwa salama na familia yake, sasa yuko huru katika nyumba bora kutokana na pato la asali na anamudu kugharamia masomo ya watoto shuleni.

Anasema mbali ya ufugaji wa nyuki hupambana na changamoto kadhaa ikiwemo uwepo wa mchwa na sisimizi sambamba na kuingiliwa na wezi wa asali.

**KUTOKA TFS**

Kaimu Meneja Mawasiliano wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), Tulizo Kilaga, anataja masoko kubwa ya asali yapo nchini Afrika Kusini, India, Botswana, Namibia, Canada, Dubai, Kuwait, Iraq, Iran, Japan, China na Lebanon.

Pia, anataja wateja wa asali na nta wa Saudi Arabia, Oman, Rwanda, Uganda, Kenya, Ufaransa, Uholanzi, Norway, Ujerumani, Uingereza, Marekani na Ireland.

Anasema wastani wa pato linalotokana na asali nchini ni shilingi milioni 818.4 na nta kwa mwaka huingiza wastani wa Shilingi bilioni 2.6 na mazao hayo yote pato lake linaweza kuongezeka kama uzalishaji utaimarika.

Kilaga anasema karne mbili zilizopita, ufugaji nyuki kibiashara ulianza baada ya kuibuka kwa teknolojia za kukabiliana na wadudu hao na kupanuka kwa soko la asali na mazao yake ikiwemo nta inayotumika viwandani.

Anasema, licha ya kuwa na zaidi ya miaka 100 ukifanyika, bado biashara ya asali duniani ni fursa kwa wananchi, lakini wengi hawajui na Tanzania ni nchi ya pili duniani katika uzalishaji asali, ikiwa nyuma ya Ethiopia.

Kalaga anasema, serikali kupitia Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), inaratibu shughuli za ufugaji wa nyuki na ushauri wa kibiashara kwa wazalishaji na wauzaji wa asali na mazao yake.

UCHUMI

ZIARA KWA WATUMISHI KATAVI...

# Majaliwa awasha moto kwa hujuma na nidhamu kazini, akikabidhi kwa TAKUKURU 'kazi iendelee'

**Na Neema Hussein, Mpanda**

NAAM! Ziara ya siku tatu ya Waziri Mkuu, Kasim Majaliwa mkoani Katavi ilimalizika juzi, hivi sasa akiwa mkoani Rukwa. Kuna tabasamu, pia mchakamchaka ameuacha mkoani hapa ujumbe mkuu 'ama kweli kazi inaendelea.'

Jana safu hii ilikuwa na simulizi alivyozindua Hospitali ya Rufani Mkoa wa Rukwa na kuwaachia tabasamu wana - Katavi, pale alipoamua kusimamia akiondoka na ajenda baada ya siku 15 zijazo iwe imeanza kazi, kuanzia wagonjwa wa nje hadi wodini huduma zinaendelea.

Ziarani humo, pia akaagiza na kusisitiza haja ya watumishi wa umma kukusanyika wote katika ukumbi wa Mpanda Social Hall. Ulikuwa mjadala wa kuanika mambo hadharani akidokeza na hapo hakuficha kitu, akianika ana siri ya walakini wa baadhi yao katika utumishi akiwa na sura kamili ya kuweka kando urafiki.

"Dhamira ya mheshimiwa Rais ni kutomvumilia mtumishi yeyote wa umma atakayefanya ubadhirifu na kukiuka kanuni, sheria na taratibu kwa makusudi," anasema, huku akihoji kwa lugha ya ukali: "Hapa Mpanda kuna mtumishi ambaye amehamishiwa hapa kutoka Igunga, Hussein Salum Nyemba yupo?"

Hapo ndipo mtumishi Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira (MUWASA) Mpanda, akasimama akiitikia kuwapo kwake na Waziri Mkuu, akaendelea na swali: "Ile tabia ya Igunga umeileta hapa ya kutofuata sheria za ununuzi? Ulipoingia ofisini uliona ndio fursa ya watu wote wanaodai MUWASA kuwa 'concert' (kukubaliana) waongeze madai, halafu unawalipa baadaye zinarudi tena jioni.

"Kama yule Mabula Mgawe alikuwa anadai milioni 5.8, ukamtaka adai milioni 9.8 na ukamlipa, ila watumishi wenzio walikwambia hayo sio madai yake, ila ukalipa halafu milioni nne zikarudi tena, zimeenda wapi? Wewe ndio unajua, umesimamia kuharibu mifumo kama ulivyokua unafanya Igunga."

Majaliwa akaendelea kumhoji katika ukumbi huo uliofurika watumishi, huku mhusika amesimama akitamka: "Hata zile pikipiki 30 ulizonunua zilikuwa kwanza zitangazwe na hapa mjini si wauza pikipiki wapo? Watu wa Idara ya Ununuzi walikushauri pikipiki zinapatikana hapa kwa shilingi milioni 2.7 kila moja, wewe ukachukua jukumu la kwenda kununua Dar es Salaam na ukanunua kwa 3,866,000 kila moja!

"Kama ungekua unaguswa usingenunua kwa bei hii, sasa hiyo ni kukiuka maelekezo kanuni za Jipsam! Pia, mmenunua mita 1000 za maji bila ya kufuata taratibu za manunuzi na wala hamkupeleka TBS kukagua ubora wa mita, hizo mmetumia (shilingi) milioni 90?

"Ukaguzi ule ulitakiwa kulipwa TBS (shilingi) milioni 10, mkaanza kutaka hiyo milioni 10 muichukue nyie, mtumie bila ya kwenda kulipa TBS na wala hakuna kibali cha TBS. Watumishi, pamoja na kuzikataa mita hizo sababu hazijahakikiwa na TBS, nyie mmeendelea kuzitumia hapa. Huo ni ukiukaji ununuzi!

"Kule Igunga zile kesi umezimaliza? Una kesi 16 kule, unajua kesi 16 ni 'too much' (zimepindukia) zingekua mbili, tatu sasa hizi za kikiuka manunuzi. Sasa Wizara ilikuleta huku na huku umeshaanza hayo."



Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira (MUWASA), Hussein Nyemba akiwa amesimamishwa kikaoni, akihojiwa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (hayupo pichani).

**AMNYOOSHEA KIDOLE**

"Wewe huwezi kufanya kazi hapa kuna mradi mkubwa wa miji 28, pia unawatisha watumishi wako, unasema wewe umesoma na waziri...Waziri wa Maji ni muadilifu, muaminifu na mchapa kazi nani hajui?" Majaliwa akawahoji watumishi na anaendelea kuwaambia watumishi, huku akitishia kumpigia simu hapo hapo Waziri wa Maji, Jumaa Aweso kupata ufafanuzi.

"Sasa mimi msisitizo wangu kwa watumishi wa namna hii, hatuwezi kuwa nao mahali pa kazi. Amehama mahali amefanya madudu ana kesi, halafu unampeleka mahali pengine na huko tena hakuna utulivu, hili nilikuwa nasisitiza kwamba, tunahitaji matumizi ya mamlaka zetu na madaraka yetu vizuri," anasema.

Hapo Waziri Mkuu anamuagiza Kamanda wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Katavi, akisema:"Nataka kwanza myapitie haya ya hapa Mpanda kabla ya kule Igunga." Hapo Kamanda wa TAKUKURU anapokea maagizo anayoorodheshewa akitamkiwa:

"Manunuzi ya pikipiki 30, manunuzi ya mita 1000, ajira za watu 25 maelezo yangu kutoka wizarani hakuna vibali hivyo wala bodi ya maji Mpanda haijaidhinisha, zile fedha zilizotakiwa kwenda TBS zimechukuliwa na ile nyongeza ya wanaodai maji hii nimechukua moja, lakini zipo nyingine.

"Yule lazima asimame kazi pembeni, wewe unakuwa huru na wale waliopo watakusaidia kazi ya kukupa kila dokumenti pitia zile mita 1000. Pitia zile pikipiki 30 zilizonunuliwa kwa bei kubwa shilingi milioni tatu," anahoji.



Watumishi wa umma mkoani Katavi, waliokusanyika katika kikaona Waziri Mkuu Kassim, katika ukumbi wa Mpanda Social Hall, Manispaa ya Mpanda.

"Huyu mwajiriwa wa Rais, huyu ambaye siwezi kumgusa, aliteuliwa na Rais eeeh sasa! Mimi namsimamisha, huyu sheria inapochunguzwa unakaa pembeni ili upate nafasi ya kupata nyaraka zote ana kesi 16 Igunga, halafu mnamkimbizia huku ndio wanakojaa watu wenye kesi? Nyie hapa Mpanda ndio mahali pa kuharibu zaidi? anahoji Waziri Mkuu.

**IDARA ARDHI**

Pia, Waziri Mkuu akahamishia hoja katika Idara ya Ardhi mkoa Katavi na kuwataka wajitathimini kutokana na migogoro ya ardhi kuwa mingi, akinena, baada ya kumsimamisha bosi katika idara hiyo: "Mjitathimini migogoro ni mingi na mingine hamuitatui kwa makusudi au kwa sababu mnafahamiana au kwa sababu ya kuheshimiana. Wewe sio Abraham Mwandamila Casto? "

Anaendelea: "Nani alikuuzia (ardhi)", akajibiwa "nilinunua kwa watu watatu." Waziri Mkuu anasoma kwenye nyaraka na kusoma mahali alikouza (jina tunalo), Abraham anakubali 'ndio nilinunua kwake'. Kisha Waziri Mkuu anauliza tena eneo la serikali pa kuuzia akinena; "Unakijua kijiji cha Bugwe anaulizwa?'na anajibiwa "ndio anakifahamu akimiliki ekari 500 za shamba."

Waziri Mkuu Majaliwa anaendelea: "Ulinunua bila kufuata utaratibu, serikali ya kijiji haina mamlaka ya kutoa ekari 500 na sasa unawakodisha watu kwenye ekari 500, halafu wanakulipa wewe mazao unaweka na masharti, yaani umeenda kuwasumbua wananchi wakati wewe ni mtumishi wa umma, umechukua eneo lao, unawapangisha tena wananchi.

"Tulitarajia wewe Ofisa Mipango Miji ndio ungewasimamia wale wananchi wapate lile eneo uwagawie wapate na fursa ya kulima wapate kujikimu, hivi wewe na wao nani mwenye shida?' anahoji Waziri Mkuu.

"Huko ni kama huwatendei haki katika hali ya kawaida ya ubinadamu. Umechukua eneo lao wanahangaika na wana mgogoro na serikali ya kijiji, wewe bado unawapangisha wanalima na masharti ya kukupa magunia ya kila zao wanalolima, hiyo mbili tatu?

"Una mgogoro na mtu anayeitwa Michael Mbonabucha? Umeng'ang'ania eneo lake, unashirikiana na Mwenyekiti wa Mtaa wa Mapinduzi hapa mjini, huyu anahangaika anatafuta mahali pa kufanya kazi, wewe umesema eneo lile ni la kwako, inaonekana wewe sababu ni mipango, miji kila eneo unachukua tu," anatamka Majaliwa.

Wakati akitamkiwa yote hayo na Waziri Mkuu, mtuhumiwa alibaki kimya na Majaliwa akaendelea:"Mimi nadhani unapanga maeneo ya watu, kumbe unapanga kwa ajili yako wewe mwenyewe kwa maslahi binafsi, halafu unachukua ardhi kwa kiwango hicho..."

Huku akitoa hisia za hasira na masikitiko, Majaliwa anaendelea: "Unatumia nafasi yako ya Ofisa Mipango Miji, hivi unanikumbuka wewe? "Hapo akamjibu "ndio nakukumbuka!" akaulizwa tena na Waziri Mkuu, "tulikutana wapi?" akajibiwa mwaka 2016," hapo akaulizwa tena na Majaliwa "ilikuwaje... huyu sio mgeni na mie namjua. Nilishawahi kumsimamisha kazi kwa sababu hii hii!

"Wananchi wa Nsimbo wanakulalamikia, ukichukua eneo na umechora mchoro wako hata halmashauri umeikatalia, kuna mchoro wa halmashauri na wewe una mchoro wako na ulishaenda kwa yule wa mkoani, ili upitishe mchoro wako, sema amekukatalia tu!"

Katika mazingira mtumishi huyo wa umma akitaka kujibu, Waziri Mkuu Majaliwa akamcharukia: "Sikiliza bwana, mimi sibahatishi na sijawahi kuonea mtu! Sijawahi kuonea mtu...."



Abraham Casto, Ofisa Mipango Miji Manispaa ya Mpanda, akijieleza kwa Waziri Mku, Kassim Majaliwa. **PICHA ZOTE: NEEMA HUSSEIN.**

**MOTO MWINGINE**

Hapo, pia anamgeukia Ofisa Ardhi mkoa Katavi akimuuliza "ule mchoro umeupitisha?"na hapo hapo anajibiwa haujapitishwa, anaulizwa tena aina ya mchoro anaoukumbuka wa Halmashauri ya Nsimbo au wa huyo Ofisa Ardhi mtajwa,

"Wananchi wanaendelea kulalamika pale Nsimbo yeye ana mchoro wake wa eneo hilo, amechora nini anajua mwenyewe, nyie mmemwambia alete mchoro, hataki kuleta amezuia kila kitu, hata halmashauri isifanye kazi yake huyu ni mtumishi wa umma wa namna gani?"akahoji Waziri huku akigeuka kumtazama kwa hasira.

"Anarudia tena, huyu ni mtumishi wa umma wa namna gani?" akimtaja ameshawahi kumsimamisha wilayani Mpimbwe kwa sababu ya kesi ya ardhi, sasa amehamia Mpanda, amesahau yaliyomkuta. Hapo Waziri Mkuu Kassim Majaliwa anatoa maagizo pia kwa TAKUKURU akisema: "Kwa kuwa mimi nina langu na nina uhakika nalo na wewe unasema kila kitu una uhakika nacho, basi TAKUKURU fanya kazi na huyu pia."

**ATOA AGIZO LA MWEZI**

Akiwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika, nako akaacha maagizo watumishi wanaoishi Mpanda kuhamia wilaya ya Tangayika na maagizo yake yalikuwa kama ifuatavyo.


"Mimi nilishakuja hapa wakati ule mnasafisha uwanja wa kujenga majengo na nilisimama wakati ule, nikahamasisha wananchi kujenga nyumba. Nilipopita tena wakati naenda Mishamo, niliona mji umetanuka kuna taa za barabarani, nyumba nzuri, lakini bado nina taarifa kwamba watumishi mnakaa Mpanda mjini.

"Tumewaleta Tanganyika muhudumie wana - Tanganyika na huduma ni saa 24 asubuhi, mchana, jioni na usiku wa manane, wewe unakaa Mpanda ikitokea dharura saa mbili usiku nani atawajibika kuhudumia?

"Natoa agizo hili la jumla, mheshimiwa Mkuu wa Wilaya, nina orodha kubwa ya watumishi wanaokaa mjini Mpanda. Nawapa mwezi mmoja tu mpaka tarehe 15 Januari kila mmoja ahamie Tanganyika, nendeni mkakae huko," anasema Waziri Mkuu.

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Chifu Hangaya endelea kutenda wema wende zako salama






**NA JOSEPH KULANGWA**

Simu: +255 713 410008
barua pepe: kulangwasos@gmail.com

WE Mtanzania, ukimwelewa Rais Dk, Samia Suluhu Hassan jinsi alivyo na anakotazama, bila shaka utaishi maisha yasiyo na mawaa na hakika utajitolea kuisaidia nchi yako isonge mbele kama anavyopanga yeye.

Ninapofuatilia kauli na matendo yake, huwa nakumbuka na kujiuliza kwa nini siku anatangazwa kuwa mgombea mwenza wa Dk. John Magufuli mwaka 2015, alipatwa na mshituko na kulia, mpaka kubembelezwa na Dk. Jakaya Kikwete.

Si kwamba Samia hakuwa anaitaka nafasi hiyo, ila bila shaka alijiuliza kwanini awe yeye na si mwingine. Alijua anaweza, lakini kwani hakukuwa na wengine wa kushika nafasi hiyo mpaka awe yeye?

Lakini, baada ya kutafakari na kusikia mawazo ya waliomtangulia, wakubwa zake na kuona kuwa kumbe alikuwa akiaminika miongoni mwa Watanzania mpaka kutakiwa kuchukua nafasi hiyo adhimu, alikubali na Mungu si Athumani, kundi lake likashinda mengine ya upinzani.

Kilio cha Samia hakikuwa kinatabiri kwamba siku moja Dk, Magufuli angeitwa na Mungu wake na hivyo yeye kupewa hatamu za uongozi kama alivyo sasa. Yawezekana, baada ya Dk. Magufuli kutangulia mbele za haki, kuna watu waliodhani Samia asingeweza.

Lakini, aliposimama akatangaza kuwa yeye ndiye Rais wa Tanzania katika maumbile ya mwanamke, ndipo watu wakafumbuka macho na kuzibuka masikio na kuamini kuwa, kumbe wana kiongozi madhubuti ambaye angesongesha mbele gurudumu la maendeleo.

Juzi kati hapa, Samia akakutana na kundi kubwa la wanawake wa CCM kupitia Jumuiya yake ya UWT. Kwa kuwa walijua wanakutana na kiongozi wao mkuu na muda mfupi baada ya kuchaguana, wakaandaa mabango kama kawaida, kumfurahisha bosi.

Akayasoma yote na kupata shaka kidogo kwa bango lililosomeka: "UWT Simama na Samia kwa Maendeleo ya Taifa". Akasema hilo hapana, linahitaji marekebisho, ili lisomeke kwa muktadha anaouona unafaa.

Akaja na lisemalo: "UWT Simama na Serikali kwa Maendeleo ya Taifa." Akimaanisha watu wasimame na taasisi wasisimame na mtu, kwani mtu ni mtu na taasisi ni watu, hivyo kwa kushikamana, bila shaka maendeleo yatapatikana. Kwa kiongozi mpenda kuvimba kichwa, hapa angefurahi na kupiga makofi, kwamba bila yeye hakuna nchi na bila yeye hakuna serikali, lakini hilo si kwa Dk. Samia. Alinikumbusha mbali kidogo.

Mnamo Julai 3, 2018, Dk. Magufuli akaalika viongozi wastaafu Ikulu ya Magogoni kuwaomba ushauri. Alialika marais wastaafu, mawaziri wakuu wastaafu, majaji wakuu wastaafu na wastaafu wengine muhimu ili kummulikia mbele aendako.

Kumbe mstaafu Benjamin Mkapa alikuwa ameliona kama alilolitoa Dk, Samia juzi kati hapa, Mkapa alisema: "Ningelipenda kusikia serikali yetu ikijitambulisha kama serikali ya CCM." Hasa walipokuwa wanatambulisha mawaziri, tukisikia serikali ya Magufuli.

Mkapa alifikia kusema hayo, kwa sababu huko nyuma hatukuwahi kusikia serikali ya Nyerere, serikali ya Mwinyi, serikali ya Mkapa, serikali ya Kikwete, bali serikali ya chama inayoongozwa na fulani, lakini lilikuja kuibuka katika utawala wa Awamu ya Tano, ya Dk. Magufuli.

Ni bahati mbaya sana, kwamba hata leo utasikia viongozi wanapojitambulisha hasa mbele ya Rais Samia, wakitoa mlolongo wa maneno: Serikali ya Awamu ya Sita ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Rais Samia Suluhu Hassan.

Mpaka anamaliza kuitambulisha mtu ameshachoka. Hivi kuna haja gani ya mlolongo huo kama si kujikomba au kama si uchawa kama wasemavyo mtaani? Kwani ukisema serikali ya Tanzania utakuwa umepunguza nini?

Tunajua fika kuwa, serikali ni moja, kwamba kama unazungumzia Tanzania ni moja na kama unazungumzia Zanzibar ambako kuna Serikali ya Mapinduzi, pia ni moja, haina haja ya kuzozomoka na sijui ni serikali ya awamu ya ngapi na nini na nini!

Tunafika mbali, kufikia kusema Rais Samia ametoa fedha za kujenga shule au zahanati au barabara au miundombinu fulani, kana kwamba fedha hizo zinatoka mfukoni mwake na si hazina ambayo ni serikali.

Kwani tukisema tu 'serikali imetoa kiasi fulani cha fedha', tutakuwa tumemnyang'anya Dk. Samia uongozi wake? La hasha, ni mpaka 2025 bado serikali hii itakuwa chini ya Dk Samia na akipenda kuendelea na wananchi wakapenda aendelee, ataendelea tu.

Naamini hapendi tu kusema, mengine anayaacha na kutenda atendavyo, akijua hayana athari hasi kwake na kwa nchi, lakini tujue tu kuwa kizuri chajiuza na kibaya chajitembeza. Dk. Samia anajiuza kwa asemayo na atendayo, akijua Watanzania wanamtazama kwa matumaini makubwa. Alamsiki!

UCHUMI

# Saruji Tanga wataja siri ya kung'ara tuzo viwanda, Dk. Mpango anena...

**Na Beatrice Moses**

UZALISHAJI wa bidhaa kwa kuzingatia ubora ni miongoni mwa mambo ambayo yanahamasishwa na viongozi wa serikali kwa sekta mbalimbali nchini, hatua hiyo ikitajwa kulenga pia kujenga ushindani mzuri kwenye soko la ndani na nje ya nchi.

Msemo wa wahenga 'chanda chema huvikwa pete' unadhihirika kwa kampuni kadhaa zilizozingatia wito wa kuzalisha bidhaa bora, kujikuta wakiibuka kuwa washindi, hali ambayo licha ya kuwapa furaha inawajengea kuaminika zaidi kwenye soko la bidhaa husika.

Kampuni ya Saruji Tanga au Tanga Cement PLC, inayozalisha saruji Chapa Simba, mshindi wa jumla wa 'Wazalishaji Bora wa Mwaka 2021' wa bidhaa za ujenzi katika Tuzo za 16 za Rais za Wazalishaji Bora wa Viwanda (PMAYA).

Katika hafla iliyoandaliwa na Shirikisho la Viwanda Tanzania (CTI) jijini Dar es Salaam, alikuwa Makamu wa Rais Dk. Phillip Mpango, aliyekabidhi tuzo kwa washindi wa Tuzo hiyo ya Rais ya PMAYA, anasisitiza umuhimu wa viwanda vya ndani kuongeza thamani ya bidhaa ghafi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Tanga Saruji tanga, , Reinhardt Swart, anazungumzia kutwaa mfululizo tuzo mbili za PMAYA zinazoandaliwa na CTI , anasema:

"Tunayo furaha kubwa kupokea Tuzo za Rais za Wazalishaji Bora wa Mwaka (PMAYA) kwa mara ya tano kutoka kwa CTI. Sababu inayotufanya tujivunie ni kwamba, PMAYA ilitutambua kuwa ni wazalishaji bora wa mwaka kwenye sekta ya viwanda."

Anaeleza kutambulika kuwa wazalishaji bora, kunatokana na utendaji kazi bora kwenye eneo la kampuni, hatua inayowadhihirisha kuwa na maadili bora ya biashara, akinena "hivyo basi, tunaishukuru CTI kwa kututambua sisi kuwa bora zaidi ya washindani wetu kibiashara"

Swart anaitaja saruji kuwa moja ya sekta zinazoongoza kwa kukuza viwanda nchini, akirejea kulikuwapo mapungufu mengi hapo nyuma, lakini wakati huo umepita na sasa biashara hiyo ndani ya dunia ya tatu inahitaji kiwango kikubwa cha uwekezaji, ili kuruhusu biashara kukuwa.

"Masoko ya dunia ya kwanza huwa na kiwango cha chini cha uhitaji wa uwekezaji mkubwa, lakini Tanzania bado inahitaji wawekezaji wengi ili kuendeleza mtaji mkubwa katika biashara kama hii," anasema.

Anabainisha kuwa wanaona kwamba, suala la makaa ya mawe kama nishati mbadala kwa viwanda vya saruji, mrabaha unahitajika kulipiwa, pia Tanzania inapaswa kulipiwa mrabaha kwenye usafirishaji wake.

"Kwa hiyo, kiwanda ambacho kipo mbali zaidi na chanzo cha malighafi kinalipa zaidi ya kiwanda ambacho kiko karibu na malighafi, kitu ambacho kinaleta ushindani usio wa haki na hivyo kuviadhibu viwanda vingine na maeneo mengine ya usambazaji wa bidhaa zetu, ambazo zimelenga kuleta ushindani wa kweli," anasema.

Meneja Masoko na Mawasiliano, Mtanga Noor, anasema kuwa "kwa nyakati zote PLC imekuwa ikijiamini na kuzalisha bidhaa zilizo bora na unaposhindana unapata kitu kilicho bora zaidi."

Anaeleza siri ya ushindi wao nikuzigatia ubora wa saruji wanaozalisha, kutoka sehemu wanakochukua malighafi na kufuatilia mchakato mzima wa uzalishaji kila hatua, bidhaa yao inapotoka getini kwenda kwa mtumiaji.

Pia, anasema.kiwanda cha saruji Tanga, kina wawakilishi kwenye masoko yote ambao hufuatilia mwenendo wa bidhaa zao na baadaye kurudisha mrejesho.

"Hivyo basi ushiriki wetu kwenye tuzo hizi una maana kubwa sana kwetu kwa kuwa tumeona umuhimu wa mashindano haya, ambayo yanasisitiza ubora wa bidhaa ambazo zinakwenda kwa wateja wetu na watanzania kwa ujumla wake kwa kuwa bidhaa bora zikienda kwa wananchi, maisha yao yanakuwa bora," Mtanga anasema.



Makamu wa Rais Dk. Phillip Mpango, akimkabidhi Mkurugenzi Mtendaji wa Tanga Cement PLC, Reinhardt Swart, tuzo ya mzalishaji wa kwanza kwenye hafla hiyo iliyofanyika hivi karibuni, Dar es Salaam. **PICHA: BEATRICE MOSES**

### MAKAMU WA RAIS

Dk. Mpango, akizungumza baada ya kukabidhi tuzo anaipongeza CTI kwa kuandaa tuzo hizo, akibainisha kuwa serikali inaeendelea kuongeza na kuimarisha miundombinu, ikiwamo ya usafirishaji kuhakikisha maeneo yote nchini yanafikika kwa urahisi.

Anaaema, serikali nayo imeendelea na ujenzi wa miradi ya umeme, kuhakikisha nishati hiyo inapatikanai kwa uhakika, huku ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) nao ukinaendelea kwa kasi, ili iweze kuongeza ufanisi katika usafirishaji mizigo kutoka sehemu moja hadi nyingine.

"Tunadhamiria pia kuiunganisha reli yetu na nchi jirani kama vile; Congo DRC na Burundi ili kuchochea biashara ya kikanda na kuwesha taifa kunufaika na huduma (logostics) na usafirishaji wa madini na bidhaa mbalimbali kutoka katika nchi hizo," anasema Dk. Mpango

Pia, Dk. Mpango anasema kuwa Serikali inaendelea na jitihada za kuongeza ufanisi wa Bandari Kuu za Dar es Salaam, Mtwara, Tanga sambamba na bandari katika maziwa makuu na kuimarisha mfumo wa forodha kwa ajili ya upitishaji na utoaji mizigo kwa haraka.

Mbali na hilo anatamka serikali inaendelea na ujenzi wa bandari kavu nchini, ikiwa ni pamoja na kupunguza msongamano wa kontena na magari kutoka bandari ya Dar es Salaam.

Anatumia nafasi hiyo, kuhimiza wenye viwanda wote hapa nchini wafanye jitihada na kuongeza uwezo wa uzalishaji katika viwanda vyao, ili kukidhi mahitaji ya ndani na hivyo kupunguza upotevu huu wa maliasili hii ya fedha za kigeni.

Washindi wengine kwenye tuzo hizo, ni Kilimanjaro Cables, wakati nafasi ya tatu ilichukuliwa na kampuni ya Ando Roofing .



Kikao cha Shirikisho la Viwanda Tanzania (CTI) kilichotoa tuzo. **PICHA: MAKTABA.**

# Majaliwa ataka mawakala pembejeo wa kutosha

Na Mwandishi Wetu

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa amewataka wakuu wa mikoa kote nchini wahakikishe kunakuwa na idadi ya kutosha ya mawakala wa pembejeo za kilimo katika maeneo yao ili kufikisha kwa ufanisi mbolea kwa wakulima.

Alisema hayo juzi alipozungumza na wakazi wa kata ya Majimoto, wilaya ya Mlele mkoani Katavi ambako alikuwa katika ziara ya kikazi. Aliwataka viongozi hao wawasimamie mawakala hao watekeleze kazi hiyo ipasavyo.

Majaliwa pia alisema serikali imetoa Sh. bilioni 150 kama ruzuku ya ununuzi wa mbolea, hivyo kazi hiyo inatakiwa kufanywa kwa ufanisi katika mikoa yote nchini.

"Nataka niwaambie mawakala kwamba fedha ya ruzuku kutoka serikalini kwa ajili ya malipo yenu ipo. Pelekeni pembejeo kwa wakulima, muhimu mfanye biashara kwa weledi na uaminifu mkubwa," alisisitiza.

Waziri Mkuu aliongeza kuwa mkoa wa Katavi ambao una mawakala 10 wa kuuza pembejeo kwa wakulima, umetengewa tani 4,956 za mbolea na kati ya hizo, tayari tani 3,977 zimeshafikishwa mkoani humo.

Kadhalika, Majaliwa aliwataka wakulima kuendelea kujihusisha na shughuli za kilimo hasa katika kipindi hiki ambacho mvua zinaendelea kunyesha kwa kuwa mbolea ipo na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan amesisitiza mkoa wa Katavi upate mbolea ya kutosha. Wakati huo huo, Waziri Mkuu alitoa muda wa wiki mbili kwa Mkuu wa Wilaya ya Mlele, Filbelto Sanga, na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpimbwe, Catherine Mashalla, wahakikishe kituo kipya cha Afya cha Majimoto kinaanza kutoa huduma.

Majaliwa alisema kwa kuwa majengo mengi yameshakamilika likiwamo la kutolea huduma za wagonjwa wa nje, viongozi wa halmashauri hiyo wanatakiwa waanze kupeleka vifaa na ifikapo Desemba 27, kituo hicho kianze kutoa huduma kwa wananchi.

Ujenzi wa Kituo cha Afya Majimoto ni utekelezaji wa sera ya serikali ya kuwa na kituo cha afya kwa kila kata ili kusogeza huduma karibu na makazi ya wananchi. Kituo hicho kilianza kujengwa Januari, mwaka jana na kinatarajiwa kukamilika Februari, mwakani kwa gharama ya Sh. milioni 423.8.



Meneja wa Benki ya Exim Tanzania tawi la Mwanza, Edwin Polle (kushoto) akikabidhi sehemu ya msaada wa majaketi yenye viakisi mwanga (Reflector Jacket) kwa mmoja wa viongozi wa madereva wa pikipiki maarufu kama bodaboda wa mkoani humo, Ally Abdulmajid ikiwa ni sehemu ya jitihada za benki hiyo katika kukabiliana na ajali za barabarani mwishoni mwa mwaka. Katikati ni Mrakibu Msaidizi wa Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani mkoa wa Mwanza, ASP. Sunday Ibrahim. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waliovamia msitu na kujenga nyumba watakiwa kuondoka

Na Mwandishi Wetu

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja, ameagiza wananchi waliovamia msitu wa kuni na kuanzisha shughuli za ujenzi wa nyumba, kuacha mara moja na kuondoka katika eneo hilo la hifadhi.

Masanja aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na wananchi katika wilaya ya Mvomero mkoani Morogoro.

"Sasa tunachowaomba kwanza kusimamisha ujenzi kwenye eneo la msitu. Pili tutaangalia wale ambao wamejimilikisha maeneo makubwa lazima tuyagawe kwa sababu wote ni wavamizi," alisema.

Naibu Waziri alisema Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa huruma yake aliruhusu eneo la msitu limegwe hekta 2,000 ambazo zitagawiwa kwa wananchi lakini wananchi wameendelea kulivamia eneo la msitu.

"Mwaka jana tulielekeza wananchi wapangwe kwenye hekta 2,000 na hiyo ni huruma ya Mheshimiwa Rais Samia. Kwanza naomba tumpongeze mama yetu ana huruma kwa sababu ilikuwa mwondolewe lakini akasema hapana hawa ni wananchi wangu wapangwe," alisema Masanja.

Aliweka bayana kuwa wananchi waliomo kwenye hekta 2,000 zilizogawiwa wako kihalali na watapimiwa ardhi na kupewa hati zao lakini waliovamia wanapaswa kuondoka katika eneo hilo.

Katika hatua nyingine , Naibu Waziri Masanja aliwataka wananchi wa kijiji cha Ngombo wilayani Malinyi, kuhifadhi mazingira na kuacha tabia ya kukata miti ovyo kwa faida ya kizazi cha sasa na cha baadaye.

# Chanzo kushindwa kufundisha KKK chatajwa

Na Devota Mwachang'a

TATIZO la wanafunzi wa shule za msingi kushindwa Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) limeelezwa linasababishwa na kufundishwa na walimu wasio na uzoefu sambamba na uhaba wa walimu 'wazee' wenye uzoefu na maadili katika kufundisha watoto wa darasa la kwanza.

Hayo yamebainishwa katika tathmini ya mwaka mmoja wa utekelezwaji wa Mradi wa Shule Bora (2021-2027) iliyofanyika baada ya utafiti uliofanywa na Cambridge Education Tanzania kwa kushirikiana na viongozi wa elimu wa halmashauri za mkoa wa Tanga.

Mradi wa Shule Bora ni zao la ufadhili wa serikali ya Uingereza kupitia mfuko wa UK Aid kwa serikali ya Tanzania uliogharimu Paundi za Kiingereza milioni 89 sawa na Sh. bilioni 271. Mradi huo utatekelezwa kwa miaka saba kuanzia mwaka katika mikoa tisa ya Tanzania kwa kupokea utaalamu wa kiufundi toka Cambridge Education Tanzania kwa kushirikiana na ADD International, International Rescue Committee na Plan International.

Tathmini hiyo imetolewa na Mratibu wa Mradi toka Cambridge Education Tanzania, Thomas Aikaruwa, katika mafunzo ya uelewa wa mradi yalitolewa kwa waandishi wa habari wa mkoa wa Tanga, maofisa kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (MoEST) na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) yaliyofanyika Korogwe hivi karibuni.

Alisema walimu vijana wengi wakitoka vyuoni, hawataki kufundisha watoto wa darasa la kwanza kwa kuepuka ugumu na usumbufu wa kufundishia KKK, lakini wanalazimika kutimiza majukumu bila kuwa na wito wengi wao wanachagua kufundisha madarasa ya juu kwa masomo ya sayansi, lugha, historia, jiografia na mengine.

"Ni kazi ngumu kufundisha Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) kwa watoto wanaoanza shule. Hii ni kazi inayofaa kufanywa na walimu wenye uzoefu ambao ni wazee. Mpango wetu ni kuwatafuta walimu wenye uzoefu wazee na wenye sifa angalau wawili toka kila halmashauri na kuwakutanisha na walimu vijana wenye wito wa kufundisha wanafunzi wanaoanza darasa la kwanza wawapatie walimu hao vijana mbinu sahihi za kuwafundisha watoto hadi waelewe kwa urahisi," alisema. Aikaruwa aliongeza kuwa kutakuwa na mafunzo ya kuwajengea uwezo waalimu watakaofundisha watoto wenye mahitaji maalum. Mradi huo umeweka nguvu zaidi kuhakikisha watoto shuleni waweze kujifunza vizuri wasaidiwe kujifunza.

Meneja Mawasiliano wa Mradi wa Shule Bora toka Cambridge Education Tanzania, Raymond Kanyambo, alisema mradi umekusudia kuboresha ujifunzaji wa watoto, ufundishaji kwa walimu, elimu jumuishi na usimamiaji wa elimu na mifumo kwa wanafunzi wa shule za msingi.

"Malengo ya mradi ni kuboresha eneo la ufundishaji kwa kutatua changamoto za walimu na kuhakikisha wanafundisha vizuri, kuwapo na mazingira sawa ya kujifunza kwa watoto wenye mahitaji maalumu yatakayowawezesha kupata elimu bora sawa na wengine hatimaye kufaulu vizuri," alisema.

Ofisa Elimu wa Mkoa wa Tanga, Newaho Mkisi, alisema mkoa unatakiwa kukidhi vigezo vya mradi wa wafadhili wa lipwa kwa matokeo yaani Education Program for Results II (EPforR II) ili kupata pesa ikiwamo kuongeza ufaulu kwa darasa la saba, kutatua tatizo la KKK miongoni mwa wanafunzi na kupunguza utoro ili watoto wengi wasome na kuhitimu kwenda shule za sekondari.

"Mkoa wetu haufanyi vizuri kielimu pamoja na kujitahidi, hivyo tunashindwa kupata pesa nyingi kutoka serikalini kwa kushindwa kufikia vigezo vinavyoangaliwa kutokana na ufaulu. Mkoa unapaswa kuongeza ufaulu kwa wanafunzi ili kufikia vigezo vinavyotakiwa vya ufaulu kuweza kupata pesa toka serikali kuu," alisema.

MAKALA MAALUM

# Mradi wa HEET unavyoleta mageuzi katika elimu ya juu

## •Mikoa isiyo na vyuo vikuu kujengewa
## •Sekta binafsi kuwa sehemu ya utekelezaji

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

MRADI wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET) ni miongoni mwa miradi mikubwa ya elimu nchini inayotekelezwa chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamira ya kuleta mapinduzi ya elimu ya juu nchini.

Dhima kuu ya mradi huo ni kuwa na elimu inayoendana na soko la ajira, dola za Marekani milioni 425 sawa na Sh. bilioni 972 zikitolewa kama mkopo na Benki ya Dunia (WB) kwa Serikali ya Tanzania kwa ajili ya mradi huo utakaovinufaisha vyuo vikuu na taasisi na kuleta mageuzi katika utoaji wa elimu ya juu.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, akizungumza kuhusu mradi huo, anasema unatekelezwa kupitia vyuo vikuu 14, Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU), Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) na Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) na taasisi tano za Wizara ya Fedha na Mipango.

Anasema mradi wa HEET unakwenda kupeleka vyuo vikuu katika mikoa ambayo haina vyuo hivyo kwa kujenga kampasi zitakazokuwa zinalelewa na vyuo vikuu kamili ambavyo vinatekeleza mradi huo.

"Kampasi hizi zitajengwa kwenye mikoa ya Mwanza, Kigoma, Lindi, Rukwa, Simiyu, Shinyanga, Tabora, Manyara, Ruvuma, Kagera, Songwe, Katavi, Mara na Singida. Mradi pia utajenga Chuo Kikuu cha Taifa cha TEHAMA, Dodoma.

"Kwenye kujenga hizi kampasi, tutakachofanya ni kuendeleza maono ya Rais wetu, Dk. Samia Suluhu Hassan wakati anahutubia Bunge, alisema 'mjaribu kutoa elimu bora ambayo inakidhi mahitaji kwa maana ya ujuzi na ufundi', hivyo kampasi zitakazojengwa tutaweka utaratibu kuwa hata kama watatoa shahada ziwe ni za ujuzi," anasema.

Anasema ubora na ujuzi ni lazima uzingatiwe katika mradi huo, akiwa na angalizo kuwa udahili utakapoongezeka, usipoteze ubora kwenye vyuo hivyo.

Anasema katika kutambua mchango wa sekta binafsi, serikali itatumia sehemu ya fedha za mradi kufadhili masomo kwa wahadhiri wa vyuo vikuu binafsi na kutoa mafunzo katika fani za afya na tiba ambapo dola za Marekani milioni 1.1 zimetengwa.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Francis Michael, anawashukuru washirika wa maendeleo wanaoshirikiana na serikali kuboresha elimu na kubainisha kuwa mradi wa HEET unatekelezwa kwa miaka mitano kuanzia 2021 hadi 2026.

"Kupitia mradi huu, serikali itatoa ruzuku kwa vyuo vikuu binafsi kwa ajili ya kusomesha wahadhiri katika masuala ya afya na tiba kutokana na mahitaji makubwa ya wataalamu katika sekta hii, lakini pia kama sehemu ya mkakati wa serikali ya kushirikisha vyuo vikuu binafsi katika kuendeleza sekta ya elimu ya juu nchini," anafafanua.

Katibu Mkuu anasema kupitia utekelezaji wa mradi wa HEET, serikali itaboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwenye vyuo vikuu na taasisi nufaika kwa kutekeleza masuala mbalimbali.

**MAENEO LENGWA**

Dk. Michael anayataja maeneo yatakayoguswa na mradi huo yanajumuisha ujenzi na ukarabati wa miundombinu kwa ajili ya matumizi ya kitaaluma na kiutawala ambapo dola za Marekani milioni 329 sawa na Sh. bilioni 753.5 zitatumika kujenga miundombinu mipya na kukarabati iliyopo zikiwamo kumbi za mihadhara na madarasa 130, maabara na karakana 108, mabweni 34, ofisi 23 na miundombinu ya mashamba na vituo atamizi 10.

Pia anasema vitawekwa vifaa vya kisasa vya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kwenye vyuo vikuu na taasisi nufaika za mradi, akibainisha uboreshaji huo utaongeza udahili katika programu za kipaumbele kutoka wanafunzi 40,000 mwaka 2020 hadi kufikia wanafunzi 106,000 mwaka 2026.

Dk. Michael anasema eneo lingine ni uboreshaji wa baadhi ya mitaala na uandaaji wa mitaala mipya ya programu za vipaumbele ili iendane na mahitaji ya soko la ajira kwa sasa.

"Dola za Marekani milioni 7.97 sawa na Sh. bilioni 18.23 zitatumika kuhuisha na kuandaa mitaala mipya zaidi ya 290 kuhakikisha elimu inayotolewa inaendana na kujibu mahitaji ya soko la ajira ndani na nje ya nchi," anasema.

Dk. Michael pia anasema serikali itatumia dola za Marekani milioni 7.79 sawa na Sh. bilioni 17.93 kuboresha mazingira ya kubuni, kuunda teknolojia na kuziendeleza ili kutatua changamoto za kijamii na kiuchumi.

**NEEMA WAHADHIRI**

Katibu Mkuu huyo anasema mradi huo utasomesha wanataaluma kuanzia ngazi ya shahada ya umahiri hadi uzamivu na kutoa mafunzo kazini kwa watumishi.

"Mradi huu unalenga kusomesha takribani wahadhiri 1,100 wakiwamo 623 katika shahada ya uzamivu na wahadhiri 477 katika shahada za umahiri. Wahadhiri na watumishi wengine kwenye vyuo vikuu, wizara na taasisi nyingine watakuwa wanufaika wa mradi kwa kupata mafunzo ya muda mfupi na viwandani ndani na nje ya nchi," anasema.

MAENEO YA KIPAUMBELE

Mratibu wa mradi huo, Dk. Kennedy Hosea anasema mradi wa HEET unalenga kuboresha mazingira ya kufundishia na mitaala ili kuendana na mahitaji ya soko la ajira.

Anabainisha kuwa mradi una vipaumbele 14 ambavyo ni uhandisi na teknolojia, TEHAMA, sayansi, sayansi ya afya na tiba, mipango miji, mazingira na teknolojia, nishati jadidifu, rasilimali maji, mabadiliko ya tabianchi, kilimo na biashara, hifadhi ya wanyamapori, utalii na ukarimu, taaluma ya viwanda na ualimu.

**MZUMBE**

Miongoni mwa vyuo vinavyonufaika na mradi huo ni Chuo Kikuu cha Mzumbe (MU) ambacho kimetengewa dola milioni 21 za Marekani kwa ajili kuboresha mazingira ya kufundisha na kuanzisha programu za vyuo vikuu zinazoendana na mahitaji ya soko la ajira.

Kaimu Mkuu wa Chuo Kikuu hicho, Prof. William Mwegoha anasema miradi inayotekelezwa na chuo chao kupitia mradi wa HEET ni ujenzi wa miundombinu ya kufundishia ambayo inachukua asilimia 79.2 ya fedha zote za mradi.


Anaitaja miradi hiyo ni kupitia mitaala na kutengeneza mitaala mipya ili iendane na soko la ajira, kuboresha TEHAMA na miundombinu yake, kuboresha uhusiano wa chuo na wadau wa nje, kuwajengea uwezo wafanyakazi wa chuo pamoja na kuanzisha kampasi mpya katika Mkoa wa Tanga.

## CHEMSHABONGO NA -00 32 00-

Na Felix Magezi
felixmagezi@gmail.com

Dondoo: Kulia
1. tendeka jambo kwa namna nzuri
5. kata, lokesheni
8. tokeza juu ya maji
9. kinyume cha faradhi
10. jambo linalokusudiwa kufanywa
11. sehemu mojawapo ya taasisi
13. madhubuti 18. thabiti
19. mkonge
22. viumbe wote
24. Wanasheria


Chini:
1. bakaya
2. sujudia
3. kasirika
4. kilevi
6. reli inayounganisha Tanzania na Zambia 7. huenda, pengine
12. sadikika 14. sadiki
15. shauku ya jambo
16. ukavu wa nchi
17. walii, sufii
20. walau
21. pengine 23. Uo



Kamilisha jedwali kwa kujaza maneno yafuatayo:

SAFARI
SOMALIA
MAMBA
FUMBO
LAOSI
BASATA
AMBATANA
ATIFALI
ANITA
AFIKI, IDI,
AMA, MEI, NNE
NDALA
MAKADIRIO

maoni SMS: 0755429240



Majibu toleo lililopita







# Profesa Mosha: Asilimia 75 ya makazi nchini ni holela

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

ASILIMIA 75 ya makazi yote nchini ni holela hali ambayo inasababisha matatizo mbalimbali kwenye jamii ikiwamo kukosekana kwa huduma za kijamii.

Mhadhiri Mwandamizi wa Chuo Kikuu Ardhi cha jijini Dar es Salaam, Prof. Livin Mosha, aliyasema hayo juzi jijini Mbeya wakati wa Mhadhara wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Mbeya (MUST) na kushirikisha wanazuoni mbalimbali wa chuo hicho.

Mhadhara huo ulifanyika ikiwa ni mwendelezo wa matukio mbalimbali kuelekeza mahafari ya 10 ya chuo hicho ambayo yanatarajiwa kufanyika leo.

Prof. Mosha ambaye ni msanifu majengo alisema maeneo mengi nchini wananchi wanajenga makazi holela kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo umaskini hali ambayo inasababisha kukosekana kwa huduma muhimu.

Alisema baadhi ya huduma ambazo hazipatikani kutokana na makazi holela ni maji, umeme, maeneo ya kupumzikia na miundombinu ya barabara kwa ajili ya usafirishaji.

"Lakini makazi holela yanasababisha ongezeko la matukio ya uhalifu kwenye jamii ikiwamo uporaji, mauaji, unyanyasaji wa kijinsia na matukio mengine ya uhalifu ambayo yanakwamisha ustawi wa jamii yetu," alisema Prof. Mosha.

Alisema serikali imekuwa ikitumia mbinu mbalimbali za kupunguza makazi holela ikiwamo urasimishaji wa makazi holela, upimaji wa viwanja na utoaji wa vibali kwa ajili ya ujenzi kwa wananchi na upangaji wa makazi.

Vilevile alisema Tanzania ni mojawapo ya mataifa ambayo yanakabiliwa na tatizo la watu kukosa makazi kwa maelezo kuwa zaidi ya watu 5,000 hawana makazi hivyo hulazimika kulala maeneo ambayo usalama wake ni mdogo.

Makamu Mkuu wa Chuo cha MUST Taaluma, Prof. Goglivin Mtui, alisema mhadhara huo ulikuwa muhimu kwa wanafunzi na wafanyakazi wa chuo hicho hasa kitaaluma.

Alisema chuo hicho ni miongoni mwa taasisi nchini ambazo zinazalisha wataalamu wengi wa majengo wakiwamo wataalamu wa kupanga miji, wahandisi majengo na wasanifu majengo.

Alisema kutokana na taaluma hizo mhadhara uliotolewa na Prof. Mosha ulikuwa muhimu na ulikuwa unawakumbusha wataalamu hao misingi mbalimbali na wajibu wao kwenye jamii.

Baadhi ya wadau walioshiriki mhadhara huo waliupongeza uongozi wa chuo hicho kwa kuandaa mhadhara huo ambao ulikuwa unafanyika kwa mara ya nne tangu walipoanza kuufanya chouni hapo.

Mmoja wa wadau hao, Leah Silvester ambaye ni mhadhiri wa chuo hicho alisema ili kupunguza makazi holela nchini, serikali inatakiwa kuweka mikakati maalumu ya kuimarisha makazi ya watu.




Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera (wa pili kushoto) na Balozi wa Uholanzi nchini, Wiebe De Boer (wa pili kulia), wakishirikiana kuzindua katalogi ya mbegu za viazi wakati wa kongamano la wadau wa kilimo cha viazi mviringo lililoandaliwa kwa ushirikiano kati ya Tanzania na Uholanzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Serikali, wadau kuunda jukwaa la kilimo cha viazi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI mkoani Mbeya imesema inakusudia kushirikiana na wadau mbalimbali wa kilimo kuunda jukwaa la wadau wa kilimo cha viazi mviringo ili kuongeza uzalishaji wa zao hilo pamoja na kushughulikia matatizo mbalimbali ya zao hilo.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera aliyasema hayo jana wakati wa kongamano la wadau wa kilimo cha vianzi mviringo lililoandaliwa kwa ushirikiano kati ya Tanzania na Uholanzi ambayo ndiyo inaongoza duniani kwa uzalishaji wa zao hilo.

Homera alisema jukwaa hilo litatumika kutatua kero mbalimbali zinazohusu zao hilo ikiwamo upatikanaji wa pembejeo za kilimo, masoko ya zao hilo pamoja na matatizo ya vipimo.

Alisema moja kati ya matatizo ambayo yanasumbua kwenye kilimo cha viazi ni matumizi ya vipimo visivyokuwa rasmi kwenye zao hilo hasa ujazo uliozidi maarufu kwa jina la lumbesa.

"Kupitia jukwaa hilo tutakuwa tunajadiliana mambo mbalimbali kuhusu uboreshaji wa kilimo cha zao hili, tunatarajia kulianzisha hivi karibuni na tunatamani liwe la nchi nzima," alisema Homera.

Alisema Mkoa wa Mbeya hasa katika Wilaya za Mbeya na Rungwe ni miongoni mwa maeneo ambayo yanazalisha viazi kwa wingi kutokana na hali ya hewa kuwa nzuri na inayovutia uzalishaji wa zao hilo.

Balozi wa Uholanzi nchini, Wiebe De Boer, alisema Uholanzi imeingia makubaliano na Tanzania kwa ajili ya kuboresha uzalishaji wa viazi mviringo.

Alisema watakuwa wanasaidia kwenye uzalishaji wa mbegu bora za viazi pamoja na mbinu za kilimo bora cha viazi mviringo ili kuongeza uzalishaji kwa kuzingatia ubora.

Mkurugenzi wa Ukanda wa Kilimo wa Kusini mwa Tanzania (SAGCOT), Geoffrey Kirenga, alisema kwa sasa Tanzania inazalisha nusu ya uwezo wake wa kuzalisha viazi mviringo kutokana na kukosekana kwa mbinu za kisasa za uzalishaji.

Alisema wakulima wengi wanatumia mbegu za kienyeji ambazo tija yake kwenye uzalishaji ni ndogo na hivyo akasisitiza kwamba ushirikiano na Uholanzi utasaidia kuongeza uzalishaji wa zao hilo.

Alisema zao hilo ni la tatu kwa uzalishaji nchini baada ya mahindi na mpunga na hivyo akaeleza kwamba ushirikiano walioingia na Uholanzi utasaidia kuongeza uzalishaji na kulifanya kuwa miongoni mwa mazao yanayoliingizia taifa fedha nyingi za kigeni.

# RC aiagiza Hospitali ya Rufani kufunga CT-Scan

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera ameiagiza Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mbeya, kufunga vifaa vya mashine ya mionzi ya CT- Scan ambavyo tayari serikali imevinunua ili wagonjwa waanze kupata huduma za uchunguzi wa kitabibu.

Alitoa agizo hilo jana alipofanya ziara ya kukagua miradi ya ujenzi inayotekelezwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mbeya.

Alisema uongozi wa hospitali unatakiwa kufunga mashine hizo kabla ya Januari 15, mwakani ili kuanza kutoa huduma kwa wagonjwa ambao baadhi wanakwenda Hospitali ya Kanda Mbeya kufuata huduma hizo na kusababisha msongamano mkubwa wa wagonjwa.

Alisema Sh.bilioni tano zilitolewa na serikali kwa ajili ya kukamilisha miradi mbalimbali hospitalini hapo ikiwamo jengo la upasuaji, wagonjwa wa dharura, ukarabati wa jengo la wagonjwa wanaohitaji uangalizi maalum (ICU).

Miradi mingine inayotekelezwa hospitalini hapo ni ujenzi wa vyumba vya radiolojia na nyumba ya mtumishi.

Alisema kukamilika kwa ujenzi wa miradi hiyo kutaongeza idadi ya vitanda vya wagonjwa watakaofanyiwa upasuaji kufikia 89 na wagonjwa sita watafanyiwa upasuaji kwa wakati mmoja.

Alidai kuwa kukamilika kwa jengo la upasuaji kutasaidia kuboresha huduma za matibabu ya wagonjwa wanaohitaji uangalizi maalum kwa wananchi wanaotoka maeneo ya Mkoa wa Mbeya na mikoa jirani kupata huduma bora na kwa wakati.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mbeya, Dk. Abdalah Mmbaga aliiomba serikali kuwaongezea Sh. milioni 200 kwa ajili ya kukamilisha miundombinu na baadhi ya vifaa ambavyo vitafungwa kwenye wodi.

Alisema tayari majengo yote yamekamilika kwa asilimia kubwa na muda wowote kuanzia sasa majengo hayo yataanza kutoa huduma lakini kikwazo ni baadhi ya kukosa vifaa.

Alibainisha vikwazo vingine kuwa ni kukosekana kwa mfumo wa kuzima moto na mfumo wa viyoyozi kwani havikuwapo kwenye mkataba uliotekelezwa.



## HABARI DODOMA

# TGNP yataja maficho ya ukatili

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

OFISA programu mwandamizi wa Mtandao wa Kijinsia Tanzania (TGNP) ameitaka jamii kuachana na mitazamo hasi anayoitaja kuchochea vitendo vya ukatili wa kijinsia ikiwamo ulawiti, ubakaji na mauaji ya wenza.

Zainab Mmary alibainisha hayo jana jijini hapo wakati wa kikao kazi cha watendaji wa serikali kuu, akisisitiza kuwa vitendo hivyo vinazidi kushika kasi nchini.

Alisema jamii inapaswa kubadili mitazamo iliyoko ili kusaidia kukabiliana na vitendo vya ukatili ambavyo vimekuwa vikiongezeka kila siku.

"Bado matukio ya ukatili nchini yanaongezeka kila siku lakini kwa kiasi fulani tunapiga hatua. Moja ya changamoto zilizoko ni jamii zetu kutobadili mitizamo kwani hata mfumo dume bado ni sababu ya watoto wetu kulawitiwa kwani mwanamume anachokitaka ni lazima akipate kwa gharama yoyote ile," alifafanua.

Alisema pamoja na matatizo yaliyoko, anafurahia kuona walau sasa jamii imeanza kubadilika kwa kujitokeza kutoa taarifa za vitendo hivyo vya ukatili.

"Zamani ilikuwa vigumu sana matukio haya ya ukatili kuzungumzwa wazi katika jamii, binti kubakwa ilikuwa ni vigumu sana kusema au mtoto kulawitiwa," alisema.

Aliishauri serikali kuendelea kutoa elimu kwa jamii ili kubadili tabia ikiwa ni pamoja na kuwezesha wananchi kiuchumi kwa kuwa watu kukaa bila kazi ya kufanya ni moja ya sababu ya kuongezeka kwa matukio hayo.

"Harakati tunazozifanya zimetiliwa mkazo sana lakini bado kuna ombwe kubwa la rasilimali fedha, hata tatizo likitokea sehemu fulani watu wanakosa uwezo wa kufika kwa wakati," alisema.

Mkurugenzi wa Sera na Mipango Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Makundi Maalum, Simon Magesa, alisema licha ya kuwapo sheria kali, bado vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto vinaendelea. "Kuna sheria ambayo inasema kuwa kama mtu akimbaka (akimnajisi) mtoto chini ya miaka 10, anafungwa maisha lakini akimbaka mtoto wa zaidi ya miaka 10 ni kifungo cha miaka 30 lakini bado watu wanafanya matukio haya.

"Sasa inabidi tuangalie na tatizo la afya ya akili katika jamii zetu ili kuchukua hatua na kumaliza tatizo hili kwani ni jambo la kushangaza mzazi kumlawiti mtoto wa kumzaa mwenyewe," alisema Magesa.



Wanafunzi wa Shule ya Msingi Mbande wilayani Kongwa wakibeba maji kwa toroli linalokokotwa na ng'ombe kwa ajili ya matumizi ya shuleni hivi karibuni. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Waziri ahimiza utunzaji wa mazingira, vyanzo vya maji

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera Bunge na Uratibu, George Simbachawene, amehimiza wananchi kuendelea kutunza mazingira na kuhifadhi vyanzo vya maji.

Simbachawene aliagiza hayo juzi wakati wa ziara yake ya kusikiliza na kutatua kero za wananchi wa Kijiji cha Mkoleko, Jimbo la Kibakwe, Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa.

"Tuanzishe mradi wetu wa maji kupitia vyanzo vya maji tulivyonavyo kwenye mlima ili tupate maji ya uhakika kwa ajili ya shughuli za kijamii," alisema.

Simbachawene aliwataka watendaji wa kata kuendelea kutoa elimu ya uhifadhi wa mazingira kwa wananchi na kutunga sheria ndogo ili kuzuia ukataji wa miti ovyo kwenye kingo za makorongo ili kuzuia mmomonyoko wa ardhi.

"Kama una miti pembezoni mwa shamba lako iache usiikate ili iendelee kuzuia mmomonyoko wa ardhi na kuharibu miundombinu ya barabara," alisema.

Waziri Simbachawene pia aliahidi kuendelea kuimarisha barabara zinazounganisha vijiji vyote vinavyounganisha Kata ya Mansa kwa kuhakikisha zinafanyiwa ukarabati katika maeneo yote korofi.

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mpwapwa, Richard Maponda, alimshukuru Waziri Simbachawene kwa jitihada zake za kuleta maendeleo kwenye wilaya hiyo kutokana na zahanati sita kufunguliwa na wagonjwa wanapata dawa.

"Kuna shule zimepata usajili ambazo zitasaidia kutatua adha ya wanafunzi kutembea umbali mrefu kwenda shuleni," alisema.

Emmanuel Nzoka, mkazi wa jimbo hilo, aliishukuru serikali kupitia kwa mbunge huyo kwa kutengeneza barabara na kuwa kwenye hali nzuri katika majira yote ya mwaka.

"Tulikuwa kisiwani kutokana na barabara kuharibika kutokana na maji ya mvua, hivyo kushindwa kupitika katika majira ya masika." alisema.

# Wataka bajeti kuzikabili mimba, ndoa za utotoni

**Na Peter Mkwavila,** CHAMWINO

BARAZA la Watoto Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino mkoani Dodoma limeomba serikali kutenga bajeti kila mwaka kwa ajili ya kuwawezesha kufanya mikutano yao ili kujadiliana mbinu za kukabiliana na ongezeko la vitendo vya ukatili, ulawiti, mimba na ndoa za utotoni pamoja na ukeketaji.

Mwenyekiti wa Baraza hilo, Wema Nollo, aliwasilisha hoja yao hiyo juzi alipozungumza kwenye kilele cha maadhimisho ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia yaliyofanyika wilayani humo.

Alisema watoto wanaiomba serikali kutenga bajeti kwa kila mwaka ili kutatua kero zinazowakabili ikiwamo ukatili uliokithiri dhidi yao.

Nollo alisema ili kutatua kero zinazowakabili watoto, lazima mikakati thabiti iwekwe kuhakikisha wanapata muda wa kukutana kwa pamoja na kujadili kile wanachokipitia shuleni na kwenye maeneo wanayoishi.

"Hivyo, serikali yetu tukufu inayoongozwa na mama yetu mpendwa Rais Samia (Suluhu Hassan) sisi kama watoto wake tunaomba halmashauri itoe bajeti itakayosaidia watoto wa kike na kiume kupata vikao vya mikutano hata kwa awamu mbili mwezi wa sita (Juni) na kumi na mbili (Desema), ili kuzijadili changamoto zetu na kutatua kero hizo," alisema Nollo.

Mwenyekiti huyo pia alisema ni wakati sasa wa dawati la jinsia kuanza kutoa elimu shuleni ambapo kwa asilimia 60 ukatili umekuwa ikitokea majumbani na asilimia 40 hutokea shuleni.

Ofisa Ustawi wa Jamii Wilaya ya Chamwino, Deodatus Damian, alisema bado kuna ugumu miongoni mwa wanajamii katika kutoa taarifa mapema ukatili unapotokea, hali inayosababisha kukosekana kwa ushahidi hasa kwa matukio ya ulawiti na ubakaji.

Damian alisema kwenye wilaya hiyo ya wamepokea visa 600 kwa mwaka vikijumuisha ukatili, vipigo, ulawiti na ubakaji.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Kamishna Msaidizi Mwandamizi, Ulrich Matei, alisema ni jukumu la kila mmoja kwenye familia kuhakikisha anasimamia majukumu yake ipasavyo kuepusha ugomvi na kusimamia misingi ya malezi kwa watoto.





## Waziri ataja sababu kutaka kuvunja ZRB

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango, Dk. Saada Mkuya, amesema kuwapo mamlaka ya kusimamia mapato kwa kiasi kikubwa kutasaidia kukusanya mapato kwa ufanisi na kubuni vyanzo vipya vya kodi.

Waziri huyo aliyasema hayo jana wakati wa kikao cha Baraza la Wawakilishi alipojibu hoja za wajumbe wa baraza hilo waliochangia Muswada wa Sheria ya Kuundwa kwa Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) na kuvunjwa kwa Bodi ya Mapato ya Zanzibar (ZRB).

Alisema kuanzisha chombo kipya cha Mamlaka ya Mapato (ZRA) kutawezesha kuwa taasisi inayojitegemea ikiwa na majukumu ya kukusanya kodi zote za ndani nchini kwa mujibu wa sheria.

Alisema kuundwa kwa mamlaka hiyo kwa kiasi kikubwa kutahamasisha ulipaji kodi kwa hiari kwa kuwahusisha walipajikodi wote na kuimarisha ukusanyaji wa kodi ya mapato.

"Hayo ndiyo malengo ya kuundwa kwa mamlaka ya kodi nchini, ili kuongeza ufanisi, uwajibikaji na ubunifu kwenye vyanzo mbalimbali vya mapato ambapo sheria ya zamani ya Bodi ya Mapato haikuwa na uwezo huo," alisema.

Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi ya Baraza la Wawakilishi, Sabiba Filfil Thani, alisema kuwapo sheria ambayo sasa inaunda ZRA, kwa kiasi kikubwa kutasaidia kuwapo mifumo ambayo itawatambua walipakodi wote nchini kwa kuwa na kazi data maalum.

Alisema hadi sasa hakuna takwimu halisi za walipakodi wakubwa ambapo matokeo yake baadhi ya wafanyabiashara wenye sifa ya kulipa kodi hawalipi.

Aliitaka Wizara ya Fedha kuhakikisha mifumo ya kodi yote inatumika rasmi kwa walipakodi ili kudhibiti mianya ambayo huikosesha serikali mapato yake muhimu kwa ajili ya maendeleo.

"Kamati ya Fedha na Uchumi ya Baraza la Wawakilishi imefurahishwa kuwasilishwa kwa muswada wa sheria ya kuanzishwa kwa Mamlaka ya Kodi Zanzibar.

"Matarajio yetu makubwa chombo hicho kitafanya kazi zake kwa ubunifu mkubwa kuhakikisha mapato ya nchi yanaimarika," alisema.

Baadhi ya wajumbe wa baraza hilo waliochangia muswada wa kuundwa kwa ZRA, waliitaka serikali kufanya ukaguzi wa fedha wa taasisi hiyo ili kuona matumizi yake na ukusanyaji wa kodi kwa ujumla wake.

# Utafiti wabaini tatizo hali ya ripoti za vyombo vya habari

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SHULE Kuu ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano kwa Umma (SJMC) ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) imefanya utafiti kuhusu hali ya ripoti za habari nchini na kubaini kiwango kidogo cha ubora wa habari zinazoripotiwa kwenye vyombo vya habari.

Akizungumza juzi visiwani hapo wakati wa uzinduzi wa ripoti hiyo ya utafiti uliofanywa, Mtafiti Mkuu kutoka SJMC, Abdallah Katunzi alisema habari nyingi zinazoripotiwa kwenye vyombo vya habari siyo za uwajibikaji na badala yake ni za matukio.

Alisema vyombo vya habari vya serikali vinavyoongoza kwa kutoa habari za matukio badala ya kukosoa serikali katika masuala ya uwajibikaji.

Katunzi alisema habari zenye maoni kinzani ni asilimia mbili tu huku habari zinazoikosoa serikali ni asilimia nne na zinazoikosoa asasi za kiraia ni asilimia 0.7 na sekta binafsi asilimia 0.5 na habari zinazosimamia uwajibikaji ni chache.

Alisema utafiti huo umefanya uchambuzi wa kazi za habari 1,887 kwenye magazeti, redio na televisheni na kati ya hizo, asilimia 52 ya habari zinatoka kwenye makundi mawili ambayo ni maendeleo na uchumi.

Mtafiti Mkuu huyo alisema asilimia 60 ya habari zinazopaswa kujibu tuhuma kutoka upande wa pili hazikutoa nafasi hiyo, asilimia 44 ya habari hizo hazina mitazamo kabisa, asilimia 14 ndizo zenye mitazamo zaidi ya miwili.

Alisema utafiti huo umebaini kuwa habari zinazotoa sauti ya wanawake ni asilimia 39, zilizotoka kwenye magazeti ndiyo zilihusisha wanawake huku asilimia 44 kwa redio na televisheni, hivyo kushauri kuongeza jitihada zaidi kusikika kwa sauti za wanawake.

Katunzi alisema kutokana na uchumi duni wa vyombo vya habari, kumesababisha kutoripotiwa kwa habari za uwajibikaji na badala yake kuishia katika matukio.

Mkuu wa Idara ya Mawasiliano ya Umma Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA), Imane Duwe, alisema asilimia kubwa ya vijana wanaokwenda kusomea taaluma hiyo, hawaisomi kwa wito bali hushawishiwa.

Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Kundo Mathew, alisema kazi ya uandishi wa habari imeingiliwa na watu wasio na taaluma.

Alisema kuwa baada ya uzinduzi huo kunahitajika kufanya tafakari kwa pamoja ili kutatua vikwazo vilivyoko na kuja na mkakati wa pamoja.

Alise serikali ipo tayari kushirikiana na wadau kuondoa changamoto hizo.

Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Tabia Maulid Mwita, alisema kwa sasa Serikali ya Zanzibar iko kwenye mchakato maalum kuhakikisha maslahi ya waandishi wa habari yanasimamiwa kama ambavyo zinafanya kada zingine kwa sababu wanafanya kazi kubwa kwenye jamii.

SJMC imefanywa utafiti huo katika vyombo 29 vya habari na kubaini udhaifu wa ubora wa habari zinazotolewa na vyombo husika huku nyingi zikiwa ni habari za matukio.



Kamishna wa Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB), Yusuph Juma Mwenda (wa pili kushoto), akikata keki kuashiria mwezi wa shukurani na furaha kwa walipakodi baada ya kumalizika kwa mkutano na wafanyabiashara katika ukumbi wa Kariakoo, Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Zimbabwe yajifunza Zanzibar mifumo ya kukusanya mapato

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAMLAKA ya Mapato Zimbabwe imefika Zanzibar kujifunza mfumo wa ukusanyaji wa mapato kupitia mtandao wa kielektroniki unaotumiwa na Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB).

Ofisa kutoka Kamishna wa mamlaka hiyo ya Zimbabwe, Misheck Govha, amesema visiwani hapa kuwa mfumo huo unasaidia kwa kiasi kikubwa ukusanyaji wa mapato.

Aliyasema hayo jana wakati wa kikao cha pamoja kilichowashirikisha watendaji wa ZRB na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwenye ofisi za bodi hiyo iliyoko Mazizini.

Alisema ameshangazwa kuona taasisi hiyo imeanzisha mfumo wake wa kushughulikia mauzo na utoaji wa risiti.

Alisema Zimbabwe nayo itaanza ukusanyaji wa mapato kwa mfumo huo na ndiyo lengo la kufika Zanzibar kujifunza kupitia mfumo huo.

Ofisa huyo alisema mkutano huo umewasaidia kubadilishana mawazo na kujifunza mambo mbalimbali ambayo wanaamini yatawasaidia katika kuimarisha mapato ya nchi yao.

Kamishna wa TRA, Swalehe Byarugada, alisema ugeni huo umekuja Tanzania kwa lengo la kujifunza jinsi ilivyofanikiwa katika kuweka mifumo ya ukusanyaji wa mapato hasa kodi za ndani.

Alisema ujumbe huo pia umeona jinsi Tanzania inavyosimamia biashara mbalimbali hasa zile ambazo zinahitaji kutumia mashine za kielektroniki.

Swalehe alisema wana mashine ambazo zinatumika kwenye maduka ya kawaida na zile zinazotumika kwenye vituo vya mafuta na Super Market ambapo Tanzania Bara imeshajiridhisha kwamba mifumo yao ipo salama na inafanya kazi.


"Kwa vile Tanzania ni serikali inayoundwa na nchi mbili za Tanganyika na Zanzibar, pia wamekuja na Zanzibar kuona namna gani tunavyofanya katika kusimamia mapato," alisema.

Kamishna huyo alisema mamlaka hiyo imejiridhisha kuona ZRB ipo mbele katika kuona kwamba kila kodi ya Zanzibar inasimamiwa na inakusanywa kwa kutumia mifumo imara na kuiwezesha serikali kupata mapato yake.

Mkurugenzi Idara ya Makusanyo ZRB, Shaaban Yahya Ramadhan, alisema ujio huo umelenga kuona utendaji kazi wa mifumo ya bodi hiyo ili na wao kuanzisha mifumo kama hiyo na kujadili kwa pamoja changamoto zinazowakabili ili nao wazuia zisijitokeze kwao.

Alisema kuwa mfumo huo umekuwa na mafanikio makubwa katika ukusanyaji wa mapato lakini unakabiliwa na changamoto ikiwamo wafanyabiashara kutotoa risiti za kielektroniki wanapofanya mauzo na wananchi kutokudai risiti wanapofanya ununuzi.

Aliahidi bodi hiyo itaendelea kutoa elimu kwa wafanyabiashara na wananchi juu ya umuhimu wa kutoa risiti za kielektroniki na wananchi kudai risiti ili kuiwezesha serikali kupata mapato yake na kuona mifumo hiyo inafanya kazi kama ilivyokusudiwa.





# Tani 100 za mahindi zatolewa kukabili upungufu wa chakula

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

SERIKALI imetoa tani 100 za chakula ili kukabiliana na upungufu wa chakula katika Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu mkoani Shinyanga.

Chakula hicho kimetolewa baada ya Mbunge wa Ushetu, Emmanuel Cherehani, kuiandikia barua Wizara ya Kilimo kuomba msaada wa chakula baada ya jimbo hilo kutozalisha chakula cha kutosha msimu uliopita kutokana na ukame.

Diwani wa Nyamilangano, Robert Mihayo, alibainisha hayo jana alipozungumza na Nipashe, akisisitiza kuwa hawawezi kuwaongoza wananchi ambao wana njaa.

Alisema kuwa baada ya kuandikwa barua hiyo na kufikishwa ofisi za Wizara ya Kilimo, mnamo Novemba 8, mwaka huu, Waziri wa Kilimo, Husein Bashe, alifanyika kazi ombi hilo na kuwapa chakula (mahindi) tani 10 kutoka Hifadhi ya Taifa ya Chakula (NFRA) na kuuziwa kwa bei nafuu.

Mihayo alisema chakula hicho kinauzwa kwa wananchi wa jimbo wa Sh. 16,600 kwa debe (ndoo yenye ujazo wa lita 20) huku mitaani, hivyo kutatua upungufu wa chakula uliowatikisa.

Alisema msaada huo umewafanya wakulima wengi kuwa na jitihada kubwa katika uzalishaji katika msimu huu kulinganisha na msimu uliopita, huku mahindi hayo yakitumika kuwasaidia wananchi wa wilaya jirani za Uyui na Kaliua mkoani Tabora.

"Tumepokea tani 100 za mahindi na kuuziwa kwa bei nafuu ambayo kila mwananchi ana uwezo wa kuimudu na msimu huu tutazalisha chakula zaidi kulinganisha na msimu wa jana kwa sababu pia tumepokea mbolea ya ruzuku mifuko 620," alisema Mihayo.

Aliwashauri wananchi kuhakikisha mahindi hayo waliyoyapata, yanatumika kama chakula tu na kuacha tamaa ya kuyauza na kupata fedha ambazo watazitumia kwa muda mfupi.

Mihayo alifafanua kuwa ili kupata mbolea ya ruzuku, kila mkulima analazimika kufika eneo inakotolewa akiwa na kitambulisho chake au namba ya usajili aliyopewa wakati wa kusajili wakulima.

Mmoja wa wakazi wa Nyamilangano, Paschal Mabula, alisema kuwa msimu uliopita hawakuzalisha chakula kingi kutokana na ukame, hali iliyosababisha kukabiliwa na uhaba wa chakula.

Elizabeth Masumbuko, mkazi wa Ushetu, alipongeza uamuzi wa serikali wa kutoa mbolea ya ruzuku kwa wakulima, akiamini itaongeza uzalishaji.

Mbunge wa Ushetu, Cherehani, alisema wananchi wanapokuwa na njaa, hawawezi kwenda shambani kuzalisha na serikali imehifadhi chakula cha kutosha ambacho mwisho wa siku inapaswa kuwapa wananchi na kuwauzuia kwa bei ya chini.

Aliwataka wananchi msimu huu wazalishe chakula zaidi kwa kuwa serikali imewapa pembejeo za kutosha kwa muda mwafaka.



Mkurugenzi Mkuu wa RUWASA, Mhandisi Clement Kivegalo (kulia), akisaini mkataba wa upanuzi mradi wa maji Lugeye wa Sh. bilioni 7.1 unaotarajiwa kuhudumia zaidi ya watu 80,000 katika Kata ya Lugeye na kuzalisha lita milioni 3 kwa siku. Katikati ni Mwanasheri wa RUWASA, Gloria Chagewi, pamoja makandarasi kutoka kampuni ya ujenzi ya Monela Construction and co LTD watakaojenga mradi huo. **PICHA: VITUS AUDAX**

## RUWASA yatia saini miradi ya bilioni 8.4/- kuzalisha maji

**Na Vitus Audax,** MWANZA

WAKALA wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) umetia saini mikataba miwili ya ujenzi na upanuzi wa miradi ya maji kwenye kata tatu za Lugeye, Lumeji na Misungwi wilayani Magu mkoani Mwanza yenye thamani ya Sh. bilioni 8.4 inayotarajiwa kuhudumia wananchi zaidi ya 80,000 wa kata hizo na kumaliza tatizo la uhaba wa maji.

Katika mkataba huo uliowahusisha RUWASA na kampuni mbili za ujezi; Mponeja Construction & Co. Ltd iliyotia saini mkataba wa mradi wa Lugeye wenye thamani ya Sh. bilioni 7.1 na Kampuni ya Lugahila Construction iliyotia saini mkataba wa mradi wa Lumeji-Misungwi wenye thamani ya Sh. bilioni 1.44.

Akizungumza jana baada ya utiaji saini wa miradi hiyo itakayozalisha lita za maji milioni tatu kwa siku, Mkurugenzi Mkuu wa RUWASA, Clement Kivegalo, alisema serikali kwa nchi nzima imetia saini miradi yenye thamani ya Sh. bilioni 800 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji vijijini.

"Kwa Mkoa wa Mwanza pekee, tumetia saini mikataba yenye thamani ya Sh. bilioni 125 kwa ajili ya miradi ya maji vijijini 43, mingine tayari imekamilika na inatoa maji ikiwa ni sehemu ya kutatua shida katika upatikanaji wa maji na kumtua mama ndoo kichwani," alisema Kivegalo.

Akitoa taarifa ya mradi huo, Meneja wa RUWASA Mkoa wa Mwanza, Godfery Sanga, alisema mradi huo utakuwa mkubwa wa uzalishaji wa maji kati ya miradi yote mkoani Mwanza, ukitarajiwa kusambaza maji zaidi ya kilometa 45 za maeneo ya vijiji hivyo.

Alisema mradi huo utakuwa na tangi kubwa la lita milioni moja, mara nne zaidi ya matangi mengine ya mkoani hapo, wakitarajiwa kuzalisha lita milioni tatu kwa siku na kuwahudumia zaidi ya wananchi 80,000 katika wilaya hiyo.

"Miradi hii miwili inatarajiwa kukabidhiwa katika kipindi cha muda wa miezi 18 na kukabidhiwa kwa wananchi, mradi mmoja wa upanuzi utagharimu Sh. milioni 7.1 huku mradi wa pili ukigharimu Sh. milioni 1.44 na zote zimekabidhiwa kwa makandarasi wawili walioshinda zabuni hizo," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Adam Malima, serikali itahakikisha inalinda miradi hiyo na kukamilika kwa wakati bila kuhujumiwa na wote watakaojaribu kuihujumu, watachukuliwa hatua bila kujali nyadhifa na hali zao.

Mkuu wa Wilaya ya Magu, Saalum Kali baada ya kushuhudia utiwaji saini wa miradi hiyo, aliwatahadharisha wananchi wilayani humo kutokuhujumu miradi hiyo na kusema kuwa wote watakaokamatwa wakihujumu miradi hiyo watafunguliwa mashtaka ya uhujumu uchumi.

Baadhi ya wananchi kutoka Kata ya lugeye waliiomba serikali kutekeleza miradi hiyo kwa wakati ili kutatua kero ya uhaba wa maji inayowakabili.

"Mimi na uzee wangu bado ninasumbuka kwenda kupanda foleni kwa muda mrefu kupata maji na kutembea umbali mrefu, ninaomba serikali ijitahidi kutekeleza miradi hiyo kwa wakati," alisema Baisimaki Kabula, mkazi wa Lugeye.

## Kusindikiza bibi harusi kwatajwa kichocheo cha ndoa za utotoni

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MILA na desturi zinazofanyika wakati wa ndoa za kimila katika Kijiji cha Ilobashi, Kata ya Masengwa wilayani Shinyanga, zimetajwa kuwa kichocheo cha ongezeko la mimba na ndoa za utotoni.

Imebainishwa kuwa ifikapo msimu wa mavuno, zinafanyika ndoa nyingi za kimila ambazo bibi harusi anapokwenda ukweni lazima asindikizwe na mabinti wenzake 10 wakiwa na wavulana 10 na kunakuwa na utaratibu wa kugawana "kila mmoja na mtu wake" na wakifika huko majira ya usiku wanakwenda kufanya mapenzi.

Mwelimishaji wa Masuala ya Ukatili Ndani ya Jamii Kijiji cha Ilobashi, Mary Lutinya, alibainisha hayo juzi alipozungumza na Nipashe kijijini huko.

"Ndoa hizi za kimila zinapaswa kuangaliwa kwa jicho la tatu kwa sababu ni moja ya chanzo cha mimba na ndoa za utotoni, haiwezekani binti anayeolewa lazima asindikizwe na mabinti wengine 10 wakiwa na wavulana wao, kila mmoja na wa kwake na majira ya usiku wanakwenda kulala pamoja," alisema Mary.

Alifafanua kuwa wakitoka huko kwenye harusi, kila mmoja anarudi nyumbani kwao huku tayari wakiwa wameshajenga uhusiano na kuendelea kufanya mapenzi na mwisho wa siku, binti anashika ujauzito na kuacha masomo na wengine kuolewa.

Kiongozi wa kidini, Mch. Edward Mashala kutoka Kanisa la P.A.G.T Masengwa wilayani Shinyanga, alisema uendekezaji wa mila na desturi ambazo zimeshapitwa na wakati unaendelea kuwa kikwazo katika kukabiliana na vitendo vya ukatili dhidi ya watoto.

Alisema binti akishapevuka, bila ya kujali kama anasoma, wazazi wanaanza kupanga mipango ya kumwozesha na asipoolewa anaonekana kama laana ndani ya familia.

"Na ndiyo maana huwaruhusu kwenda kwenye hizo harusi za kimila ili wakapate mabwana," alisema.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Kata ya Masengwa wilayani Shinyanga, Atupokile Maseta, alisema ndoa hizo za kimila zipo na wao kama viongozi wamekuwa wakilikemea suala hilo na kuwapatia mabinti elimu ya kujitambua na afya ya uzazi kwa kutofanya mapenzi katika umri mdogo.

# CRDB na IFC zakubaliana maeneo sita ya ushirikiano

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya CRDB na Shirika la Kimataifa la Fedha la Benki ya Dunia (IFC) wamekubaliana maeneo sita mahususi ya ushirikiano katika juhudi zao za kukuza ujumuishi wa kifedha Tanzania na ukanda mzima wa Afrika Mashariki.

Makubaliano hayo yamefikiwa na watendaji wakuu wa taasisi hizo mbili wakati wa mkutano wao huko Washington uliofanyika sambamba na Mkutano wa Wakuu wa nchi za Afrika na Marekani.

Kwenye mkutano huo, ujumbe wa Benki ya CRDB uliongozwa na Mwenyekiti wa Bodi, Dk. Ally Laay, Makamu Mwenyekiti, Prof. Neema Mori na Mkurugenzi Mtendaji, Abdulmajid Nsekela, huku IFC ikiwakilishwa na Mkurugenzi anayesimamia ushirikiano na Taasisi za Fedha Duniani, Tomasz Telma.

IFC ni mshirika wa muda mrefu na wa kimkakati wa Benki ya CRDB na imekuwa na jukumu muhimu katika kusaidia mkakati wa benki tangu 2014.

"IFC imekuwa na mchango mkubwa katika mafanikio ya Benki ya CRDB katika kipindi cha miaka minane iliyopita na katika kufanikisha utekelezaji wa mkakati wetu wa miaka mitano ambao unamalizika mwaka huu," alisema Nsekela katika taarifa yake iliyowasilishwa kwa vyombo vya habari jijini.

Alisema mkutano wa Washington ulilenga kuwaleta pamoja viongozi wakuu wa taasisi hizo mbili ili kujadili maeneo ya ushirikiano na uungaji mkono.

"Tumekubaliana kushirikiana katika masuala yanayohusu ufadhili wa shughuli za wanawake na vijana; ufadhili wa miundombinu nchini Tanzania, Burundi na DRC pamoja na kusaidia upanuzi wa huduma za benki yetu kwenye ukanda wa Afrika Mashariki na Kusini," Nsekela alisema.

Taasisi hizo mbili, alisema pia zilikubaliana kushirikiana katika ufadhili wa miradi ya mazingira, kilimo biashara pamoja na kuijengea uwezo Benki ya CRDB katika kubuni na kusimamia miradi ya ufadhili kiuchumi.

Katika maelezo yake wakati wa mkutano huo, Telma alielezea kwa kina uzoefu wa IFC katika kufadhili miradi Tanzania na akabainisha kuwa nchi ina fursa nyingi za kiuchumi, huku akipongeza jitihada zinazofanywa na serikali katika kufungua uchumi.

Alieleza kwa kina uhusiano wa IFC na Benki ya CRDB, akiipongeza benki hiyo kwa utendaji mzuri kulinganisha na taasisi nyingine za kifedha.

Telma alisema kwa kuwa IFC na Benki ya CRDB wamekuwa wakifanya kazi pamoja kwa miaka mingi na ana matumaini kuwa majadiliano hayo yatafungua fursa mpya za ushirikiano zaidi kati ya taasisi hizo mbili.

Katika mada yake katika mkutano huo, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Nsekela alieleza kuwa benki yao ina mizania ya Sh. trilioni 10.9 na mtaji wa Sh. triloni 1.4.

Alisema benki hiyo pia inajivunia kupanua wigo wa upatikanaji wa huduma za kifedha kupitia njia mbadala na kuchochea ukuaji wa kiuchumi.

Ikiwa na CRDB Wakala zaidi ya 25,000, na huduma mbadala za kidijitali ikiwamo SimBanking, SimAccount, pamoja na ATM za kubadilisha fedha, asilimia 93 ya miamala ya Benki ya CRDB inafanyika nje ya tawi.

Kutokana na ufanisi huo, mwaka 2021 faida halisi ya Benki ya CRDB ilipanda hadi Sh. bilioni 268 kutoka Sh. bilioni 36 pekee mwaka 2017 huku faida ya jumla ya miezi tisa ya kwanza ya mwaka huu 2022 wa ikifika Sh. bilioni 257.

Benki hiyo imerekodi amana za Sh. trilioni 7.672 hadi robo ya tatu ya 2022 kutoka Sh. trilioni 4.326 zilizosajiliwa mwishoni mwa 2017.



Mwenyekiti wa Bodi ya CRDB, Prof. Neema Mori (wa pili kushoto) na Mkurugenzi wa CRDB, Abdulmajid Nsekela (kulia), wakiwa pamoja na Mkurugenzi wa IFC anayesimamia ushirikiano na Taasisi za Fedha Duniani, Tomasz Telma (wa pili kulia) na Mwakilishi Mkazi wa IFC nchini, Frank Ajilore (kushoto) walipokutana kujadili ushirikiano baina ya taasisi hizo jijini Washington, Marekani juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Celebi kuendelea kuvutia wawekezaji usafiri anga

**Na Maulid Mmbaga**

KAMPUNI ya Celebi Tanzania imeahidi kuendelea kuvutia wawekezaji wa kigeni kwenye sekta ya usafiri wa anga, pamoja na kutoa fursa ya ajira na mafunzo kwa Watanzania wanaofanyiakazi sekta hiyo ili kuhakikisha usalama wa watu.

Akizungumza na Nipashe juzi jijini Dar es Salaam, wakati wa hafla iliyowakutanisha wadau wa sekta hiyo, Mkurugenzi wa Celebi Tanzania inayotoa huduma za kwenye usafiri wa anga, Gaudence Temn, alisema kampuni hiyo inalenga kukuza utendaji na kuleta mabadiliko katika sekta ya anga.

Alisema kutokana na jitihada za serikali za kuvutia wawekezaji ndani na nje ya nchi, wameweka mikakati ya kupambana na changamoto za utendaji katika utoaji wa huduma za usafiri wa anga, ikiwamo kuanzisha kitengo maalumu cha kutoa mafunzo endelevu kwa watendaji wa sekta hiyo.

"Hizi huduma katika viwanja vya ndege ni eneo ambalo linahitaji utaalamu wa hali ya juu, hakuna mhitimu yeyote ambaye ametoka chuoni ameiva kwa ajili ya kufanya kazi hizi, lazima kuwapika tena upya kwa kuwafundisha kwa vitendo," alisema

"Zinaweza kuonekana ni kazi nyepesi, lakini ukweli zinahitaji uangalifu wa hali ya juu na mafunzo maalumu kuhakikisha kwamba mfanyakazi anatoa huduma zake kwa njia ya usalama, asisababishe madhara yoyote kwa ndege, abiria na ndege kwa namna yoyote," alisema Temn.

Pia, alisema kuna baadhi ya vitu wanafunzi hawafundishwi shuleni na kutoa wito kwa wahusika kuhakikisha wanafanya jitihada za kupata 'soft skill's' zitakazowasaidia katika utendaji kazi wao wa kila siku.

Aidha, alibainisha kuwa wako katika mkakati mkubwa wa kununua vifaa vitakavyowawezesha kuhudumia ndege katika viwanja wanavyofanyia kazi ili kuimarisha huduma na usalama katika usafiri wa anga.

Mwenyekiti wa Kamati ya Waendeshaji wa Mashirika ya Ndege nchini (AOC), Fadhili Karanja, alisema jambo kubwa wanaloliangalia ni kuhakikisha viwanja, ndege, wateja na wafanyakazi wanaotoa huduma za usafiri wa anga wanakuwa salama.

"Katika suala la usalama tunazidi kujifuza na kuongeza uelewa na tunaendelea kupiga hatua kulingana na kasi ya teknolojia, muhimu tutaendelea kusisitiza na kuhakikisha usalama wa wateja wetu, na kwenye vyombo vyetu," alisema Karanja.

# NMB yaanzisha ufunguaji akaunti ndani ya dakika 2

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB imezindua utaratibu wa kufungua akaunti kidijitali na kuanza kuitumia ndani ya dakika mbili.

Hatua hiyo inaongeza msukumo mpya katika jitihada za taifa za ujumuishwaji wa kifedha na upatikaji kiurahisi wa huduma za kidijitali za fedha.

Kwa mujibu wa Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara, Filbert Mponzi, sifa kubwa ya suluhisho la NMB Pesa Akaunti ni kuwa na mchakato mfupi wa kufungua akaunti mpya.

"Hii ni suluhisho la kusaidia kutatua changamoto za kifedha ambazo si tu ni akaunti inafunguliwa hapo hapo mteja alipo, bali pia ni nafuu kwa sababu haina gharama nyingi kama ada za mwezi," alisema.

Pia alisema pindi usajili wa mteja mpya unapokamilika, akaunti yake itafunguliwa mara moja na kuanza kutumika moja kwa moja wakati huo ikiruhusu upatikanaji wa huduma zote za msingi kama ile ya NMB Mkononi.

Alisema moja ya malengo makubwa ni kuwakwamua Watanzania walio nje ya mfumo rasmi wa kibenki, NMB ikiitambulisha sokoni huduma hiyo ya kufungua akaunti kidijitali kwa kasi zaidi nchini kwenye stendi ya mabasi yaendayo mikoani ya Magufuli.

Mponzi alimwambia, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla kuwa ufunguaji huo mpya wa akaunti unafanyika mahala popote na hauhusishi karatasi ya aina yoyote mfunguaji haitaji kwenda wala kufika kwenye matawi yao.

Makalla alisema ni fursa kwa Watanzania wote kuwa na akaunti ya benki.

Mponzi alisema huduma hiyo ni muhimu hasa kwenye maeneo ambayo upatikanaji wa huduma za kifedha bado ni mdogo na wenye akaunti za benki ni wachache.

Kwa sasa NMB akaunti zaidi ya milioni tano na kila ziku zaidi ya 3,000 zinafunguliwa.

"Sote ni mashuhuda kuwa ulimwengu sasa unaelekea kuwa wa kidigitali kwa karibu kila jambo, na kwa hilo Benki ya NMB imekuwa ikipambana kila mara kuibuka na suluhisho la kidigitali ambalo litazidi kurahisisha utoaji huduma zetu lakini kuzifanya pia ziwe bora zaidi kwa wateja wetu.

"Benki ya NMB imekuwa ikitumia teknolojia kutoa huduma za viwango vya kimataifa kwa wateja wake. Tumeanzisha ufunguaji huu mpya wa akaunti kidijitali ili kukuza zaidi ujumuishwaji na uwezeshaji wa Watanzania ambao bado wako nje ya mfumo rasmi wa kibenki," alisema.

Aliongeza kuwa NMB Pesa Account pia itawawezesha wateja kuweka na kutoa fedha kwa NMB Pesa Wakala pamoja na kufanya malipo kwa njia ya LIPA Mkononi.

Mponzi alibainisha kuwa mwaka 2022 ulipoanza, lengo la NMB lilikuwa ni kufungua akaunti mpya milioni moja. Mpaka juzi, walikuwa wamefungua akaunti 1,012,344.

"Hii inamaanisha kwa siku moja tu NMB tunafungua akaunti mpya 3,135. Ndio maana halisi ya huduma za kifedha jumuishi Tanzania," alitamba.

Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Heri James, alisema uzinduzi wa NMB Pesa Akaunti utasaidia ustawi wa biashara na uchumi wilayani humo na Tanzania kwa ujumla.



Waziri wa Fedha na Mipango, Dkt. Mwigulu Nchemba akiteta jambo na Balozi wa India nchini Tanzania Binaya S. Pradhan, aliyeongoza ujumbe wa wawekezaji katika sekta ya bima kutoka nchini mwake walioonesha nia ya kuwekeza katika sekta hiyo nchini walipokutana na kufanya mazungumzo katika Ofisi Ndogo za Wizara ya Fedha na Mipango, Jijini Dar es Salaam jana.**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Samia aridhia ekari 5,113 kupewa wakazi Morogoro

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan ameridhia ekari 5,113 kupewa wakazi wa eneo la CCT, Kata ya Dakawa wilayani Mvomero, mkoani Morogoro na kuwataka wanaoendelea kuingia kwenye hifadi kuondoka.

Tamko hilo la Rais Samia kuridhia lilitolewa jana na Kamati ya mawaziri wanane wa kisekta kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika katika eneo hilo.

Kamati hiyo inayoongozwa na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, ilisema wakazi hao awali walivamia eneo hilo ambalo ni hifadhi ya msitu wa kuni.

"Tumuheshimu Mheshimiwa Rais kwa huruma yake hii ya kuwapa eneo kwa sababu nyinyi ni wavamizi wa msitu wa kuni na mlitakiwa kutoka wote, ila mmepewa ekari 5,113 ili muweze kujenga makazi yenu," alisema Ndaki.

Aidha, Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ridhiwani Kikwete, alimtaka Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Morogoro kuwapanga wakazi hao katika eneo lililoruhusiwa ndani ya siku 90.

Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja, amewataka wananchi waliovamia eneo ambalo halipo katika aliyoyatoa Rais waondoke na kuwataka kutoendelea na ujenzi katika eneo ambalo ni la hifadhi ya msitu huo ili kuepuka kubomolewa makazi yao.

Nao wakazi wa eneo hilo, wamepokea kwa mikono miwili na kumshukuru Rais kuwagawia eneo hilo ili waweze kuendelea na ujenzi katika eneo lililoruhusiwa.

# Wataka mkataba kuruhusu meli kumwaga maji baharini

**Na Beatrice Moses**

TANZANIA imetajwa kuwa miongoni mwa nchi ambazo hazijaridhia mkataba wa mazingira unaohusu umwagaji wa maji yanayowekwa kwenye meli ili kuweka mlinganisho wa uzito inapokuwa haina mzigo.

Maji hayo yanatajwa kuwa ni mojawapo ya vyanzo vya uharibifu na hatarishi kwa viumbe hai vya baharini na kupaswa kumwagwa kwa uangalizi maalum ili kulinda usalama wa mazingira ya bahari husika.

Mkurugenzi wa Usalama na Mazingira Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi Sekta ya Uchukuzi, Stella Katondo, akizungumzia umuhimu wa mkataba huo alisema, nchi inaporidhia inautekeleza kwa taratibu zilizowekwa ikiwamo kuyachakata maji kabla ya kumwagwa.

"Tumekubaliana na tumehimizana kuharakisha michakato, ili tuweze kuridhia na tuandae kanuni za utekelezaji kwa wenye meli wakifika wazingatie kanuni, lengo ni kuwa na mazingira salama ya bahari," alisema.

Katondo alisema hayo jana baada ya kumalizika kwa mafunzo ya uelewa kuhusu kusimamia umwagaji wa maji yanayotumika kwenye meli katika maeneo ya bandari. Mafunzo hayo yametolewa na Shirika la Bahari la Kimataifa (IMO).

Katondo alisema umwagaji maji unasimamiwa kwa kuwa yanakuwa na viumbe hai, ikiwamo mimea na wanyama ambavyo vipo tofauti kule vinapotoka, hivyo huwa vamizi na wanaweza kuwala au kuwashambulia viumbe wenyeji au hata kuambukiza sumu hatari.

"Kama samaki tunaokula wakikutana na hawa viumbe vamizi wanaweza wakabadilika, wakapata sumu, wanaweza wakaliwa wakapotea kwa hiyo madhara hayo ndiyo shirika limeona ni vyema kuyasimamia," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC), Kaimu Mkeyenge, alisema kuwa kuna umuhimu wa kuridhia mkataba huo ili kuendelea kuimarisha usalama wa mazingira ya bahari nchini.

"Kuna umuhimu wa kuridhia mkataba huu, kwani kutoridhia unakuwa una meno ya kutekeleza yaliyomo, kwa sasa tunachofanya ni kuwashauri meli zinazoingia nchini kuhakikisha wanamwaga hayo maji kwa umbali wa maili 200 kutoka kwenye maji ya nchi kavu ili isiathiri yanayotumika kwenye uchumi wa nchi ikiwamo uvuvi," alisema Mkenyenge.

Alisema maendeleo endelevu ya bahari ni muhimu katika kukuza uchumi wa buluu na kukubali mkataba huo pia ni kuunga mkono hatua ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kuunganisha nchi katika kufanya kazi ipasavyo na mashirika ya kimataifa, hivyo kufikia malengo ya kimaendeleo yaliyowekwa. Alisema Tanzania imetumia vyema nafasi ya mafunzo hayo yaliyohusisha nchi 15 za Afrika, imeomba mafunzo mengine kwa IMO, ikiwamo ya kujikinga na ajali za majini zinazoweza kuzuilika.


FOMU YA MIRATHI-2
JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA
Katika Mahakama ya Mwanzoya Wilaya ........
Kituo cha Mjini
Mkoa wa Mjini

Usimamizi wa Mirathi Na. 91/2022

KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHENU
HADIJA MOHAMED WA MWEMBESONGO KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA MOHAMED RAMADHANI

TANGAZO

(Kanunu ya 5 (2) kanuni za usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 20/ Mwezi 12 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Zingatia;
Endapo kuna yeyeto mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
* Wosia wa Marehemu huyu upo Mahakamani na waweza kukaguliwa
* Marehemu hakuacha wosia
* Futa isiyohusika

Imetolewa leo tarehe 12 mwezi 12 mwaka 2022




KUPOTEA KWA VYETI



**GRACE AMADEO MWANKULUSI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne, Chenye namba **S3140-0017** kilichotolewa na Baraza la Mtihani wa Taifa kwa mtihani wa mwaka 2010. katika shule ya **NZONDAHAKI SECONDARY SCHOOL.** Pamoja na cheti cha Chuo Chenye namba **BTCSS.07/12/T.152** kilichotolewa na **TANZANIA PUBLIC SERVICE COLLEGE** mwaka **2013.** Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya Polisi namba **MB/RB/32/2011.**

ANATAFUTWA



Ndugu **Mariam Hussein Lindwe** pichani anatafutwa na polisi Kwa tuhuma za kujihusisha na vitendo vya kinyume na maadili na Wizi wa kuaminiwa, Taarifa imeripotiwa polisi **No. BUG/RB/1245/2022, Tarehe 12/4/2022** yeyote mwenye taarifa zake anaombwa atoe taarifa polisi kituo cha karibu nae. Donge nono litatolewa kwa atakayemuona

KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**SAIMON MAZIKU ELIAS**

Anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC. 915 CJA** aina ya **TVS**. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake. Taarifa ya Polisi. **KAH/RB/718/2022.**

# DIAMOND AWEKA REKODI MPYA



NYOTA wa muziki wa Bongofleva, Naseeb Abdul maarufu Diamond Platnumz ameweka rekodi mpya kwenye jukwaa la kimataifa la video la Youtube.

Diamond ameibuka kuwa msanii wa kwanza kutoka Kusini mwa Jangwa la Sahara kufikisha watazamaji bilioni mbili kwenye mtandao wa YouTube.

Hadi Alhamisi ya Desemba 15, video za mwimbaji huyo zilikuwa zimetazamwa mara bilioni mbili.

"Diamond Platnumz amepitisha jumla ya views bilioni mbili kwenye YouTube. Yeye ndiye msanii wa kwanza wa Kusini mwa Sahara kufikisha hatua hii," ilisema lebo ya WCB kupitia mtandao wa Instagram.

Bosi huyo wa WCB ameorodheshwa miongoni mwa wasanii bora wa Bara la Afrika kwa kuzingatia talanta, mafanikio na hata utajiri.

Wengine kwenye orodha hiyo ni pamoja na Burna Boy, Davido, Wiz Kid na Fally Ipupa.



## SHUSHO AFUNGUKA KUHUSU HARMONIZE

MWIMBAJI wa nyimbo za Injili, Christina Shusho, amevunja ukimya kuhusu kitendo cha msanii wa Bongofleva, Harmonize kubusu miguu yake.

Wawili hao walikutana jijini Eldoret nchini Kenya na Harmonize alipiga magoti na kuibusu miguu ya Shusho kwa furaha huku akimtaja kama mtumishi wa Mungu mmoja ambaye ni wa kweli kuwahi kutokea.

Na Shusho ameamua kufunguka kuhusu hilo na kumtaja Harmonize kuwa kijana mwadilifu anayeipambania sanaa ya Tanzania.

Alisema hivi karibuni atafunguka kwa kina kiini cha mazungumzo yao ambayo walikuwa nayo baada ya kukutana wote Kenya, japo kuwa kila mmoja alikuwa kwenye shoo yake.

"Nikiwa Kenya kwenye huduma nilifurahi kukutana na Mtanzania mwenzangu naye kaja kupeperusha bendera ya Tanzania. Tuliyoyaongea na Harmonize ni stori ya siku nyingine. Mungu akubariki mwanangu," aliandika Shusho.

Harmonize kwenye chapisho hilo alimshukuru mwimbaji huyo kwa kuwa kielelezo bora huku akimtakia Mungu kumfunika kwa damu yake.

## JOKETI AACHIA PICHA ZA UJAUZITO



KWA mara ya kwanza tangu ilipofahamika kwamba ni mama kijacho, Mkuu wa Wilaya ya Temeke, DC Jokate Mwengelo, ameachia picha zake za ujauzito na kuwapagawisha wengi wakiwamo mastaa kedekede nchini Tanzania.

Jokate ambaye wengine humuita Jojo au Kidoti ameachia picha hizo kwenye kurasa zake za mitandao ya kijamii na kuandika:

"Hakutakuwa na mwanamke yeyote atakayepoteza mimba wala kuwa tasa katika nchi yenu. Nami nitawajalia maisha marefu. Kutoka 23:26.

Kabla ya kuteuliwa kuwa Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe na baadaye kuhamishiwa Wilaya ya Temeke, Jokate alikuwa nyota wa mitindo, muziki, filamu, utangazaji na mrembo maarufu kwenye mitandao ya kijamii.

# TFF YAZIONYA KLABU USAJILI DIRISHA DOGO

**Na Adam Fungamwangwo**

SHIRIKISHO la Soka Nchini (TFF), limezionya klabu zote zinazofanya usajili kwa ajili ya kuboresha vikosi vya kipindi hiki cha dirisha dogo kuwa makini, kufanya usajili na uhamisho kwa wakati na kuacha tabia ya kusubiri hadi dakika za mwisho ndiyo kuanza kukimbizana na muda.

TFF pia imesema klabu itakayosajili mchezaji mwenye mkataba na klabu nyingine, na mchezaji atakayesaini klabu mbili kwa wakati mmoja, kanuni zitafuata mkondo wake, huku ikishauri kuwa hili ni dirisha la kuboresha na kuimarisha vikosi na si kusajili kikosi kizima.

Shirikisho limesema hayo kufuatiwa kufunguliwa kwa dirisha dogo la usajili jana saa sita ya usiku, ambapo klabu za Ligi Kuu Tanzania Bara, Ligi ya Wanawake, Ligi ya Championship na Ligi Daraja la Kwanza zitaruhusiwa kufanya usajili na uhamisho kwa wachezaji, zoezi ambalo litafanyika kwa kiasi cha mwezi mmoja hadi Januari 15, mwakani.

"Dirisha la Usajili, Ligi ya Wanawake, Championship, Ligi Daraja la Kwanza, linachukua mwezi mmoja hadi Januari 15, timu zinafanya usajili, pamoja na uhamisho, yoyote anayeona kuna maboresho au kuimarisha kikosi chake, basi ni wakati wake huu.

Dirisha dogo ni wakati wa kuongeza nguvu au kuimarisha kikosi, siyo wa kusajili kikosi kizima, tumeshatoa semina ni jinsi gani usajili huu unatakiwa kufanyika mwanzoni mwa msimu mameneja waliitwa, naamini kwa kipindi hiki chote hakutakiwa na changamoto yoyote katika eneo hilo la kusajili," alisema Ofisa Habari na Mawasiliano wa TFF, Cliford Ndimbo.

Hata hivyo alisema wanatoa nafasi kwa klabu yoyote itakayopata changamoto wakati wa kusajili au kuhamisha mchezaji kuwasiliana na TFF ili kutatua changamoto.

"Tunatoa nafasi kwa klabu yoyote ikipata changamoto wakati wa kusajili au kuhamisha mchezaji, basi wawasiliane na TFF ili kuhakikisha changamoto zao zinatatuliwa kabla ya dirisha kufungwa.

Dirisha ni mwezi mmoja, klabu zitumie muda vizuri, waache ule mtindo wao wa kusubiri hadi siku za mwisho ndiyo wanaanza kuhangaika kufanya usajili, muda unaruhusu na zile klabu ambazo zitasajili wachezaji ambao bado wana mikataba na wachezaji watakaosaini mara mbili, bahati nzuri kanuni zipo wazi na zitahusika kuwahukumu," alisema.



Baadhi ya wadau wa kupinga rushwa ya ngono Tanzania, wakicheza muziki kabla ya kuanza mkutano wa kitaifa wa kuweka mikakati ya kupambana na rushwa hiyo jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# *Kipa Mtibwa aanza mazoezi mepesi*

**Na Shufaa Lyimo**

GOLIKIPA wa Mtibwa Sugar, Mohamed Makaka, ameanza mazoezi mepesi baada ya kukaa nje kipindi kirefu kutokana na jeraha la kuvunjika mkono.

Akizungumza na gazeti hili jana daktari mkuu wa timu ya Mtibwa, Laurent Francis amesema mchezaji huyo ataanza kucheza rasmi mwezi ujao.

"Licha ya kuwa ameanza mazoezi mepesi bado kuna kipimo cha mwisho ambacho atafanyiwa wiki ijayo ili tujue kama mwezi ujao ataweza kukaa langoni," alisema Francis.

Daktari huyo alisema hali yake kwa sasa inaendelea vizuri tofauti na ilivyokuwa kipindi cha nyuma.

Kwa upande wake kocha mkuu wa timu hiyo, Salum Mayanga alisema malengo yake ni kushika nafasi ya tano kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu.

"Malengo yangu ni kutoka kwenye nafasi tuliyoko na kupanda juu mpaka nafasi ya tano, hakuna linaloshindikana kama tukiendelea kushirikiana," alisema Mayanga.

Alizungumzia mchezo wao wa leo dhidi ya timu ya Namungo kuwa wamejipanga vema kupata pointi tatu kwenye uwanja wao wa nyumbani.

"Tunamheshimu mpinzani wetu hivyo tutaingia kwa tahadhari kuhakikisha hatuupotezi mchezo huo," alisema.

## Zimamoto haijajitoa kwenye ubingwa

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Zimamoto imesema bado haijajitoa katika mbio za ubingwa wa Ligi Kuu ya Zanzibar msimu huu licha ya mchuano kuwa mkali.

Akizungumzia na gazeti hili Kocha Mkuu wa timu hiyo, Mohammed Ali Hilali "Tedy", alisema wanaendelea kukiimarisha kikosi chao kuelekea mzunguko wa pili wa ligi na lengo lao ni kuhakikisha wanatwaa taji la Ligi Kuu ya Zanzibar msimu huu.

Alisema ana matumaini makubwa ya kutwaa taji hilo kwa kuwa ana kikosi kizuri kinachoweza kupambana na kufanikiwa ndoto ya timu hiyo kwa msimu huu. Alisema anajua takribani timu tano zote zinautaka ubingwa wa ligi hiyo, lakini na wao hawapo nyuma kuhakikisha lengo lao linafanikiwa baada ya kulikosa msimu uliopita.

"Tunamatumaini makubwa ya kuunyakuwa ubingwa msimu huu, kwani tunakikosi kizuri ambacho naamini kitatuwezesha kufanya vizuri," alisema.

Aidha, akizungumzia juu ya kuboresha kikosi chake katika kipindi hiki cha usajili mdogo, alisema wamepanga kusajili wachezaji wawili ambao ni nafasi ya ulinzi pamoja na ushambuliaji.

Zimamoto ipo nafasi ya sita katika msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar ikiwa na alama 23 huku katika michezo 15 ya mzunguko wa kwanza imeshinda michezo saba, ikitoka sare miwili na kupoteza sita.

## Filamu 25 za Maisha Magic Bongo zawania tuzo za TAFFA

**Na Mwandishi Wetu**

IKIWA ni msimu wa pili wa tuzo za filamu za TAFFA (Tanzania Film Festival Awards) zinazoandaliwa na Bodi ya Filamu Tanzania, zaidi ya filamu 25 zinazopatikana katika chaneli za Maisha Magic Bongo zimefanikiwa kuchaguliwa kuingia katika mchakato wa mwisho wa kuwania vipengele mbalimbali katika tuzo hizo kwa mwaka huu.

Tuzo hizo zinatarajiwa kufanyika Jumamosi ya Desemba 17, mwaka huu, katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha AICC jijini Arusha huku lengo kuu likiwa ni kuleta mapinduzi ndani ya tasnia ya filamu nchini.

Kwa mujibu wa ofisa uhusiano wa Dstv, Grace Mgaya, wasanii wa filamu za Mwali, Jua Kali, Pazia, Yalaiti, Huba, Kitimtim na Sinia ndio wanaoongoza kuteuliwa kwenye vipengele vya kuwania tuzo hiyo.

Pia alisema filamu mpya za Still Okay to Date, Merchandizer nazo hazikuachwa nyuma.

Baadhi ya filamu na wahusika walioteuliwa kuwania vipengele mbalimbali katika tuzo hizi ni pamoja na mtunzi wa tamthilia bora ambapo wanashindanishwa, Azizi Mohamedwa Huba, Leah Mwendamseke wa Jua Kali na Mutran Tamimu wa Mwali.

## ZISIKUPITE

### OUNAHI AWINDWA

KLABU ya Leicester iko tayari kulipa kiasi cha euro milioni 45 kumnunua kiungo wa Morocco, Azzedine Ounahi kutoka klabu ya Angers, ingawa Barcelona pia wamekuwa wakimnyatia kiungo huyo mwenye umri wa miaka 22. (***L'Equipe***)

### RAMOS ATAKIWA MAN

MANCHESTER United wanatarajia kufanya uchunguzi kuhusu kupatikana wa mshambuliaji wa Benfica na Ureno, Goncalo Ramos mwenye umri wa miaka 21 ingawa kocha, Erik ten Hag ameambiwa kuwa hana uhakika mshambuliaji huyo atawasili Januari. (***ESPN***)

### CHELSEA KUACHANA NA NKUNKU

KLABU ya Chelsea haitazamii kuendeleza mipango yao ya kumsajili mshambuliaji wa Ufaransa, Christopher Nkunku mwenye umri wa miaka 25 kutoka RB Leipzig msimu wa joto, licha ya jeraha la mwisho wa msimu alilopata mshambuliaji wao wa Albania Armando Broja mwenye miaka 21. (***Fabrizio Romano***)

### VLAHOVIC KUONDOKA JUVE

KUNA "uwezekano mkubwa" mshambuliaji wa Serbia, Dusan Vlahovic mwenye umri wa miaka 22 akaondoka Juventus mwaka 2023, huku dirisha la Januari likitarajiwa kuamua uwepo wake. Chelsea ni miongoni mwa klabu ambazo zinawasiliana na wakala wake. (***Ben Jacobs, Twitter***)

### MOUKOKO ANAVUTIWA

CHELSEA wanakabiliwa na ushindani kutoka kwa Manchester United na Liverpool kumnunua Youssoufa Moukoko wa Borussia Dortmund, lakini klabu zinazovutiwa zitalazimika kumshawishi mshambuliaji huyo wa Ujerumani mwenye umri wa miaka 18 kwamba hatosajiliwa kukaa benchi. (***Mirror***)

### KOCHA KUMSHAWISHI MOUKOKO

KLABU ya Borussia Dortmund inatumaini uhusiano wa Youssoufa Moukoko na kocha Edin Terzic utasaidia kumshawishi fowadi huyo, ambaye mkataba wake unamalizika msimu ujao. (***Fabrizio Romano, Twitter***)

### GAKPO ATAKIWA MADRID

KLABU ya Real Madrid ina nia ya kumsajili fowadi wa Uholanzi, Cody Gakpo mwenye umri wa miaka 23 kutoka PSV Eindhoven ili kumrithi mshambuliaji wa Ufaransa, Karim Benzema, 34. (***AS***)

### FELIX APEWA OFA

MSHAMBULIAJI wa Ureno, Joao Felix mwenye umri wa miaka 23 anapewa ofa kwa klabu za Ligi Kuu ya Englanda wakati anataka kuondoka Atletico Madrid Januari, huku Manchester City, Manchester United, Arsenal na Aston Villa zikimnyatia . (***Mirror***)

### JOAU AGOMBEWA

KLABU za Manchester United na Arsenal zinaonekana kuwa chaguo zaidi kwa Joao Felix, huku Atletico ikiwa tayari kusikiliza ofa za zaidi ya euro milioni 100. (***AS***)

### HAG AAHIDIWA

KOCHA wa Manchester United, Erik ten Hag ameahidiwa fedha nyingi za kujenga upya kikosi chake - licha ya mipango ya familia ya Glazer kuiuza klabu hiyo. (***Sun***)

### DUMFRIES ATAKIWA MAN

KLABU ya Manchester United inataka kumsajili beki wa kulia wa Uholanzi, Denzel Dumfries mwenye umri wa miaka 26 kutoka Inter Milan, jambo ambalo litafungua milango kwa Barcelona kumsajili mlinzi wa kulia wa United, Diogo Dalot mwenye umri wa miaka 23. (***Sport***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# GRIEZMANN: KUCHEZA DHIDI YA MESSI NI TOFAUTI SANA

## ●●● Asema fainali itakuwa ngumu, kwa sababu Argentina ina mashabiki wengi...

**DOHA,** Qatar

KUCHEZA dhidi ya Lionel Messi katika fainali ya Kombe la Dunia ni "mpango tofauti kabisa", kwa mujibu wa Antoine Griezmann baada ya timu yake ya Ufaransa kufuzu fainali watakayokutana na Argentina Jumapili.

Ufaransa ilimaliza mbio za Morocco kwa ushindi wa 2-0 kwenye nusu fainali huku mabao ya Theo Hernandez na Randal Kolo Muani yakiwapeleka Les Bleus hao kwenye fainali ya pili mfululizo ya Kombe la Dunia.

Kikosi cha kocha Didier Deschamps kinaweza kuwa timu ya kwanza tangu Brazil mwaka 1962 kutwaa kombe la Dunia mara mbili mfululizo, baada ya kunyanyua ya kulitwaa mwaka 2018 nchini Urusi.

**Lakini waliosimama kwenye njia yao ni Argentina ya Messi, ambao waliifunga Croatia Jumanne na kutinga fainali ya sita ya Kombe la Dunia.**

Huku mechi ya fainali dhidi ya Ufaransa ikiwakilisha fursa ya mwisho kwa Messi kutwaa taji la Kombe la Dunia, Griezmann amekiri kwamba itakuwa kazi ngumu kucheza dhidi ya Argentina.

"Timu yoyote iliyo na Messi ni pendekezo tofauti kabisa," alisema Griezmann akiwaambia waandishi wa habari baada ya mechi.

"Mechi zote ambazo tumeona Argentina wakicheza, tunajua jinsi wanavyocheza - ni ngumu.

"Wanaonekana kuwa katika kiwango cha juu, sio Messi pekee - wana wachezaji wazuri sana.


"Tunajua utakuwa mchezo mgumu na wana mashabiki wengine."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,058,2

MECHI KALI
KAGERA SUGAR
VERSUS
AZAM
1 | 2.78
X | 2.26
2 | 1.83

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
airtel money
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# TEN HAG ASEMA KUUZWA KWA MAN KUTABADILISHA MAMBO

**MANCHESTER, England**

KUUZWA kwa Manchester United kutoka familia ya Glazer litakuwa jambo jema kwa klabu hiyo kwa mujibu wa kocha, Erik ten Hag.

The Glazers, ambao wamemiliki United tangu 2005, walitangaza mwezi uliopita kuwa wako tayari kuiuza klabu hiyo huku wakipanga "kutafuta mbinu mbadala".

Kumekuwa na shinikizo kwa Glazers katika miaka ya hivi karibuni, huku maandamano yakionekana mara kwa mara kutoka kwa mashabiki.

Huku United ikitafuta kushindana na uwezo wa kifedha wa Manchester City, pamoja na wamiliki wapya wa Saudi Arabia wa Newcastle United, Ten Hag anahisi uwekezaji mpya Old Trafford itakuwa habari ya kusisimua kwa klabu hiyo.

"Kutakuwa na uwekezaji zaidi unaowezekana ambao ni mzuri," alisema Ten Hag.

"Sisi (Ten Hag na Mkurugenzi Mtendaji Richard Arnold) tulizungumza juu ya utamaduni tunaotaka, tulizungumza juu ya malengo na utamaduni na alithibitisha kuwa hautabadilika.

"Itakuwa bora zaidi kwa sababu fedha nyingi zitapatikana kwa mradi huu."

Wamiliki wa Liverpool, Fenway Sports Group walithibitisha kuwa wanatafuta uwekezaji mpya Novemba, huku Chelsea ikichukuliwa na mfanyabiashara Mmarekani Todd Boehly mapema mwaka huu.

Ten Hag anaamini kuongeza uwezo wa kifedha wa United ni muhimu kwa kuwa wanatazamia kurejea kwenye jedwali la juu la soka la Uingereza, baada ya kubeba mataji matatu pekee tangu kuondoka kwa kocha, Alex Ferguson mwaka 2013.

"Kuna mabadiliko ya hali unapolinganisha (Ligi Kuu) na miaka mitano au 10 iliyopita," Ten Hag aliongeza.

"Newcastle wanakuja, hata West Ham, labda hawapo kwenye jedwali lakini wana uwekezaji mkubwa. Tottenham hakika na sihitaji kuzungumzia City na Liverpool au Chelsea.

"Unaweza kuhesabu kwa haraka klabu saba au nane ambazo zinaweza kushiriki ligi hii.

"Pia inahusu mkakati, sio fedha tu. Lakini ni wazi kwamba usipokuwa na wachezaji sahihi na wachezaji bora hautafanikiwa na kufikia malengo uliyojiwekea."

# Regragui: Morocco imeipaisha Afrika

**DOHA, Qatar**

KOCHA Walid Regragui ameipongeza Morocco kwa kuifanya nchi yao na Afrika kujivunia, lakini amekubali kwamba hawakuwa na uwezo wa kuifunga Ufaransa kwenye nusu fainali ya Kombe la Dunia.

Ikiwa ndio timu ya kwanza kufuzu nusu fainali ya kombe la Dunia, walikutana na kipigo cha mabao 2-0 na mabingwa watetezi Ufaransa wanaonolewa na kocha Didier Deschamps kwenye uwanja wa Al Bayt, Jumatano.

Mabao ya Theo Hernandez na Randal Kolo Muani yaliiwezesha Ufaransa kufuzu fainali na sasa watacheza dhidi ya Argentina, Jumapili.

Na Regragui amesema Morocco wameweka historia kwenye michuano



hiyo baada ya kuwatoa Ubelgiji, Hispania na Ureno.

"Tuligundua tumepata mafanikio makubwa tayari, tunajua kwamba vyombo vya habari vilituunga mkono, tuliona jinsi kila mtu alivyokuwa na furaha," alisema katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mechi.

"Tumekatishwa tamaa, tulitaka kuweka hai ndoto ya watu wa Morocco, tutalazimika kutafakari kushindwa huku. Tumefurahishwa na tulichofanikiwa, lakini tulihisi tungeweza kwenda mbali zaidi.

"Tulitoa taswira nzuri ya Morocco na Afrika, ikiwakilisha nchi yetu na bara letu, tulienda mbali tulivyoweza kwenye mashindano na hilo ni kubwa, lakini tutalazimika kufanya vizuri zaidi katika siku zijazo.

"Tunapaswa kufanya hivyo mara kwa mara ikiwa tunataka kuwa kwenye ramani ya soka. Huenda tusiwe wazuri kama Hispania, Brazil au England, lakini nataka kufuzu kwa kila mashindano."

## HABARI MICHEZO

211,696/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 17/12/22 | 19:30 | Aquila Montevarchi vs Rimini FC 1912 | 2.70 | 3.05 | 2.70 |
| 02. 17/12/22 | 19:30 | Olbia Calcio vs Lucchese Libertas 1905 | 3.00 | 3.10 | 2.42 |
| 03. 17/12/22 | 20:00 | SC Pisa vs Brescia Calcio | 2.34 | 3.15 | 3.10 |
| 04. 17/12/22 | 20:00 | Akritas Chlorakas vs Nea Salamina Famagusta | 2.95 | 3.25 | 2.36 |
| 05. 17/12/22 | 21:30 | Beitar Jerusalem FC vs Maccabi Netanya FC | 2.90 | 3.25 | 2.42 |
| 06. 17/12/22 | 22:00 | Estrela Amadora vs FC Penafiel | 2.48 | 3.20 | 2.80 |
| 07. 17/12/22 | 22:30 | Reggina 1914 vs SSC Bari | 2.36 | 3.05 | 3.15 |
| 08. 17/12/22 | 23:00 | Real Oviedo vs Sporting Gijon | 2.50 | 2.80 | 3.15 |
| 09. 18/12/22 | 07:00 | Western United FC vs Western Sydney Wanderers | 2.70 | 3.40 | 2.46 |
| 10. 18/12/22 | 13:30 | Bandirmaspor vs Pendikspor | 2.50 | 3.30 | 2.70 |
| 11. 18/12/22 | 14:00 | CD Atletico Baleares vs Real Murcia CF | 2.32 | 3.10 | 3.15 |
| 12. 18/12/22 | 14:30 | Turris Calcio vs Calcio Foggia | 2.75 | 3.05 | 2.65 |
| 13. 18/12/22 | 15:45 | AO Egaleo 1931 PAE vs Chania Kissamikos | 2.33 | 2.95 | 3.30 |
| 14. 18/12/22 | 16:00 | Cosenza Calcio vs Ascoli Calcio 1898 | 2.90 | 3.00 | 2.55 |
| 15. 18/12/22 | 16:00 | Modena FC vs Benevento Calcio | 2.41 | 3.10 | 3.00 |
| 16. 18/12/22 | 20:45 | Palermo FC vs Cagliari Calcio | 2.70 | 3.15 | 2.65 |
| 17. 18/12/22 | 21:00 | Burgos CF vs SD Huesca | 2.36 | 2.90 | 3.30 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

IJUMAA - 16/12/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 1950 | Ruvu Shooting vs Ihefu FC | 2.21 | 2.82 | 3.41 |
| 15:45 | 1830 | Haras EL Hodood vs Al Masry Club | 4.48 | 2.79 | 2.03 |
| 15:45 | 5028 | Ismaily SC vs Pyramids | 5.38 | 3.34 | 1.70 |
| 16:00 | 2825 | Bahir Dar Kenema FC vs Mekelakeya | 2.19 | 2.90 | 3.70 |
| 16:00 | 4136 | Mtibwa Sugar vs Namungo | 2.35 | 2.72 | 3.26 |
| 16:00 | 4549 | Marines FC Gisenyi vs Sunrise | 3.41 | 2.82 | 2.21 |
| 16:00 | 4674 | AS Kigali vs Gorilla FC | 1.44 | 3.85 | 6.82 |
| 16:00 | 4697 | Hapoel Afula vs Hapoel Acre | 2.77 | 3.22 | 2.51 |
| 16:00 | 4835 | El Fahem vs Hapoel Petah Tikva | 2.41 | 3.15 | 2.95 |
| 16:00 | 4864 | Bnei Yehuda vs Ahi Nazareth | 2.14 | 3.19 | 3.44 |
| 16:00 | 5770 | Hapoel Kfar Saba vs Ironi Hasharon | 2.02 | 3.25 | 3.75 |
| 16:15 | 4605 | PSS Sleman vs Psis Semarang | 2.72 | 2.97 | 2.53 |
| 16:30 | 1752 | Churchill Brothers vs Minerva FC | 2.17 | 3.25 | 3.01 |
| 17:00 | 1622 | Levadiakos vs Aris Salonica | 5.27 | 3.81 | 1.54 |
| 18:00 | 3364 | Al Raed Club vs Al Nasr Riyadh | 6.59 | 4.49 | 1.44 |
| 18:00 | 4256 | National Bank vs Zamalek | 4.99 | 3.39 | 1.73 |
| 18:30 | 5883 | ES Bafing vs Societe Omnisport | 2.97 | 3.07 | 2.28 |
| 19:00 | 1449 | Kagera Sugar vs Azam | 2.78 | 2.26 | 1.83 |
| 19:00 | 5822 | Ethiopia Electricity vs Hadiya Hosahina FC | 3.76 | 2.98 | 2.01 |
| 20:00 | 1241 | Al Ahly Cairo vs Coca Cola | 1.47 | 4.09 | 6.58 |
| 20:00 | 2356 | AEK Larnaca vs Omonia Nicosia | 1.98 | 3.40 | 3.70 |
| 20:00 | 2793 | Caykur Rizespor vs Goeztepe | 2.06 | 3.36 | 3.17 |
| 21:00 | 3709 | Denguele Sport vs LYS Sassandra | 2.54 | 2.93 | 2.74 |
| 21:00 | 5538 | Voluntari vs Farul Constanta | 3.67 | 3.08 | 2.07 |
| 21:30 | 4516 | Santa Clara vs FC Arouca | 2.73 | 3.12 | 2.42 |
| 21:30 | 4799 | CD Feirense vs Leixoes | 2.19 | 3.11 | 3.11 |
| 22:00 | 1561 | FC Eindhoven vs VVV Venlo | 1.96 | 3.55 | 3.40 |
| 22:00 | 2325 | Helmond Sport vs Den Bosch | 2.39 | 3.51 | 2.62 |
| 22:00 | 2480 | Telstar vs Maastricht | 1.71 | 4.04 | 3.94 |
| 22:00 | 3307 | Roda Kerkrade vs PEC Zwolle | 2.91 | 3.55 | 2.17 |
| 22:00 | 3339 | ADO Den Haag vs FC Oss | 1.56 | 4.15 | 4.94 |
| 22:00 | 4189 | NAC Breda vs Almere City | 2.66 | 3.45 | 2.38 |
| 22:00 | 4259 | De Graafschap vs Willem II Tilburg | 2.52 | 3.36 | 2.57 |
| 22:00 | 5430 | Heracles Almelo vs Dordrecht | 1.21 | 6.35 | 9.92 |
| 22:00 | 5896 | Jong Utrecht vs Jong AZ Alkmaar | 2.66 | 3.50 | 2.36 |
| 22:45 | 2454 | Ballymena Utd vs Larne | 7.79 | 4.29 | 1.35 |
| 22:45 | 2538 | Bala Town vs Gap Connahs Quay | 2.16 | 3.26 | 3.02 |
| 22:45 | 4856 | Flint Town United vs The New Saints | 12.70 | 6.84 | 1.14 |
| 23:00 | 2470 | Le Mans vs Orleans | 1.90 | 3.36 | 3.85 |
| 23:00 | 2875 | Birmingham vs Reading | 2.11 | 3.12 | 3.51 |
| 23:00 | 3604 | Aberystwyth Town vs Penybont | 3.79 | 3.69 | 1.77 |
| 23:00 | 3605 | Chateauroux vs Sedan | 1.78 | 3.46 | 4.26 |
| 23:00 | 4302 | Dunkerque vs Bourg Peronnas | 2.27 | 3.21 | 3.01 |
| 23:00 | 4531 | Tenerife vs FC Andorra | 2.16 | 2.97 | 3.57 |
| 23:00 | 4770 | Cholet vs Red Star | 3.84 | 3.35 | 1.90 |
| 23:00 | 5073 | Nancy vs FC Martigues | 2.21 | 3.16 | 3.16 |
| 23:00 | 5122 | Saint Brieuc vs Villefranche Sur Saone | 2.96 | 3.25 | 2.28 |
| 23:00 | 5290 | Concarneau vs Le Puy | 1.45 | 4.14 | 6.51 |
| 23:30 | 1796 | Porto vs FC Vizela | 1.26 | 5.98 | 9.37 |
| 23:30 | 2530 | GD Chaves vs Mafra | 1.94 | 3.60 | 3.60 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# NMB YAKABIDHI PIKIPIKI YA MASTABATA DODOMA

**Mwandishi Wetu, DODOMA**

MKAZI wa Kizota jijini Dodoma, Salum Rajabu amekabidhiwa pikipiki yake baada ya kushinda katika shindano la MastaBata Kote Kote linaloendeshwa na Benki ya NMB.

Rajab alikabidhiwa pikipiki hiyo jana na Meneja wa NMB Tawi la Kambarage jijini Dodoma, Emiliana Wilson ambaye alisema mshindi huyo alipatikana katika shindano la Mastabata Kote Kote lililoendeshwa wiki iliyopita.

Akikabidhi pikipiki hiyo, Emiliana alisema ushindi katika shindano hilo siyo tatizo gumu, bali siri yake ni kutumia MasterCard ya Benki ya NMB katika kufanya miamala.

Meneja alisema hadi jana shindano hilo ambalo linakwenda awamu ya tano, walishatoa zaidi ya Sh. milioni 100 kwa washindi 300 na hivi karibu walitoa pikipiki mbili na fedha kwa washindi.

"Shindano letu halibagui, tunashindanisha wateja wetu wote wanaotumia MasterCard, wapo wanaoshinda Sh. 100,000, wanaoshinda pikipiki na wengine mwanzoni mwa mwaka watashinda safari ya Dubai ambayo kila mshindi atakwenda na mwenza wake na kukaa huko kwa siku nne," alisema Emiliana.

Jana meneja huyo alichezesha shindano hilo kutokea Dodoma ambapo mshindi wa pikipiki alipatikana Shamsanga Samu kutoka Kimara huku Sia Rajabu kutoka Msasani akiwa miongoni mwa washindi 75 waliojishindia Sh. 100,000 kila mmoja.

Meneja Mwandamizi Idara ya Fedha na Uwezeshaji katika Biashara za Kadi kwa Benki ya NMB, Erick Emmanuel, alisema wataendelea kumwaga noti kwa washindi hivyo wajitokeze kushiriki. Emanuel alisema awamu zilizotangulia zimekuwa na mafanikio makubwa ambapo washindi wametoka kila kona ya nchi, hivyo mafanikio hayo yamepelekea kuanza kwa msimu wa tano ambao utaratibu wake ni kuchezesha shindano hilo kupitia matawi yake yote kwa zamu.

Akizungumza baada ya kukabidhi pikipiki yake, Salum Rajabu alisema hakutegemea kama angeshinda kwa kuwa hakuamini kama anafanya mashindano.

Rajabu alisema ni utaratibu wake kutumia Master Card kwa ajili ya kufanya miamala na kulipia huduma mbalimbali kupitia kadi yake.

"Kwamba ningeibuka mshindi hiyo sikujua, lakini sikujua kama nilikuwa nashindana ila napenda kutumia mfumo huu kwa sababu ni rahisi na salama zaidi, hivyo itakuwa jambo jema niseme kuwa tuendelee kutumia mafumo huu," alisema Rajabu.

Kuhusu ushindi alisema haubagui kwa kuwa ingekuwa hivyo, huenda hata yeye asingekuwa miongoni mwa washindi kwa kuwa hana uhusiano na wahusika zaidi ya akaunti yake ya benki anayoitegemea.




Meneja wa NMB Tawi la Kambarage, Emiliana Wilson (kushoto), akimkabidhi funguo na pikipiki, Salumu Jumanne (katikati) ambaye ni mshindi wa droo ya MastaBata KOTEKOTE. Makabidhiano hayo yalifanyika jijini Dodoma jana. Kulia ni Meneja Mwandamizi wa Fedha Kitengo cha Kadi NMB, Erick Emmanuel. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# YANGA YAKIRI IPO KUNDI GUMU CAF

INATOKA UK. 32

ya mzunguko wa pili wa ligi hiyo kufikia malengo yao.

"Malengo yetu makubwa ni kuhakikisha tunakusanya pointi kila mechi ili kuendelea na kampeni yetu ya kupata matokeo mazuri katika michezo iliyopo mbele yetu katika kufanikisha mbio za kutetea taji letu la ubingwa," alisema kocha huyo.

Alisema baada ya juzi kufanya mazoezi asubuhi na jana wamefanya jioni kwa sababu ya timu hiyo inaingia kambini tayari kwa mechi zilizopo mbele yao ikiwemo dhidi ya Polisi, Coastal Union na Azam FC kabla ya kwenda visiwani Zanzibar kushiriki kombe la Mapinduzi.

Yanga ambayo inaongoza kwa pointi 38 kwenye Ligi Kuu watashuka uwanjani kesho Jumamosi kucheza na Polisi kwenye uwanja wa Benjamin Mkapa.

# Michezo

Ijumaa Desemba 16, 2022

Nipashe




UKURASA 29

**Griezmann: Kucheza dhidi ya Messi ni tofauti sana**



Mchezaji wa Ufaransa, Theo Hernandez (wa pili kushoto), akifunga bao la kwanza wakati wa mchezo wa Nusu Fainali ya Kombe la Dunia dhidi ya Morocco kwenye Uwanja wa Al Bayt nchini Qatar juzi. Ufaransa ilishinda mabao 2-0 na kutinga fainali ya michuano hiyo na itacheza na Argentina Jumapili. **PICHA: MTANDAO**

# YANGA YAKIRI IPO KUNDI GUMU CAF

## Uongozi waweka mkakati kuimarisha kikosi, kesho kuwavaa Polisi kwa Mkapa...

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Yanga umekiri kuwa wamepangwa kundi gumu hivyo wanatarajia kuanza kampeni ya maandalizi kwa kuongeza nguvu kikosini kuelekea michuano hiyo itakayoanza kutimua vumbi Februari 10 na 11 mwakani.

Yanga ambayo ni mwakilishi wa Tanzania kwenye mashindano ya Kombe la Shirikisho imepangwa kundi D pamoja na TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, US Monastir ya Tunisia na Real Bamako ya Mali.

Mabingwa hawa watetezi wa Ligi Kuu Bara wataanza kutupa karata yao ugenini Februari 12 kwa kuwavaa US Monastir huku wakirejea nyumbani Februari 19 kuwavaa TP Mazembe kwenye uwanja wa Benjamin Mkapa.

Yanga itasafiri tena kwenda nchini Mali kuwavaa Real Bamako Februari 26 na kukamilisha mzunguko wa kwanza Machi 8 na itaanza mechi za mzunguko wa pili kwa kumenyana na Bamako Machi 19.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Makamu wa Rais wa Yanga, Arafat Haji alisema wakati benchi la ufundi likiendelea kuandaa timu na maandalizi kuelekea duru la pili na michuano hiyo, viongozi wanafanya majukumu ya kufuatilia wapinzani wao.**

Alisema wanajivunia kuwepo na wachezaji na kocha katika mataifa ambayo wanakwenda kucheza na itakuwa rahisi kwa kuanzia kwa sababu hawatakuwa wageni katika mataifa hayo.

“Tunatambua nchi zote tunazokwenda kucheza ni wenyeji kwa sababu ya baadhi ya wachezaji wetu na kocha Nasreddine Nabi wametoka mataifa hayo,” alisema.

“Kikubwa benchi la ufundi linaendelea kufanya kazi yao na sisi viongozi tunatekeleza yale ambayo anahitaji kocha ikiwemo kuwafuatilia wapinzani wetu na kuandaa mazingira ya mechi za ugenini ili kufikia malengo yanayotarajiwa,” alisema Arafat.

Alisema wanahitaji kufanya vizuri katika michuano hiyo kwa kusonga mbele kufuzu kucheza hatua ya robo fainali ya kombe la Shirikisho , kufikia huko lazima wajiandae kikamilifu.

Katika hatua nyingine kikosi cha Yanga kimeingia kambini jana jioni kwa ajili ya kujiandaa na mchezo wa mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Polisi Tanzania .

Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Cedric Kaze alisema baada ya mapumziko mafupi, jana waliingia kambini kujiandaa na maandalizi

INAENDELEA UK. 31

# Makundi Kombe la Mapinduzi hadharani

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KAMATI ya Kombe la Mapinduzi Zanzibar imetangaza makundi ya michuano hiyo itakayoanza kutimua vumbi Januari Mosi 2023.

Akitaja makundi hayo mbele ya waandishi wa habari jana, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Khamis Abdallah alisema michuano hiyo itashirikisha jumla ya timu 12 na kutakuwa na makundi manne.

Katika makundi hayo, Kundi A zipo timu za Azam FC, Malindi SC na Jamhuri, huku Kundi B, imezikutanisha timu za Yanga SC, Singida Big Stars pamoja na KMKM SC.

Kwa upande wa kundi C zipo timu za Simba SC, Mlandege FC pamoja na KVZ FC na kundi D zipo timu za Namungo FC, Aigle Noir pamoja na Chipukizi FC.

Aidha alisema kuwa mchezo wa ufunguzi wa michuano hiyo utakutanisha timu ya Mlandege dhidi ya KVZ mchezo utakaochezwa majira ya saa 10:15 katika Dimba la Amaan.

Na majira ya Saa 2:00 usiku kutakuwa na mchezo kati ya Malindi dhidi ya Jamhuri.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042